

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Saba – Tarehe 14 Novemba, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatuh Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**NAIBU SPIKA:** *Chief Whip.*

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):-**

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake wa Mwaka 1972 (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and their Destruction*) of 1972.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

**MHE. JORAM I. HONGOLI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):-**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake wa Mwaka 1972 (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and their Destruction*) of 1972.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizi wake wa Mwaka 1972 (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and their Destruction*) of 1972.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa niaba yake ambaye ni Makamu Mwenyekiti.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI  
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango.

**MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMAMI MKUU WA KAMBI  
RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:-**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

**NAIBAU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 85

**Ongezeko la Vijana na Akina Mama Wasiokuwa na Kazi**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA aliuliza:-**

Katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano kumekuwa na ongezeko kubwa la kundi la vijana na akina mama wasiokuwa na kazi hususan katika Majiji makubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na kadhalika:-

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu ongezeko hilo la akina mama na vijana wasiokuwa na kazi ambao wakati mwingine hujingiza katika vitendo vya kiuhalifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuwezesha kuongezeka kwa fursa za ajira na hivyo kupunguza tatizo la ajira hapa nchini, kama ifuatavyo:-

(i) Uwekezaji wa miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na usambazaji wa umeme vijijini; ujenzi wa barabara mijini na vijijini; na kusambaza maji mijini na vijijini. Miundombinu hiyo ni kichocheo cha ukuzaji uchumi na ukuzaji wa fursa za ajira hususan kwa vijana na akina mama;

(ii) Uwekezaji mkubwa katika mafunzo ya ufundi stadi na mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa vijana na akina mama kuwawezesha kujajiri, kupitia programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi;

(iii) Kuweka utaratibu wa kuwezesha vijana wasomi hususan waliomaliza mafunzo kwenye vyuo vya elimu ya juu na kati; kuanzisha makampuni kwa ajili ya kujajiri na kuajiri vijana wengine. Hadi sasa makampuni 36 ya vijana yameanzishwa kwa utaratibu huo ambapo makampuni 22 kati ya hayo yameunganishwa na Mamlaka ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma (*PPRA*) kwa ajili ya kupata upendeleo wa kupata zabuni Serikalini na kwenye taasisi za umma yakiwa kama makundi maalum;

(iv) Kuhakikisha akina mama na vijana wanaunda vikundi vya ujasiriamali ili kuititia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (*NEEC*) wawezeshwe mitaji kuititia mikopo iliyotolewa na Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, hasa Mifuko ya Maendeleo ya Vijana na Maendeleo ya Akina Mama;

(v) Serikali inaendelea kutengeneza fursa za ajira kuititia utekelezaji wa miradi mikubwa ambapo katika kipindi cha miaka miwili ya 2016/2017 na 2017/2018, jumla ya fursa za ajira 644,821 zimezalishwa;

(vi) Kusimamia utekelezaji wa sheria ya kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Majiji kwa ajili ya mikopo ya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu;

(vii) Kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini na urahisi wa ufanyaji biashara ili kuchochea uanzishwaji wa viwanda vingi zaidi vitakavyotoa ajira kwa nguvu kazi ya nchi yetu hususan vijana na akina mama; na

(viii) Kutenga maeneo maalum ya kilimo na biashara, kuititia Mamlaka za Mikoa na Wilaya ili vijana wengi na akina mama wapate maeneo ya kufanya shughuli za biashara na uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa wadau wote nchini kuendelea kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mipango na miradi mbalimbali ya kuongeza fursa za ajira kwani, suala la ajira ni mtambuka na siyo la Serikali peke yake. Jukumu kuu la Serikali ni kuweka miundombinu wezeshi kama niliyotaja awali ili wadau ikiwepo sekta binafsi wawekeze na kuongeza fursa za ajira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha, swalii la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, majibu yalikuwa marefu kweli kweli. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Serikali kupitia Bunge hili na ahadi za Chama cha Mapinduzi, mliahidi mtapeleka shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Mpaka sasa hivi hizi shilingi milioni 50 mmeshazipeleka katka vijiji vingapi? Wimbi hili la vijana na akina mama wengi wanaokimbilia kwenye haya majiji niliyoyataja wanatoka vijiji. Naomba kauli ya Serikali, ni vijiji vingapi mmepeleka hiyo shilingi milioni 50? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na hii michezo ya Bahati Nasibu ambayo inachezwa, inatangazwa na vyombo nya habari kupitia *TBC*, kwa mfano, Tatu Mzuka, Bikio na *SportPesa*. Michezo hili imekuwa ikilathiri sana vijana na akina mama, hawa wajasiriamali wadogo wadogo, hawataki kufanya kazi, yaani kila mtu anahangaika atafute pesa namna ganiacheze michezo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua katika michezo hii 25% inaingia Serikalini, je, ni kwa nini sasa Serikali msiweke utaratibu mzuri ili hii michezo inufaishe hawa vijana na akina mama kuliko sasa hivi ambapo inawaathiri sana hawa vijana na hawataki kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM suala la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji limezungumzwa na limewekwa kwa ajili ya kuchochea uchumi wa maeneo mbalimbali hasa vijiji kwa maana ya *ku-improve rural economy*. Mpango wa Serikali katika eneo

hili, kama ambavyo nilishawahi kutoa majibu hapo awali, ni kuhakikisha kwanza kabla hatujaanza utekelezaji wa ahadi hiyo, ile misingi na miundombinu yote muhimu inakamilika na baadaye ndiyo utaratibu uanze kutekelezwa kutokana na kwamba sasa tutakuwa tumeshaweka mazingira hayo wezeshi. Kama ambavyo tulipata *experience* katika mifuko iliyopita hasa Mfuko ule wa JK ambapo wahusika wengi hawakufikiwa, ndiyo maana dhamira ya Serikali imeona kwamba kwa sababu bado tuna mifuko mingi ya uwezeshaji, tunayo bado nafasi ya kuendelea kuwawezesha wananchi wetu kupitia mifuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ambayo inaratibu mifuko zaidi ya 42, lina ukwasi wa kiasi cha shilingi trillioni 1.3 ambazo ni mikopo na ruzuku kwa vikundi vya akina mama na vijana. Kwa hiyo, bado Serikali inayo nafasi ya kutekeleza ahadi hiyo na nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni sehemu ya llani ya Uchaguzi wa CCM na jambo hilo linaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili amezungumza kuhusu michezo ya kubahatisha. Rai na falsafa ya Serikali Awamu ya Tano ni kuwafanya Watanzania wote kupata vipato vyao kupitia kufanya kazi. Msisitizo mkubwa ni kufanya kazi. Kwa hiyo, wale wanaofanya michezo ya kubahatisha ni sehemu yao pia ya maisha, lakini kama Serikali, msisitizo mkubwa ni watu kufanya kazi, kujielekeza katika shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea rai ya Mheshimiwa Mbunge na tutatengeneza utaratibu mzuri ili makampuni haya ambayo yanafanya shughuli hii pia yafanye kazi ya kunufaisha wananchi kupitia utaratibu huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna mikakati wa kuwahamasisha hawa vijana na wanawake ambao hawana kazi wawe katika makundi. Tungependa kuona utekelezaji unaanza hapa Dodoma. Huu mji ni mchafu, unahitaji kufanyiwa usafi tuone utekelezaji wa hivyo vikundi vitakavyoweka Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya Serikali katika hali ya usafi. Anatoa kauli gani kuhusu hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ruth Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mikakati ya Serikali katika uwezeshaji wa vikundi vya akina mama na vijana ni pamoja na marekebisho yaliyofanyika kwenye miongozo ya Manunuzi ya Umma ili zaidi ya asilimia 30 ya zabuni za ndani za katika Halmashauri, Manispaa na Majiji zitumike kuwezesha vikundi hivi. Vikundi hivi vinafanya kazi katika ujenzi wa barabara, kusafisha barabara na kufanya masuala ya usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uzoaji wa taka katika eneo ambalo amelitaja la Dodoma, kwanza sina hakika na takwimu alizozisema kwamba Dodoma ni Mji mchafu sana, inawezekana kwa maono ya haraka haraka, lakini sasa hivi katika Miji ambayo inafanya vizuri katika eneo la usafi ni pamoja na Dodoma. Hivi sasa zipo Kampuni za Usafi ambazo ziko hapa na akina mama na vijana ndio wanaoshiriki moja kwa moja na wamepata ajira kupitia zoezi hilo la uzoaji wa taka katika Jiji la Dodoma. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, swali la nyongeza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na swali la msingi, kwa kuwa tatizo la ajira ni tatizo kubwa katika nchi yetu; na kwa kuwa wahitimu wa vyuo vikuu wamekuwa wengi na hawaajiriki na Serikali haina uwezo wa kuajiri; ni kwa nini Serikali isiimarishe Vyuo vya VETA katika maeneo mbalimbali ili vijana wetu wapate ujuzi ambao utasaidia katika hii dhana nzima ya viwanda? Je, Serikali inaweza kutoa msisitizo mkubwa kupeleka vijana katika vyuo hivyo badala ya kuwapeleka kwenye vyuo vikuu ambavyo hawaajiriki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, jibu swali moja maana ameuliza mawili. Jibu la kwanza tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu inatelekeza Mpango wa Ukuzaji Ujuzi ambao umeanza mwaka 2016 mpaka mwaka 2021 wenye lengo la kuwajengea ujuzi stahiki vijana wa Kitanzania ili wawe wana sifa za kuajirika na kuweza kuwaajiri vijana wengine. Katika mkakati huo, Serikali inachokifanya hivi sasa, tumeingia makubaliano na Chuo cha VETA na Chuo cha *Don Bosco*, navyozungumza hivi sasa, tumeanza kuwachukua vijana wote wale ambao wamehitimu Kidato cha Nne na Darasa la Saba tunawapeleka katika Vyuo hivi vya Ufundji ambapo Serikali inagharamia mafunzo yao yote. Mpaka ninavyozungumza hivi sasa, takriban vijana 8,952 wamenufaika katika awamu ya kwanza ya mafunzo haya na programu hii ni endelevu na tunategemea kuwafikia vijana milioni 4.4 ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba nasi tunafamu, katika farsafa ya uchumi wa vivanda huwezi kuendelea usipokuwa una nguvu kazi hii ya kada ya kati ambayo ndiyo muhimu sana katika *ku-drive* hiyo *economy*. Nasi kama Serikali tumeliona, tumelifanya kazi na programu hii inaendelea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Ahadi ya Mheshimiwa Rais Wilayani Malinyi**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 aliahidi kujenga majengo katika Makao Makuu ya Wilaya ya Malinyi kuititia Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) ambao unahusisha Ofisi ya Halmashauri, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na nyumba za watumishi, lakini hadi sasa hakuna dalili yoyote ya utekelezaji:-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi hii utaanza na kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** aliibusi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ya kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Majengo ya Ofisi za Halmashauri na nyumba za watumishi uliana mwaka wa fedha 2016/2017 na mpaka mwezi Juni, 2018 Serikali imeshapelekwa jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Halmashauri ambapo ujenzi wa msingi umekamilika na ujenzi wa ghorofa ya kwanza unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Septemba, 2018 Serikali imepeleka kiasi cha shilingi milioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, swal la nyongeza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri yenye kuleta tumaini kwa wakazi wa Malinyi. Pamoja na pongezi hizi, Wilaya ya Malinyi ni mojawapo ya Wilaya mpya zilizopo pembezoni zenye changamoto nyingi pamoja na majengo na miundombinu. Mkuu wa Wilaya pamoja na timu yake; watu kama nane hivi, wanafanya kazi katika vyumba viwili ambavyo vimefadhiiliwa na hospitali inayomilikiwa na taasisi ya dini ya KKKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira hayo, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana ambayo ni ngumu kupata tija. Nini *commitment* ya Serikali ndani ya bajeti inayokuja 2019/2020 kujenga na kumaliza nyumba ya Mkuu wa Wilaya ili aweze kupata nafasi ya kufanya kazi vizuri zaidi kama inavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, sambamba na changamoto inayompata Mkuu wa Wilaya na timu yake ya

watumishi pale wilayani, hali kadhalika wafanyakazi wa Halmashauri ambao wengi wametoka Wilaya nyingine wamekuja pale, wana changamoto kubwa ya kupata nyumba za kupanga. Mji ule ni mdogo, wengine inafikia hatua wanakaa pembezoni mwa ule Mji Mdogo na wengine wanakaa kwenye nyumba za wageni. Huu ni mzigo mkubwa kiuchumi na hata kicutendaji. Ni lini Serikali itaelekeza mashirika yake mawili haya; *National Housing Corporation* na *Watumishi Housing* yaweze kujenga nyumba za makazi kwa wafanyakazi wale? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la kwanza la nyongeza anataka kupata *commitment* ya Serikali juu ya suala zima la kuharakisha ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya. Katika jibu langu la msingi, nimeonesha *commitment* ya Serikali imipeleka jumla ya shillingi milioni 350 kwa kuanzia. Nachoomba ni Halmashauri kuhakikisha kwamba wanasmamia hizo pesa zitumike vile inavyotakiwa kwa uharaka ili baada ya fedha hizo kutumika tuone uwezekano wa kuweza kuongeza fedha nyingine ili kumalizia ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue fursa hii kuhimiza *TBA Tanzania* nzima ambao tumewapa mikataba ya kujenga nyumba za Wakuu wa Wilaya, Ofisi na Ofisi kwa ajili ya Wakuu wa Wilaya, wahakikishe kwamba jitihada zinaongezwa ili kuongeza kasi ya ujenzi wa majengo haya, yakamilike Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, anasema kwamba kuna wafanyakazi ambao wanatalazimika kukaa kwenye nyumba za wageni, wangehitaji wapate nyumba na angependa *commitment* kutoka Serikalini juu ya

*National Housing* kwenda kujenga kule. Kwanza, kwa wananchi wa Malinyi hiyo ni fursa. Ni vizuri kwanza wao wenyewe wakahakikisha kwamba wanajenga nyumba za kutosha ili hao wafanyakazi ambao wanahangaika sehemu za kupanga waweze kupanga katika nyumba hizo na wakaongeza kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *National Housing* kwa kadri itakavyoonekana kwamba inafaa, kwa sababu na wao wanakwenda sehemu ambayo wakienda kuwekeza inalipa; wakiona kama inafaa kwenda kuwekeza Malinyi, naamini watakwenda huko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Naibu Waziri wa TAMISEMI kwa majibu yake mazuri. Napenda kuongeza tu suala la ujenzi wa nyumba katika Halmashauri zetu kwa kutumia Shirika la *National Housing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *National Housing* wako tayari kujenga katika Halmashauri yoyote, nasi tulishatoa maelekezo kwenye Halmashauri zetu kwamba Halmashauri yoyote ilio tayari itoe *commitment* yake kwamba *National Housing* wanapokuja kujenga, wana uhakika wa nyumba siyo chini ya kumi na kuendelea zitachukuliwa na Halmashauri. Zile nyingine za ziada zinajengwa kwa ajili ya wananchi wengine wa kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *National Housing* wako tayari. Kinachotakiwa ni Halmashauri kuwa tayari na ardhi ambayo haihitaji kulipiwa fidia wala gharama zozote. Wao wakija, wanaingia makubaliano namna ya kulipana watakapokuwa wamekamilisha nyumba zao. Mkataba unakwenda mpaka miaka mitano kutegemeana na idadi ya nyumba ambazo wanachukua Halmashauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tabora Manispaa hakuna kabisa Ofisi ya Halmashauri na watu hao wanafanya kazi kupitia kwenye jengo la Mahakama ya Mkoloni; lakini Serikali ilishatupa pesa nusu tukaanza ujenzi miaka mitano iliyoleta na tumekuwa tukileta bajeti zetu kila mwaka ili tumalizie jengo lile ambalo halijamaliziwa. Je, ni lini sasa Serikali italeta pesa kumalizia Ofisi ya Tabora Manispaa ili nasi kama Manispaa tuweze kuwa na ofisi? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ujenzi wa ofisi kwa za Halmashauri ulishaanza. Pia ni vizuri tukafanya mawasiliano na Mheshimiwa Mbunge tukajua ujenzi huo umefikia kiwango gani na kiasi gani cha fedha ambacho kinahitajika ili kuweza kumalizia ujenzi huo? Ni ukweli usiopingika kwamba kwa Manispaa ya zamani kama Tabora inahitaji kuwa na ofisi kulingana na hadhi na heshima yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tukimaliza kipindi hiki cha maswali tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili tuone namna nzuri ya kuweza kuhakikisha ujenzi huu unakamilika kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa

Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

Na. 87

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Nyashimo – Dutwa**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI (K.n.y. MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI)** aliuliza:-

Wakati akiwa katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2015, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliahidi ujenzi wa barabara ya Nyashimo – Dutwa na ile barabara ya mchepuko kupitia Mkula Hospitali kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini ahadi hiyo muhimu ya Mheshimiwa Rais itaanza kutekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 Mkoani Simiyu alifanya mikutano katika Vijiji vya Mkula na Dutwa tarehe 12, Septemba, 2015. Katika mikutano hiyo, Mheshimiwa Rais aliahidi kuzijenga kwa kiwango cha lami sehemu mbili za barabara za mchepuo kwa Barabara ya Bariadi – Lamadi ambazo ni eneo la Mkula (kilometra 1.76) na Dutwa (kilometra 2.8). Aidha, Wizara yangu kupitia *TANROADS* tayari imeshajenga kilometra 1.18 ya eneo la Mkula; na katika mwaka wa fedha 2018/2019 imepanga kujenga mita 580 za eneo la

Mkula kukamilisha barabara hiyo na kuanza mita 800 za eneo la Dutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haina kumbukumbu kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya Nyashimo – Dutwa (kilometra 49) kwa kiwango cha lami. Ahadi iliyopo ni ya kuendelea kuiimarisha barabara hiyo kwa kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali. Hivyo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), Mkoa wa Simiyu itaendelea kuiimarisha kwa kiwango cha changarawe barabara ya Nyashimo – Dutwa (kilometra 49) kwa kuifanyia matengenezo stahiki ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudu kubwa za Serikali kwa sasa ni kutekeleza sera yake ya kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa na nchi jirani kwa barabara za lami ambapo kwa upande wa Mkoa wa Simiyu, Serikali imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Bariadi hadi Lamadi (kilometra 71.8) na sehemu ya Mwigumbi hadi Maswa (kilometra 50.3) na inaendelea na ujenzi wa kiwango cha lami wa sehemu ya Maswa – Bariadi (kilometra 49.7) ili kuunganisha Makao Makuu ya Mikao ya Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Mara na nchi za jirani za Kenya kwa barabara za lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuviweka lami vipande vya barabara vya Mkula na Dutwa. Barabara hii ya Nyashimo – Dutwa ni barabara muhimu sana kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Busega na Wilaya ya Bariadi na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema hawana kumbukumbu, naomba sana wakajaribu kuangalia kwa sababu hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais pia. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri waende wakaangalie vizuri na mwone ni kwa namna gani barabara

hii ya Nyashimo – Dutwa inaweza ikajengwa kwa kiwango cha lami ili isaidie wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuuliza swalii la nyongeza. Hali ya namna hii pia ipo kwenye Wilaya ya Maswa, barabara ile ya kutoka Njiapanda - Ikungu kwenda Malampaka, Serikali iliahidi kuanza upembuzi yakinifu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba, naomba uulize swalii tafadhali.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza swalii. Kipande cha barabara hiyo kutoka Njiapanda kwenda Malampaka ni lini sasa upembuzi yakinifu utakamilika ili ujenzi kwa kiwango cha lami uweze kuanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mashamba Ndaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza shukrani ambazo amezitoa Mheshimiwa Mbunge nazipokea kwa niaba ya Serikali. Niseme tu kwamba barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni barabara muhimu na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tumejipanga kuhakikisha barabara hii tunaiweka katika kiwango cha changarawe ili iweze kuitikika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga barabara kiwango cha lami siyo tu kwa kufuata ahadi za Mheshimiwa Rais, ipo mipango ambayo tumeiweka kwa ajili ya kujenga barabara za lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa eneo hili kwamba kwenye mipango yetu ya siku za usoni tutawenza kujenga barabara hii katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara inayotoka lkungu kwenda Malampaka ni kipande ambacho kinaunganisha kuja barabara hii ya kutoka Mwigumbi kwenda Maswa. Tunafahamu kwamba eneo hili kuna mpango wa kutengeneza eneo la hifadhi ya bandari kwa maana ya kuhifadhiya mizigo na kadhalika. Upo umuhimu mkubwa wa kutengeneza hii barabara katika kiwango cha lami ambacho kinastahili, kiwango cha lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira kwamba mipango yetu kwa siku za usoni hiki kipande hiki cha barabara tutakizingatia ili pia kiweze kuhudumia eneo hili la bandari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kama ilivyo kwa wananchi wa Busega, mwaka 2015 wananchi wa Korogwe walihidiwa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Korogwe - *Old Korogwe* – Dindira – Bumbuli - Soni kilometra 74. Nataka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini ahadi hii kwa wananchi wa Korogwe itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Timetheo Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli eneo hili la barabara hii Mheshimiwa Mbunge aliyoitaja kutoka Korogwe – Dindira -Soni ni barabara muhimu itaweza kwenda kutuunganisha na wenzetu upande ule wa Malamba. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili tuone kwenye mpango yetu imepangwa lini. Hata hivyo, zile hatua za awali tulishaanza, tunaitambua barabara hii ni muhimu. Kwa hiyo, tuwasiliane ili tuangalie kwenye mpango mkakati yetu *exactly* ni lini barabara ile tutaitengeneza? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Willy Qambalo, swali la nyongeza.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom na ile ya Karatu – Mang’ola – Matala - Mto Sibiti kwa kiwango cha lami uliahidiwa na viongozi mbalimbali wa nchi hii akiwemo Rais wa sasa. Je, ni lini sasa barabara hiyo itaweza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Qambalo, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na ahadi ya ujenzi wa barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba harakati za ujenzi zilishaanza kwa sababu ule usanifu wa barabara, hasa hiki kipande ambacho kinapita Karatu kandokando ya Ziwa Eyasi kule, usanifu ulishakamilika, tumeshatambua mahitaji muhimu ya kujenga barabara hii. Hicho kipande kingine cha barabara ambacho kinapita tena kutoka Mbulu kutokea kule Sibiti kupita Haydom, Mheshimiwa Mbunge pia anafahamu kwamba tunaendelea na usanifu na kuandaa michoro na kujua gherama za barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kifupi ni kwamba yale maeneo korofi ya Mto Sibiti ili tuungane sasa upande wa Karatu na wenzetu wa Simiyu, hivi karibuni kuna tenda itatangazwa kuongezea sasa kilometra 25. Kwa hiyo, ujenzi wa daraja unakamilishwa na kipande cha kilometra 25 kinatengenezwa. Baadaye sasa tukipata fedha tutajenga barabara muhimu sana kuunganisha Mkoa wa Manyara na mikoa ile ya jirani. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nyashimo – Dutwa kule Busega ina uhusiano sana na barabara mbili za Muheza. Nilitaka kujua, barabara ya Muheza – Amani kilometra 36 pamoja na Tanga – Pangani ambazo ziliahidhiwa na Mheshimiwa Rais pia zipo kwenye bajeti ya mwaka huu kwa kiwango cha lami, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami itaanza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Adadi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba tuko kwenye mpango wa kufanya matengenezo ya barabara hizi. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Adadi lakini nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga. Nampongeza Mheshimiwa Aweso pia amefuatilia sana hii barabara kutoka Tanga Mjini kwenda Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilihakikishie tu Bunge lako kwamba tunatangaza zabuni ya ujenzi wa barabara hii muhimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Balozi Adadi, Mheshimiwa Aweso na Wabunge wote tujue kwamba tunatangaza zabuni hii. Ombi langu kwa Mheshimiwa Aweso, maana anaafuatilia sana ili wawekezaji wengi waje Pangani, namwomba tu aendelee kuhamasisha wawekezaji waje kujenga eneo la Pangani ili kuinua uchumi wa Pangani na Tanga kwa ujumla. Sasa hii barabara tunaenda kuijenga na

tukianza Tanga ni mwendelezo wa barabara hii ambayo tutakwenda kujenga mpaka eneo la Bagamoyo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudzi za Serikali katika kujenga barabara mbalimbali katika Mitaa ya Jiji la Dar es Salaam, ambapo naipongeza sana ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini ninalo swali. Kwa kuwa Serikali imeahidi kujenga barabara ya Nzasa – Kilungule – Buza kwa kiwango cha lami kwa kupitia Mradi wa *DMDP*, ambapo ujenzi huo ungeanza rasmi katika mwezi Januari lakini mpaka sasa hakuna hatua zozote za awali zinazoendelea. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wahusika wa mradi huo ili waweze kutekeleza ahadi hiyo kwa haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikasema kwa ufupi tu kwamba, kama kuna mkandarasi amepewa kujenga barabara hii ya Nzasa – Kilungule, ni kauli ya Serikali kumwelekeza mkandarasi afanye ujenzi kulingana na mkataba ulivyo. Nitafuatilia ili kuona kuna changamoto gani ili tuweze kuzitataua kama zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba avute subira leo leo nitafuatilia njue kuna shida gani. Kwa sababu, ni nia ya Serikali kuhakikisha pale ambapo kuna mradi tunaanza kuujenga, mradi

ujengwe kwa kiwango, lakini ukamilike kwa muda kwa sababu wananchi wanasubiri kupata huduma. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Antony Calist Komu, Mbunge wa Moshi, Vijijini.

Na. 88

**Kupandishwa Hadhi Barabara ya Kutoka Getifonga –  
Mabogini – Chekereni - Kahe**

**MHE. ANTONY C. KOMU** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Gatefonga – Mabogini – Chekereni – Kahe mpaka Wilaya ya Mwanga ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro, lakini haipititiki kipindi cha mvua:-

Je, ni kwa nini Serikali haikubaliani na mapendekezo ya RCC Kilimanjaro ya kuipandisha hadhi barabara hiyo, kuwa chini ya *TANROADS*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Antony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Getifonga – Mabogini – Chekereni - Kahe mpaka Wilaya ya Mwanga ni barabara ya Wilaya chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliunda Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (*TARURA*) kuititia Sheria ya Wakala

wa Serikali Na.30 ya mwaka 1997 ili kusimamia kikamilifu barabara za vijiji na mijini. Aidha, kufuatia kuanzishwa kwa *TARURA*, Serikali imesitisha upandishaji hadhi wa barabara za wilaya kuwa barabara za mikoa. Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijiini na Mijini (*TARURA*) itaendelea kuifanya matengenezo barabara hiyo ili ipitike majira yote ya mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Calist Komu, swal la nyongeza.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza mswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa kilimo na kule kuna mradi mkubwa sana na wa kisasa wa *Moshi Lower Irrigation Scheme* wa mpunga na barabara pekee inayotumika kwa ajili ya kusafirisha bidhaa zinazotoka kule ni hii. Kwa kuwa kuna ule Mpango wa Awamu ya II wa Kuendeleza Kilimo Nchini (*ASDP II*) na kuna fedha kwa ajili ya kuboresha barabara za ndani ya ule mradi, ni kwa nini Serikali isikubali mimi, Mheshimiwa Mbatia ambaye anahusika vilevile, TAMISEMI na Wizara ya Kilimo tukakaa na kuona ni namna gani tunaweza kutumia sehemu ya fedha kutoka katika huo Mradi wa *ASDP II* ili kunusuru hii barabara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, naomba vilevile ndugu zangu Wizara ya Makamu wa Rais, Mazingira, tufuatane pamoja kwenda kwenye eneo hilo na kuona ni namna gani tunaweza tukabuni njia mbalimbali za kukabiliana na hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi na kukosekana kwa makinga maji ambayo kila wakati wa mvua kunatokea maafa makubwa na barabara hii kubadilika kuwa mfereji ili tuweze kuinusuru hiyo barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani yote mawili ni maombi. Kwa hiyo, kama umemkubalia kukutana, wewe mwambie uko tayari kukutana naye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Komu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri alikuwa anatoa ushauri, kama ulivyosema, lakini namwomba tu aongeze ushirikiano mzuri kwa sababu ziko *forum* mbalimbali ambao anaweza akazifanya ili kuweza kutatua changamoto ambazo zinaonekana. Hii ni pamoja na kuzungumza kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa, yale mapendekezo yakija, sisi kama Serikali, tuko tayari kuyachukua. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Owenya, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Moshi vijijini kuna barabara ya kutoka Kiboroloni - Kikarara – Tuduni, ambapo barabara ile ni ya kuitisha watalii kwa sababu kuna lango la kupandia mlima. Barabara ile imekuwa ikitolewa ahadi tangu 2005 na *TANROADS* wamekuwa wakiweka vibao kuwafanya wanancni waamini kwamba barabara ile inatengenezwa, lakini mpaka leo barabara ile hajifanyiwa upembuzi wowote ule. Nataka kupata jibu kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini barabara ile itaanza kukarabatiwa kwa kiwango cha lami kama ilivyokuwa imeahidiwa tangu enzi za Mheshimiwa Rais Kikwete na hatimaye kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Owenya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba eneo hili la Mkoa wa Kilimanjaro ni eneo ambalo muunganiko wake wa barabara uko katika *standard* ya juu ukilinganisha na maeneo mengine. Kwa sababu, barabara kuu za Kilimanjaro tumekamilisha kuziunganisha kwa asilimia 100 na barabara za mikoa ziko katika harakati...

**WABUNGE FULANI:** Zitaje.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Ni maeneo mengi, sio rahisi kutaja hapa, tunaendelea kuziunganisha barabara hizi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba alivyoliletta hapa naona kama eneo hili linaweza kuwa mahsus, nahitaji kultazama. Kwa hiyo, namuahidi tu kwamba, tutapata muda mzuri wa kuiona hii barabara na hayo maelezo aliyoynatoa kwamba mara nydingi kunawekwa vibao, nafikiri siyo utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo, nitapenda hili tulipate kwa undani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara zinapitika, lakini ni nia yetu pia kuhakikisha kwamba maeneo muhimu ambayo yanaweza kutusaidia kupata kipato kipitia utalii tunayaweka katika hali nzuri ili tuweze kuhamasisha na kupandisha uchumi wa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swalii la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba hata ukisoma kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, ambayo wanasema sasa hivi ndiyo inatekelezwa, lakini kuna baadhi ya maeneo utekelezaji

wake umekuwa wa kusuasua, hasa zaidi kwenye ujenzi wa barabara inayoanzia Masasi - Nachingwea - Ruangwa mpaka - Nanganga na hasa zaidi Masasi – Nachingwea yenyeye urefu wa kilometra 42 na inaunganisha katika Wilaya ya Masasi na Wilaya ya Nachingwea. Nataka awaeleze watu wa Masasi pia na Nachingwea, ni lini barabara hii itatengenezwa kwa kiwango cha lami kadiri ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Cecil Mwambe siku hizi anasoma sana Ilani ya Chama cha Mapinduzi baada ya kugundua ina mambo mazuri sana. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nampongeza tu Mheshimiwa Cecil Mwambe. Nafikiri tumuige tu kusoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi ili sisi kama Serikali tuweze kupata ushauri na kutekeleza dhahiri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara hizi alizotaja Mheshimiwa Mwambe, nafahamu Mheshimiwa Mwambe tumeongea mara nyingi na nafikiri atakubaliana nami kwamba hata yale madaraja muhimu ya kuunganisha kutoka upande wake kuja Nachingwea ujenzi unaendelea vizuri. Wananchi walikuwa na hatari nyingi, wanaliwa na mamba katika maeneo yale na tunaendelea kuboresha vizuri. Hata ushauri wake wa kuboresha uzito wa madaraja ambayo yanaendelea, tunasimamia kama Serikali. Kwa hiyo, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa ufupi kwamba, hiki kipande cha barabara cha Nachingwea kinachouganisha kuja Nanganga, kinanganisha eneo la Mheshimiwa Cecil, lakini pia kile kipande cha kutoka

Nanganga kuja Ruangwa kurudi Nachingwea barabara hizi zote ni muhimu sana na anafahamu tuko kwenye hatua nzuri ya kuanza ujenzi. Kwa hiyo, kwa sababu anafahamu hivyo sihitaji kusema sana lakini kwa ufupi ni kwamba, barabara hizi alizozitaja tumezitazama kwa macho makini kutokana na umuhimu wa uzalishaji katika maeneo haya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa, sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Hitaji la Kuweka Ruzuku katika Pembejeo zote**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali imekuwa na kigugumizi cha kuweka ruzuku katika pembejeo zote ili wakulima wote waweze kuzinunua kwa bei ya chini tofauti na ilivyo sasa ambapo mfumo huo unawanufaisha wachache?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Jimbo la Mombasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2003/2004 Serikali ilianza kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo, ikiwemo mbolea na mbegu bora kwa lengo la kuhamasisha wakulima kutumia pembejeo ili kuongeza uzalishaji, tija na usalama wa chakula nchini. Utaratibu huu wa ruzuku ulitolewa kwa mifumo mbalimbali ikiwemo vocha za pembejeo kwa wakulima na mikopo kwa vikundi vya riba nafuu. Aidha, hadi kufikia msimu wa mwaka 2013/2014 takribani kaya zaidi ya

milioni tatu zilinufaika na ruzuku ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha za pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo iliyokuwa inatumiwa na Serikali kuwafikishia wakulima pembejeo za ruzuku imekuwa na changamoto nyingi ikiwemo udanganyifu, pembejeo kutowafikia wakulima kwa wakati na kuwanufaisha wakulima wachache. Kwa kutambua changamoto hizo, katika msimu wa mwaka 2017/2018, Serikali ilianza kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (*Fertilizer Bulk Procurement System – BPS*). Aidha, mfumo huo una faida nyingi ikiwemo kuongeza upatikanaji wa mbolea kwa wakati, kupunguza bei za mbolea, pamoja na kutoa fursa kwa wakulima wote kununua na kutumia mbolea kwa kadiri ya uwezo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kufuta ada na tozo mbalimbali ambazo hazina tija kwa wakulima, ikiwemo tozo kwenye mbegu ambazo zitasaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kupunguza bei ya mbegu bora kwa mkulima. Aidha, katika mwaka 2017/2018 tozo saba zimefutwa na tozo tano zimefutwa katika mwaka 2018/2019 kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kupunguza bei ya mbegu bora kwa wakulima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Silinde, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jitihada za Serikali ambazo wameonesha katika majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amenijibu, ni kufuta tozo nyingi na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (*Fertiliser Bulk Procurement System*). Vilevile ukipitia kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi na yenyeewe inaonesha kabisa kwamba walikuwa na lengo la kusaidia kuongeza fedha za ruzuku kwenye pembejeo kwa

wakulima. Sasa niulize swalii dogo tu kwenye hili. Pamoja na llani ya Chama cha Mapinduzi kuzungumza, ni kwa nini Serikali inashindwa kutekeleza llani yake yenyewe kwa sababu bei ya pembejeo imekuwa ikipanda pamoja na jitihada zote hizo ambazo zimekuwa zikifanyika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili. Pamoja na kununua mbolea kwa bei ya jumla huoni kwamba mfumo wanaoutumia sasa wa manunuzi wa *bulk procurement* unasababisha gharama kubwa kwa Serikali. Mimi niili kuwa tu nataka nitoe kama maoni yangu, ni kwa nini sasa Serikali isijenge viwanda kwa ajili ya kuzalisha pembejeo nchini ili pembejeo hizo zipatikane hapa? Nikisema pembejeo nafikiri unaelewa namaanisha mbolea, mbegu na viuatilifu vyote kwa pamoja. Ni kwa nini sasa...

**NAIBU SPIKA:** Umeshauliza maswali yako Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza anauliza ni kwa nini Serikali ya Chama cha Mapinduzi hatutekelezi ilani ya chama chetu? Kwanza nampongeza ndugu yangu Mheshimiwa Silinde kwa kusoma llani kujua mambo mazuri yaliyopo kwa ajili ya wakulima wa Tanzania. Nasi kama Serikali, llani ya Chama cha Mapinduzi ndiyo mwongozo wetu na tunaitekeleza. Ndiyo maana mwaka jana tulileta hapa sheria ya kuweka Mfumo wa Kununua Mbolea kwa Pamoja. Lengo kubwa ni kupunguza bei ya mbolea kwa wakulima wetu. Kwa hiyo, zote hizo ziliikuwa ni katika juhudii za kutekeleza llani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini hatukuufanya ule mfumo wa mwanzo? Ni baada ya kugundua udanganyifu mkubwa sana wakati tunapotoa ruzuku zile za vocha, zile ruzuku ziliikuwa zinaishia mifukoni mwa watu wachache na mpaka sasa hivi Serikali tuko kwenye mchakato wa kwenda

kuwapeleka katika vyombo vyaa sheria wote waliohusika kutafuna hela za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni ushauri. Kwanza tumeupokea, lakini tulishaanza kuufanyia kazi tangu juzi na mpaka sasa Serikali tuko katika majadiliano na wenzetu wa nchi mbili; nchi ya Morocco kwa ajili ya kuzalisha mbolea hapa nchini ya kupandia (*DAP*) kwa sababu nchi ya Morocco ndiyo wazalishaji wakubwa wa mbolea ya kupandia duniani. Pia tuko katika majadiliano ya mwisho na wenzetu wa Uingereza kwa ajili ya kuja kuwekeza katika kiwanda cha mbolea kwa ajili ya mbolea ya kukuzia. Kwa hiyo, yote mawili tumeyachukua na tunayafanya kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Ungando, Mbunge wa Kibiti, Mheshimiwa Julius Kalanga, Mheshimiwa Profesa J.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msiwe na haraka sana, kwa sababu lazima tuangalie watu ambaa hawana maswali. Hawa walioitwa wameleta ujumbe hapa mbele. Kwa hiyo, usione kama umesimama halafu hujaitwa, ameitwa aliyekaa kwa sababu Kanuni zetu zinaruhusu taratibu zote.

Mheshimiwa Mwakajoka, swali la nyongeza. (*Kicheko*)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei elekezi ambayo inatolewa na Serikali imekuwa haina msimamo kwa sababu mabadiliko ya gharama ya usafirishaji wa pembejeo kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani na bei ambazo zinabadilika kwenye Soko la Dunia kwa ajili ya kununua pembejeo. Serikali imejipanga namna gani kuhakikisha kwamba bei elekezi inayokuwa imeshatoa inakuwa na msimamo na wananchi wanaifuata kama ambavyo Serikali imeelekeza? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mwakajoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii lake kuhusu bei elekezi anasema haina msimamo. Bei elekezi ni dira tu yaani ni bei ambayo tunataka isizidi hapo kwa ajili ya kwenda kuwauzia wakulima. Kama alivyo sema, bei hizi zinazingatia hasa gharama za uzalishaji na usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali baada ya kuliona hilo, kwa sababu tumetoa bei elekezi kwa ajili ya mbolea ile mpaka imfikie mkulima, lakini bei za usafiri zinapanda mara kwa mara kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta. Tumewaelekeza Wakuu wa Mikoa wote ambao ndio wasimamizi wakuu mikoani kuangalia hali halisi za umbali wa sehemu zao na vijiji vyao ili mbolea ile ifike isimumumize msafirishaji lakini pia ifike katika bei ambayo wakulima wanaweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la Soko la Dunia, ni kweli, kwa sasa mbolea zimepanda duniani, baada ya Serikali ya China ambao ni wazalishaji wakubwa wa mbolea, kuzuia mbolea yao isitoke nje ya nchi yao. Kwa hiyo, imesababisha *demand* kuwa kubwa kuliko *supply*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, sasa aulize swalii lake.

Na. 90

### **Kusimama kwa Mradi wa Maji Awamu ya Tatu**

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE** aliuliza:-

Ni muda sasa tangu ujenzi wa miundombinu ya Mradi wa Maji Awamu ya Tatu usimame:-

(a) Je, Serikali imeshachukua hatua gani ili kusaidia kuondoa tatizo kubwa la maji katika Halmashauri ya Chalinze?

(b) Je, ni lini sasa mradi huo utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliani, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Chalinze, lenye Sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na uboreshaji wa huduma ya maji katika Halmashauri ya Chalinze ambapo imeshakamilisha mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili. Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa maji Chalinze kwa awamu ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mradi wa Chalinze awamu ya tatu, Serikali imeamua kumrejesha Mkandarasi wa *Overseas Infrastructure Pvt Limited* ya India aliyekuwa amesimamishwa kwa sababu ya kuchelewa kukamilisha mradi ili amalize kazi zilizobaki. Uamuzi umefikiwa ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huo kwa kuwa kuajiri mkandarasi mpya ingechukua muda zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi huyo amepewa masharti mapya yatakayohakikisha kazi inafanyika kwa kasi. Masharti mapya ni pamoja na kuhakikisha analeta fedha nchini za kuwalipa Makandarasi wadogo aliowaajiri (*sub-contractors*) na kuleta wataalam wa kutosha na wenye uzoefu. Kwa mujibu wa makubalino, mkandarasi anatakiwa kukamilisha kazi hiyo Desemba, 2018. Wizara itaendelea kufuatilia ili kuhakikisha mkandarasi huyo anakamilisha kazi

kwa muda uliopangwa na endepo atashindwa hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri yanayotia moyo wana Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, mradi huu umekuwa wa muda mrefu sana na tumekuwa tunauliza sana humu ndani na hata juzi alipokuwepo Makamu wa Rais kule Jimboni yalitolewa majibu kwamba mradi huu utakamilika mwezi Desemba. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, mimi ninaishi na watu wa Chalinze pale chini kabisa, mradi huu siyo kweli kwamba unaweza ukakamilika mwezi Desemba kama ambavyo mmetuahidi. Swali la kwanza, je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba kweli wanachoahidi kinatekelezeka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, yuko tayari kwenda nami baada ya Bunge hili ili kujihakikishia mwenyewe na haya majibu yake anayotoa Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naamini ulifuatilia ziara ya Makamu wa Rais. Sasa ahadi zilizotolewa kule zisije hapa mbele zikatoka tofauti, pamoja na kwamba swali limeulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Chalinze.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Ridhiwani Kikwete kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa dhati ya moyo wangu nampongeza kwa sababu amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana wa mradi huu tangu mwanzo mpaka sasa katika kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. Laiti Bunge lako lingekuwa linatoa tuzo, ningeshauri Mheshimiwa Ridhiwani apewe kwa kuwapigania wananchi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli sisi kama Wizara ya Maji, hatutakuwa tayari kwa wakandarasi ambao watachelewesha miradi ya maji. Nimhakikishie sisi kama Wizara ya Maji tutaendelea kuusimamia mradi huu na mkandarasi akishindwa kufikia malengo tuliyopanga, tutatumia nguvu ya sheria katika kuhakikisha tunamkata *retention* na kuhakikisha kwamba hatua nyingine dhidi yake zinafanyika ili mradi ule ukamilike na wananchi waweze kupata maji na azma ya Mheshimiwa Rais iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwenda na mimi Chalinze, nataka nimhakikishie kwamba mwenda kwao haogopi kiza. Mimi nipo tayari kuambatana naye kwenda Chalinze kuongeza nguvu ili mradi ule uweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 91

#### **Miradi ya Maji Kata za Jimbo la Mufindi Kaskazini**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Katika Tarafa ya Ifwagi kuna wafadhili wa *RDO* wamejitokeza kusaidia katika mradi wa maji Kata za Mdaburo, Ihanu, Ifwagi na Luhunga na wananchi wamekuwa wanachangia katika miradi hiyo:-

Je, ni lini Serikali itaona haja ya kuunga mkono miradi hiyo ya maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

## **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kuna wafadhili kutoka Shirika lisilo la kiserikali (*Rural Development Organization - RDO*) ambalo imesaidia ujenzi wa mradi wa maji kwa kushirikiana na Halmashauri katika Kata za Mdabulo, Ihanu, Ifwagi na Luhunga na wananchi wamekuwa wanachangia katika miradi hiyo. Miradi inayotekelizwa na *Rural Development Organization* katika Kata tajwa hapo juu, Serikali imesaidia kutoa wataalam wake wakisaidia usanifu na usimamizi wa kitaalam wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013 hadi 2018, Shirika la *Rural Development Organization* limejenga miradi ya maji katika vijiji sita vya Ludilo, Kidete, Ikanga, Mkuta, Ibwanzi na Nandala katika Kata za Mdabulo, Ifwagi na Ihanu ambapo jumla ya vituo vya kutochotea maji 182 vimejengwa, Ludilo (33), Kidete (52), Ikanga (28), Mkuta (9), Ibwanzi (36) na Nandala (24). Pia katika mwaka huu wa fedha 2018/2019 wafadhili wa *Rural Development Organization* wanaendelea na ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji vitatu vya Mkonge, Luhunga na Igoda, ambapo kwa sasa mradi umekamilika katika Kijiji cha Mkonge jumla ya vituo 14 vya kuchotea maji vimejengwa na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawashukuru wafadhili kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika Halmashauri ya Mufindi. Kwa kutambua mchango wao katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali ilisogeza umeme katika chanzo cha maji cha Mradi wa Maji wa Vijiji vya Mkonge, Luhunga na Igoda vilivyopo katika Kata ya Luhunga. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha

wananchi waishio vijiji ni wanapata huduma ya maji safi na salama na hivyo kufikia lengo la asilimia 85 ya wananchi ifikapo 2020.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, swali la nyongeza.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na maelezo mazuri ya Serikali, nina maombi mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la kwanza, naiomba Serikali ije Mufindi kwenye Jimbo la Mufindi Kaskazini na Kusini itembelee ijionee miradi hiyo ambayo inasaidiwa na wafadhili, kusudi ipate nafasi ya ku-*cheap in.*(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili, hawa Wafadhili wenzetu wa *RDO, Water of Africa* na Baba Paroko Misosi, wanasaidia kwa kiasi kikubwa miradi ya maji katika Majimbo yetu yote mawili, Jimbo la Mufindi Kusini na Mufindi Kaskazini. Naiomba Serikali itenge wasaa wa kukutana na hawa wafadhili kusudi ionyeshe *appreciation* kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa niaba ya Serikali. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, maombi mawili hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge na pia ni Mwenyekiti wa Kamati yetu pamoja na Wajumbe wake, wamekuwa msaada mkubwa sana kwa Wizara yetu katika kuhakikisha tunatekeleza miradi mbalimbali katika kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu ombi lake, nipo tayari kutembelea Jimbo lake, lakini pia kuwatuma wataalam wetu wa Wizara kwenda kuangalia upungufu katika kuhakikisha tunautatua ili wananchi wake waendelee kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna nyingine ya kipekee, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake binafsi za kutafuta wafadhili kuweza kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Namhakikishia kwamba sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo cha kukutana na wafadhili hao katika kuhakikisha tunaendeleza mahusiano mazuri ili kutatua matatizo ya maji nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini.

Na. 92

**Mradi wa Maji Huhudumia hadi Bukoba Vijijini**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Mradi mkubwa wa maji uliopo Manispaa ya Bukoba una tanki kubwa la maji lililo karibu na Kata ya Karabayaine Bukoba Vijijini lakini mradi huo hauhudumii maeneo ya Bukoba Vijijini yaliyo karibu:-

Je, kwa nini mradi huo usihudumie maeneo ya Kata za Karabayaine, Katoma, Kanyengereko, Mamku na Bujugo yaliyo Bukoba Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imekamilisha mradi mkubwa wa maji safi katika Manispaa ya Bukoba. Mradi huo ulisanifiwa kuhudumia wakazi wa Manispaa ya Bukoba pamoja na wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni katika Manispaa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza upanuzi wa mtandao wa maji safi, kutoka kwenye mradi huo mkubwa kwenda kwenye maeneo ya pembezoni ya Manispaa ya Bukoba kwa awamu. Kwa awamu ya kwanza upanuzi wa mradi huo unahuishisha Kata za Kahororo, Kibeta, Ijuganyondo, Kagondo, Kashai na baadhi ya maeneo ya Nshambya na Nyanga. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya upanuzi wa mradi huo katika maeneo ya pembezoni utahusisha maeneo ya Karabayaine, Maruku na Kanyengereko pamoja na maeneo mengine ya pembezoni. Awamu wa pili inatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Serikali itaendelea kutafuta vyanzo vingine vyta maji kwa ajili ya Vijiini vya Katoma na Bujugo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jasson Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini napenda kusema kwamba maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Naibu Waziri haya ya Kahororo, Kibeta na mengine yapo mjini, Manispaa ambao hawajawahi kuwa na shida ya maji, mimi nazungumzia Bukoba Vijiini ambako kuna shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lengo la Serikali ni kusaidia wananchi ambao wana tatizo la maji kama kwangu Bukoba Vijiini wapate maji kwa gharama nafuu kama inawezekana. Manispaa wana mradi huo mkubwa ambao nimeusema ambao umejengwa na umekamilika na ni mkubwa sana, unatoa maji mara mbili ya mahitaji ya Bukoba Mjini, Manispaa na kwa hiyo, ni hasara kwa Bukoba Mjini kuwa na mradi huo ambao maji yote hayatumiki. Kata hizi ambazo zimetajwa za Bukoba Vijiini ziko karibu na tanki kubwa la maji la kwenda Bukoba Mjini, kwa sababu Bukoba Mjini ni bonde, walijenga tanki juu kusudi maji yaende mjini kwa bubujiko (*gravity*). Sasa Kata za Karabayaine, Katoma, Kanyengereko, Maruku, Bujugo na Nyakato ziko jirani sana

na tanki hilo kwa hiyo, ni rahisi kupeleka maji pale kwa gharama nafuu. Je, Serikali haioni kwamba ni nafuu kufanya mradi huu kwa Bukoba Vijijiini katika maeneo haya ambayo nimeyataja ya Kata hizi za Karabayaine na nyingine ili wananchi wapate maji? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa dhati ya kuwapigania wananchi wa Jimbo la Bukoba Vijijiini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha Watanzania wa Mijini na Vijijiini wanapata maji safi na salama na yenye kuwatoshaleza. Serikali imefanya jitihada kubwa sana ya kuhakikisha inatekeleza mradi mkubwa sana. Sasa safari moja huanzisha hatua nyingine. Tumeshaanza hatua ya kwanza ya kujenga mradi, lakini hatua ya pili ni katika kuhakikisha tunasambaza mradi huo.

Mheshimwia Naibu Spika, namwomba Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bukoba, ahakishe anawapelekea maji wananchi wa Katoma na Bujugo kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezekiel Maige, swali na nyongeza.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali yangu inatekeleza mradi mkubwa wa maji kwa kushirikiana na Mgodi wa Bulyanhulu kutoa maji eneo la Mhangu Shinyanga Vijijiini kuja eneo la llogi karibu kabisa na Mgodi wa Bulyanhulu. Sida yangu ni kwamba mradi huu unatekelezwa kwa ubia baina ya Serikali na Mgodi wa

Bulyanhulu wa Acacia. Utoaji wa fedha mpaka sasa hivi ni ule tu unaotoka Serikalini, lakini Acacia hawajatoa fedha yoyote pamoja na kwamba walipaswa watoe hadi shilingi bilioni 5 kufikia sasa. Nataka kujua, Serikali inachukua hatua gani ili kumbana huyu mbia atoe fedha ili mradi uende kwa kasi kama ambavyo imekusudiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Ezekiel Maige kwa kazi nzuri anayoifanya. Kikubwa, nataka nimhakikishie sisi kama Serikali tumekuwa tukifanya jithada ya kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia washirika mbalimbali. Nataka nimhakikishie mradi ule hautakwama na sisi kama Serikali tunaendelea na mazungumzo na wenzetu kuhakikisha mradi huu unakamilika kama ulivyopangwa.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 93

#### **Upungufu wa Madaktari – Hospitali ya Rufaa Iringa**

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa haina Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto:-

Je, ni lini Serikali itaongeza idadi ya Madaktari walau wafike Madaktari kumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swal Na. 93 niruhusu nitumie Bunge lako Tukufu kuwaarifu Watanzania kuwa leo ni Siku ya Kisukari Duniani na bahati mbaya tunashuhudia ongezeko la wagonjwa wa kisukari katika maeneo ya mijini na vijiji, takribani 9% ya Watanzania wana ugonjwa wa kisukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwahimiza wananchi kupima afya zao ili kujitambua kwamba wana ugonjwa wa kisukari, kwa sababu mara nydingi watu wengi hawajitambui kama wana ugonjwa huu. Pia kujiepusha na mambo ambayo yanaweza kusababisha kupata ugonjwa wa kisukari ikiwemo ulaji wa vyakula usiofaa, kutofanya mazoezi na kunywa pombe kupita kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kujibu swal la Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa ina jumla ya Madaktari Bingwa watano kama ifuatavyo; Daktari Bingwa wa Upasuaji, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Akina Mama na Afya ya Uzazi, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Daktari Bingwa wa Macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wapo Madaktari saba, waajiriwa wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa ambao kwa sasa wapo katika vyuo mbalimbali nchini wakisomea masomo ya Kibingwa. Madaktari hao wanasomea Udaktari Bingwa katika maeneo ya magonjwa ya akina mama na afya ya uzazi (3); Daktari wa Watoto (1); Upasuaji wa jumla (1); Radiolojia (1); na Ngozi (1). Inatarajiwa kuwa ifikapo mwaka 2020 wote watakuwa wamemaliza masomo yao na hivyo kufanya idadi ya Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Mkoa wa Iringa kuwa 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Madaktari saba wa Hospitali hii wakiendelea na masomo yao ya Udaktari Bingwa, Hospitali hii pia hupokea Madaktari Bingwa wa fani mbalimbali kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kufundisha wanafunzi wa Chuo hicho wanaotumia Hospitali hii kujifunza kwa vitendo. Madaktari hawa huja Hospitali kila baada ya wiki mbili na kufanya kazi kwa muda wa wiki mbili. Madaktari Bingwa wanaokuja kwa utaratibu huu ni Madaktari Bingwa wa magonjwa ya watoto, upasuaji wa jumla, magonjwa ya ndani na magonjwa ya akina mama na afya ya uzazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa inayoikibili Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa ni Daktari Bingwa wa Watoto. Watoto wengi katika Mkoa wa Iringa wanapata shida ya matibabu kutokana na kutokuwa kuwa na Daktari Bingwa wa pale hospitali. Namwomba Mheshimiwa Waziri, mpango uliopo ni kweli na hao wa *UDOM* huwa wanakuja, lakini wapo wasiokuwa na uwezo wa kuwapeleka watoto wao Hospitali ya Ikonda, ni lini Serikali itampeleka Daktari Bingwa wa Watoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa pamoja na Daktari Bingwa wa Pua, Masikio na Ugonjwa wa Koo? Nashukuru. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru

sana Mheshimiwa Mama Mwamwindi kwa swali lake zuri hasa katika kufuatilia afya ya mama na mtoto kwa Mkoa wa Iringa na kuwasemea wanawake wa Iringa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza, Daktari mmoja kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, anasomea Uduktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto na tunatarajia atamaliza 2020. Huyu ni mmoja wa Maduktari Bingwa 125 ambaa Wizara ya Afya tunawasomesha. Tumetumia takribani shilingi bilioni 2.4 na tutawasambaza katika hospitali mbalimbali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwajulishe na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba mpango wetu kama Wizara ya Afya baada ya kuzichukua Hospitali za Rufaa za Mikoa, tumebainisha Maduktari Bingwa nane ambaa tunawataka wawepo wawili kila Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Tutakuwa na Duktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto, Duktari Bingwa wa Magonjwa ya Akina Mama na Uzazi, Duktari Bingwa wa Upasuaji wa Jumla, Duktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa na Magonjwa ya Ajali, Duktari Bingwa wa Radiolojia, Duktari Bingwa wa Dawa za Usingizi na Duktari Bingwa wa Magonjwa ya Pua, Koo na Masikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mama Mwamwindi kwamba tumewachukua mwaka jana kwenda masomoni na ndani ya miaka miwili watu hawa watakuwa wamemaliza masomo na tutawapeleka katika hospitali. Tutawapa mikataba ya kufanya kazi katika Hospitali za Serikali kwa muda wa miaka mitatu kabla ya kwenda katika hospitali binafsi. Huo ndioy mkakati ambaa tumeuweka. (*Makofij*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mna maswali wa nyongeza lakini muda wetu umekimbia kidogo. Kwa hiyo, tutaendelea na swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 94

### **Ugonjwa wa Alzheimer**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Kumekuwa na taarifa kadhaa kuhusu ugonjwa wa wazee kupoteza kumbukumbu, kwa kitaalam (Alzheimer):-

- (a) Je, ukubwa wa tatizo hilo ukoje?
- (b) Je, nini mkakati wa Serikali katika kudhibiti ugonjwa huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Iringa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kupoteza kumbukumbu kwa wazee ni pana na linajumuisha magonjwa mengi, ugonjwa wa Alzheimer ukiwa ni miongoni mwa magonjwa hayo. Ugonjwa wa Alzheimer unaaminika kuwa ndio chanzo kikuu cha tatizo la kumbukumbu kwa wazee duniani kote likichangia zaidi ya asilimia 60 ya matatizo yote ya kumbukumbu duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujua ukubwa wa tatizo hili katika nchi yetu, mwaka 2014 kulifanyika utafiti Wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro na ripoti kutolewa katika Jalada la Kitafiti la Kimataifa la Afya ya Akili kwa Wazee la mwaka 2014. Utafiti huu ulionesha kuwa tatizo la kumbukumbu kwa watu wazima wenye umri wa miaka 70 au zaidi linakadiriwa kufikia 6.4% kwa wazee wote nchini Tanzania. Utafiti huo,

ulielezea kuwa katika wazee waliobainika kuwa na shida ya kumbukumbu, 44% ya tatizo hilo lilsababishwa na ugonjwa na Alzheimer.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ugonjwa wa Alzheimer hauna tiba maalum, Wizara imejikita katika kudhibiti matatizo yanayozuulika ambayo huchochea ongezeko la ugonjwa huo. Mkakati huo unahusisha upatikanaji wa huduma za tiba kwa magonjwa chochezi ya Alzheimer kama vile kisukari, *pressure*, kiharusi na magonjwa ya akili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swalii la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Nilikuwa naomba tu kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa ugonjwa huu umekuwa na athari kubwa sana kwa wazee wengi nchini, yakiwemo mauaji ya vikongwe wakidhaniwa ni wachawi na wengine kutengwa na jamii zao. Je, ni kiasi gani cha elimu kinatolewa kwa jamii ili kuepusha athari kubwa sana kwa wazee wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langi la pili, je, matibabu ya ugonjwa huu yanapatikana katika ngazi gani ya hospitali? Kwa sababu hata katika Mkooa wetu wa Iringa wazee wengi wamekuwa wakipata taabu sana katika kufuatilia matibabu ya ugonjwa huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka kukiri kwamba bado kuna uelewa mdogo ndani ya jamii yetu kuhusu ugonjwa huu wa *Alzheimer* ambao unawakumba wazee wenye umri zaidi ya miaka 65 na kuendelea. Nampongeza sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kuwa ni mtetezi na wazee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba moja ya sababu ambazo wazee wanauliwa ni kwa sababu ya kukosa kumbukumbu, mzee anaweza kuwa anataka kwenda sokoni, akajisahau akajikuta ameingia kwenye nyumba ya mtu mwingine lakini kwa sababu tu hana kumbukumbu akatuhumiwa kwamba ni mchawi. Namshukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kulileta suala hili ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, nataka kukiri hatujafanya vizuri kama Wizara lakini nataka kuititia Bunge hili kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge katika muktadha mzima wa kusimamia haki, ustawi na maendeleo ya wazee, tutao kipaumbele katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa huu wa *Alzheimer*, hasa kuihamasisha jamii kutimiza wajibu wao katika kuwatunza na kuwalea wazee, kwa sababu matatizo mengi yanasaababishwa na upweke kati ya wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni Watanzania, tusiige tabia za Kizungu za kuwadharau na kutowathamini wazee wetu. Kwa Tanzania tatizo halijakuwa kubwa sana lakini wenzetu Ulaya ni tatizo kubwa sana kwa sababu wazee wengi wanakuwa wapweke, hivyo wanakosa shughuli na watu mbalimbali wa kuchangamsha ubongo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swal lake la pili, matibabu yanapatikana katika hospitali ya ngazi gani? Niseme kwamba katika eneo hili pia hatujafanya vizuri. Lazima niwe mkweli kwa Waheshimwia Wabunge. Matibabu yanapatikana katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Kanda; *KCMC*, Bugando, Muhimbili na Hospitali ya Mirembe. Kwa hiyo, lengo letu ni kuhakikisha pia tunaweka Madaktari wa

Magonjwa ya Afya ya Akili katika hospitali zote za rufaa za mikoa ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa ili sasa wazee wa Mkoa wa Iringa wenye taitizo la magonjwa haya na magonjwa mengine waweze kupata huduma kwa haraka na kwa urahisi na bila kikwazo chochote. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha.

Na. 95

#### **Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa - Rukwa**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA (K.n.y. MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA)** aliuliza:-

Je, ni lini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa itajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa una Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (Sumbawanga Hospitali) inayotoa huduma za rufaa kwa Halmashauri nne za Mkoa huo hadi sasa. Hata hivyo, Hospitali hiyo inazo changamoto za ufinyu wa nafasi na hivyo kuhitaji ujenzi wa miundombinu mipya ili kukidhi mahitaji ya utaaji wa huduma za afya ngazi ya Hospitali ya Rufaa kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa. Kutohana na changamoto hiyo, Serikali ya Mkoa wa Rukwa

imefanya juhudzi za kutafuta eneo jipya la ekari 100 liliopo Milanzi ndani ya Manispaa ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Hospitali za Mikoa kuhamishiwa Wizara ya Afya, tayai Timu ya Wahandisi wa Wizara imetembelea eneo hilo kwa lengo la kubainisha hatua muhimu za kuchukua ili kuanza ujenzi wa Hospitali mpya ya Mkoa wa Rukwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nashukuru kwa majibu yake mazuri, lakini vilevile nampongeza kwa kazi nzuri anayoifanyia Taifa hili. Pamoja na hayo, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya Hospitali za Mikoa kuhamishiwa Wizara ya Afya, Serikali tayari ilikuwa imeshatoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu mipyä. Kazi hiyo ilishaanza kwa kufanya *mobilization*, kupima udongo, kazi iliyofanya na Chuo Kikuu cha *MUST*. Sasa kinachosubiriwa ni kupata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili ujenzi huo uanze?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini Serikali itatoa fedha ili ujenzi uanze, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 ndiyo tutatenga fedha za ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Rukwa kwa sababu mwaka huu tunajenga Njombe, Simiyu, Katavi, Geita na Songwe. Kwa hiyo, Mkoa wa Rukwa tutajenga 2019/2020 kwa sababu mikoa hii haina kabisa Hospitali za Rufaa za Mikoa. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Wizara wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 96

**Chuo cha Maendeleo ya Wananchi  
(Tango FDC) kuwa VETA**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Serikali ilikuwa na mpango mahsus wa kukarabati na kuongeza majengo katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tango *FDC* katika Jimbo la Mbulu Mjini ili kukifanya kuwa Chuo cha *VETA* Daraja la Pili:-

(a) Je, ni lini mpango huo utatekelezwa ili kuwapatia ujuzi vijana wanaokosa nafasi katika vyuo vingine?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isitizame upya miongozo ya usimamizi na uendeshaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuleta tija zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
aliibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu, Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufunsi Stadi katika kufikia azma ya Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Kwa sasa, Serikali haina mpango wa kuvibadili Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuwa *VETA*.

Badala yake, Serikali imejikita katika kuviboresha vyuo hivyo kwa kuvikarabati na kuongeza vifaa vya kujifunzia na kufundishia ili viweze kutoa mafunzo bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 20 imeshaanza na inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2018. Awamu ya pili inatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2019. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tango, kipo katika Mpango wa awamu ya pili.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara inakamilisha kuhuisha Mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kufuatia maboresha hayo, mtaala wa mafunzo utatumia lugha ya Kiswahili. Tuzo zitakazotolewa zitakuwa zenye ubora na zinazotambullika kitaifa na katika ngazi nyingine za mafunzo kwa wale watakaotaka kuijendeleza zaidi. Mwongozo huo unatarajiwa kuanza kutumika Januari, 2019.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Wizara kuititia Naibu Waziri na Waziri wake, natoa shukrani za dhati kwa Waziri na Naibu wake kwa ziara nzuri waliyofanya katika Jimbo la Mbulu Mjini hususan kwa maendeleo ya taasisi za elimu. Sasa naomba kuuliza maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, changamoto kubwa inayoikabili vyuo hivi vya katika kwa maana ya vyuo vya diploma na cheti ni pamoja na gharama kubwa ya chakula, karo na gharama nyingine kwa wanafunzi. Je, ni kwa nini sasa Serikali isitazame utaratibu mzuri wa wanafunzi hawa kupata gharama nafuu pengine kwa mkopo au kwa namna nyingine ya uendeshaji katika kuhitimisha na kufanikiwa kwenye masomo yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, moja ya changamoto inayotokea ni ukosefu wa magari katika vyuo hivi vya *FDC* na vyuo vingine vya diploma na cheti nchini. Je, ni kwa namna gani Serikali itatazama utaratibu wa kuvipatia vyuo hivi magari kwa ajili ya huduma ya dharura inapotokea kwa wanafunzi na watumishi wengine katika mazingira ya chuo? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Issaay, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Issaay pamoja na Mheshimiwa Flatei kwa kazi nzuri ambayo tumeshuhudia wakiwa wanafanya kwenye sekta ya elimu, kwa kweli wanajitahidi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama kubwa za uendeshaji kwenye vyuo vya *FDC*, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa pamoja na mpango unaoendelea wa kukarabari vyuo hivi, lakini vilevile Serikali au Wizara kwa maana hiyo imejipanga kuangalia namna bora zaidi ya kuviendesha ili wananchi wengi waweze kunufaika na huduma ambazo zinatolewa. Kwa hiyo, tumejaribu kuangalia mahitaji yote ya kuweza kuendesha vyuo hivyo kwa ufanisi. Kwa hiyo, tukishamaliza ukarabati, tutaenda kwenye hayo mengine ili vyuo hivyo viweze kuendeshwa kwa hali ambayo inaweza ikafikiwa na wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu hilo la magari, nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kuhusiana na mazingira jumla ya kufundishia na kujifunzia, Wizara imedhamiria kuondoa changamoto zote zilizopo ikiwa ni pamoja na changamoto ya vitendea kazi na tunafahamu kwenye vyuo hivi magari ni kitendea kazi muhimu. Kwa hiyo,

katika mpango huo tutahakikisha kwamba changamoto hiyo inaondolewa.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 97

### **Posho za wazee wa Mabaraza ya Mahakama**

**MHE. SILAFU J. MAUFI** aliuliza:-

Ukomo wa Bajeti katika Mfuko wa Mahakama tangu mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019 hauko rafiki kwa Mahakama kukamilisha majukumu yake hasa kuwalipa Wazee wa Mabaraza ya Mahakama:-

(a) Je, Serikali inawaangalia vipi Wazee hao kwa malimbikizo ya posho zao?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhusu kuongezeka posho za Wazee wa Mabaraza ya Mahakama?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango wa Wazee wa Mabaraza ya Mahakama katika kutoa haki kwa wananchi. Katika mwaka 2017/2018, Serikali ilifanya uhakiki wa malimbikizo ya posho za Wazee wa Mabaraza yenye jumla ya Sh.115,455,000/= na kubaini kuwa malimbikizo halali yalikuwa ni Sh.59,960,000/= sawa na asilimia 52 ya madai yote ya posho. Kiasi kilichosalia cha

Sh.55,495,000/= kilibainika kuwa siyo halali kutohana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa vielelezo au uthibitisho wa kumalizika kwa mashauri husika na fomu za uthibitisho wa madai. Hivyo, Serikali imechukua hatua kwa kuanza kulipa malimbikizo yaliyohakikiwa na yanategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhairi kwamba viwango vya malipo ya posho wanazolipwa Wazee wa Mabaraza kwa sasa havilingani na hali halisi na muda unaotumika kutoa huduma hiyo. Kwa kuzingatia hilo, Mahakama ya Tanzania, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, imeanza kulipa nauli na posho ya chakula kwa Wazee wa Mabaraza wanaoitwa kushiriki mashauri ya vikao kwa ngazi ya Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha viwango vya posho kwa kadri bajeti ya Mahakama itakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silafu Maufi, swali la nyongeza.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kwa majibu ya Serikali niliyopata hivi sasa. Pamoja na shukrani hiyo, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imetoa sababu zilizopelekea kupatikana kwa shilingi milioni 55 kuwa siyo malipo halali, napenda kuuliza kwamba ni nani mwenye dhamana ya kufuatilia, kuhakikisha kwamba inatoa fomu za madai, taarifa ya kukamilika kwa mashauri ili hawa wazee waweze kupata haki zao? Swali langu ni nani mwenye dhamana ya kufuatilia sababu halisi ambazo zimezungumzwa na Serikali za hizi shilingi milioni 55 ambazo hawa Wazee wa Mabaraza ya Mahakama bado wanadai ili waweze kulipwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba posho wanayopewa Wazee wa

Mabaraza ya Mahakama haikidhi hali halisi na wanafanya kazi kubwa zaidi na hata hizo posho zenyewe hazilingani. Je, sasa Serikali ipo tayari kuweka ndani ya bajeti posho za Wazee wa Mabaraza kwa bajeti ya mwaka 2019/2020 ili suala hili lisitokee tena kwa Wazee wetu wa Mahakama kukosa kulipwa posho zao kwa wakati? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anawapigania Wazee wa Mahakama kwa kutambua mchango wao mkubwa katika utendaji wa haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii la kwanza la nani mwenye dhamana ya kufuatilia, katika malimbikizo ya madeni ambayo Serikali inapaswa kulipa, hatua ya kwanza inayofanyika ni uhakiki wa madeni ili kujiridhisha kama madeni haya ni sahihi na baadaye Serikali iweze kulipa. Katika hatua ya awali, baadhi ya nyaraka zilikosekana na ushahidi wa kumalizia kwa mashauri. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali pamoja na wadai wenyewe kwa maana ya Wazee kushirikiana kwa pamoja kupata nyaraka zile muhimu ili baadaye malipo yaweze kufanyika. Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wazee wa Mahakama pamoja na Serikali, tunakaa kwa pamoja kuangalia uhalali wa nyaraka hizo na baadaye waweze kulipwa stahili zao kwa sababu ni haki yao ya kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swalii la pili, Serikali inatambua umuhimu wa Wazee wa Mahakama na ndiyo

maana Wazee hawa wanatambuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura Na. 11 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002, kwa kuwatambua rasmi kwamba ni sehemu ya utendaji kazi wa Kimahakama. Bajeti ya Serikali itakaporuhusu, kwa jinsi Mfuko wa Mahakama unavyoendelea, tutaona namna nzuri ya kuweza kuboresha maslahi ya Wazee hawa. Kwa kuanzia, tumeanza kutoa posho ya chakula na nauli kwa wale wazee ambao wapo katika Mahakama Kuu ili kuwaongezea motisha katika utendaji wa kazi zao.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Fidia kwa Askari wanaojeruhiwa au  
kufariki wakiwa kazini**

**MHE. MAULID SAID MTULIA** aliuliza:-

Askari wa Jeshi la Polisi wanafanya kazi kubwa ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Kazi hiyo ni ngumu na ya hatari hasa ikizingatiwa kuwa matukio ya mauaji ya Askari wetu wa Jeshi la Polisi yanayoongezeka:-

(a) Je, Serikali hutoa kiasi gani cha fedha kama fidia kwa Askari aliyegeruhiwa au kufariki dunia akiwa anatekeleza majukumu yake ya kila siku?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea posho ya mazingira magumu na hasa baada ya Askari wetu kulengwa shabaha wao binafsi na wahalifu kinyume na ilivyokuwa awali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifautavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli jeshi la polisi lina dhamana ya kulinda maisha na mali za raia, aidha, askari anapopatwa na tukio la kupoteza maisha hulipwa fidia ya shilingi milioni 15 na pale inapotekeaa askari kujeruhwa na kupata ulemavu wa kudumu wakati akitekeleza wajibu wake Serikali hulipa fidia kulingana na madhara aliyo yapata baada ya kuthibitishwa na Kamati ya Maslai kwa Askari Walioumnia Kazini ambayo inajumuisha daktari.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuongeza posho ya mazingira magumu kwa askari polisi. Hata hivyo Serikali inakusudia kuisha posho mbalimbali za askari polisi ili ziweze kulipwa kulingana na mazingira halisi ya sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maulid Said Mtulia swalii la nyongeza.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tunakubaliana kwamba vijana hawa wanafanya kazi kubwa sana, lakini vilevile tunakubaliana kwamba inapotokeza wanajeruhwa au kuuawa Taifa linapoteza nguvu kazi na wananchi na wazazi wao kwa ujumla, lakini kiwango cha shilingi milioni 15 kama fidia ya vijana wetu kuuawa wakiwa kazini hakitoshi.

Je, Serikali inaonaje sasa ikaongeza kiwango hiki kutoka shilingi milioni 15 mpaka walau milioni 50 ili kiendane na wakati tuliokuwa nao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, vijana wetu wa jeshi la polisi wanafanya kazi kubwa sana lakini

wanalalamikia kwamba wanapopandishwa madaraja na vyeo huchukua zaidi ya miaka zaidi hata miwili mpaka minne, mishahara yao aibadilishwi kulinga na nafasi walizopewa. Sambamba na hilo umezuka mtindo hivi sasa, wanapopelekwa kozi wanakatwa pesa zao za *ration allowance* ili kugharamia kozi ilhali Serikali ndiyo yenye wajibu wa kuwasomesha

Je, Serikali inatoa kauli gani ya kukomesha vitendo hivi kuhakikisha askari polisi anapopandishwa cheo mwezi huo huo aanze kupata mshahara wake na akienda kozi asikatwe *allowance* yake yoyote kwa sababu ni kazi ya Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mtulia kwa kazi kubwa ambayo anaifanya tangu alipojiunga na upande huu wa pili unaoonesha dhamira ya dhati katika kutekeleza llani hii ya CCM, na ndiyo maana Mheshimiwa Naibu Spika Tulia, Mheshimiwa Mtulia kwa sasa ametulia na ndio maana anaafuatilia maslahi ya askari wa Jeshi la Polisi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba askari wetu wanfanyakazi kubwa, mazingira hatarishi; na ndiyo maana iwe ni usiku, iwe ni mchana iwe ni giza kuwe mwanga, iwe ni mvua iwe ni jua, askari hawa wanafanyakazi ili kuhakikisha Watanzania wanakuwa na amani na usalama nakufanya shughuli zao za maendeleo na za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanapokuwa wanaumia ama wanakufa wakiwa wanatekeleza wajibu wao, ndiyo maana Serikali tunawalipa shilingi milioni 15 kama fedha za fidia. Wazo la Mheshimiwa Mtulia ni wazo zuri, sisi kama Serikali tunalichukua kwa ajili ya kwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili lina maeneo mawili yanayohusu upandishwaji wa vyeo na marekebisho

ya mishahara kuchelewa, lakini pia amezungumzia *ration allowance*, nitajibu swali moja ili yawe maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa askari polisi wanapokwenda mafunzoni fedha zao za chakula huwafuata kokote kule wanakokwenda. Lengo la fedha hizi ni kwa ajili ya lishe kwa askari wetu. Tunataka jeshi lenye askari wenye afya, askari ambao lishe inatengeneza fiziki ya askari. Kwa hiyo, fedha hizi askari lazima azitumie kama fedha za chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa familia ya askari hawa polisi, kuna wakati wanamezea mate posho hizi za chakula, kuna wakati wanazikodolea macho posho hizi za chakula, niwaombe waziache posho hizi wao waendelee na mishahara ya askari ilhali posho hizi waweze kuzitumia askari wenyewe. Tukiruhusu hilli jambo ni sawa na mkulima ambaye ameuza jembe, jembe liliopoisha akala na mbegu na hivyo hakuweza kupanda. (*Makofii*)

Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mtulia ni dhamira yetu kwamba askari hawa tutendelea kuhuisha posho zao mbalimbali kwa ajili hawa ili ziweze kuwasaidia. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho kwa kipindi chetu cha maswali tutaleta matangazo kwenu kabla hatujaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu.

Tangazo la kwanza linahusu wageni, tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika. Kundi la kwanza ni wageni 20 wa Mheshimiwa Spika ambao ni viongozi wa UVCCM Taifa wakiongozwa na Ndugu Tabia Mwita ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana CCM Taifa, karibuni sana. (*Makofii*)

Pia mionganii wao yupo Ndugu Raymong Mwangwala ni Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa, karibuni sana viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia na wajumbe wote ambao mmeambatana nao. (*Makofii*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na hawa ni Taasisi ya Vyombo vyta Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (*MISA Tanzania*) wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Salome Kitomary, karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt... aah, huyu kapewa U-daktari naona leo sijui kama kapewa leo ama ni..., najua ni injinia huyu, sijui kama ni daktari pia.

Wageni wanne wa Mheshimiwa *Engineer Atashasta* Nditiye ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni familia yake na wapiga kura wake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mke wake Ndugu Rosemary Nditiye, karibuni sana wageni wetu. Mheshimiwa Nditiye kama umeshakuwa Dkt. tafadhali mjishe Mheshimwa Spika ili tusiwe tunapata kigugumizi hapa mbele. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimwa Jumaa Aweso ambaye ni Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaye ni Baba yake mdogo kutoka Pangani Mkoani Tanga na huyu ni Ndugu Omari Ibrahim, karibu sana baba yetu. (*Makofii*)

Wageni wanane Mheshimiwa Angella Kairuki ambaye ni Waziri wa Madini, hawa wanatoka taasisi ya *Doris Mollel Foundation* wakiongozwa na kiongozi wa taasisi hiyo Ndugu Doris Mollel, sijajua wamekaa upande gani, karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 33 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira na Vijana na hawa ni wanafunzi kutoka Shule ya Sheria kwa Vitendo (*Law School*) wakiongozwa na Rais wa Serikali ya Wanafunzi ndugu Denis Mbwana. Karibu sana, tunawatarajia mfanye vizuri huko *Law School* mje sokoni tuone namna ambavyo mmepikwa sawasawa. Hata hivyo

nasikitika sijawafundisha hata kidogo, nawatakia kila la kheri. (*Makof!*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambaye ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, huyu ni mtoto wa rafiki yake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam anaitwa Washington Manyeki. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, mtoto huyu amefaulu vizuri mitihani yake ya darasa la saba na mzazi wake (baba yake) alimuahidi akifafulu atamleta Bungeni kwa sababu mtoto ndicho alichokuwa anataka na leo amefika kwa hivyo ametimiza ndoto yake. Kwa hiyo, nimirikie kila kheri katika masomo yaliyo mbele yake, lakini pia niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge ahadi tunazotoa tujitahidi kutekeleza, wazazi pamoa na sisi Wabunge. (*Kicheko/Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Oscar Mukasa ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dodoma, karibu sana. (*Makof!*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Lucy Owenya ambaye ni mdogo wake kutoka Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro, ndugu Roseline Mushi, karibu sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo na hapa tunao wanafunzi 206 na walimu sita kutoka Shule ya Sekondari ya Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Upendo Saronga, karibuni sana watoto wa Makao Makuu hapa Bungeni. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengine ya kazi, tangazo la kwanza Wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira mnatangaziwa na Mwenyekiti wenu Mheshimwa Suleiman Ahmed Saddiq kuwa leo tarehe 14 Novemba, 2018 kutakuwa na kikao cha Kamati kwa ajili ya kujadili ajenda muhimu. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa *dispensary* ya zamani mara tu baada ya kuahirisha kikao cha Bunge saa saba mchana. Kwa hiyo mnaombwa mhudhurie hicho kikao bila kukosa. (*Makof!*)

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Susan Lyimo ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote kuwa tarehe 14 Novemba, 2018 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote. Semina Hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara ya baada ya kuairisha Kikao cha Bunge saa saba mchana. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanawake wote mnaomba muhudhie semina hiyo muhimu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge ninalo pia tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wabunge Waislam Mheshimiwa Mbaraka Dau na anawatangazi Waheshimiwa Wabunge wote waislam kuwa leo tarehe 14 Novemba, 2018 saa saba mchana baada ya kuahirisha Bunge kutakuwa na kikao. Waheshimiwa Wabunge wote waislam mnaombwa kufika bila kukosa. Ukumbi utakuwa ni Msekwa sasa sijajua ni Msekwa ipi, lakini nadhani wanafahamu wapi watakatuna, kwa hiyo, Mheshimiwa Dau ana waomba muhudhurie bila kukosa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo lingine kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya Mtakatifu Thomas More Bunge Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, anawatakazia kuwa leo tarehe 14 Novemba, 2018 kutakuwa na Ibada ya misa kwa wakristo wakatoliki mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge katika ukumbi wa Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki ibada ya misa hiyo. Pia misa hiyo itakuwa rasmi kwa ajili ya kuwaombea wapendwa wetu Marehemu Samuel John Sitta aliyekuwa Spika mstaafu, lakini pia mwalimu Samson Kasuku Bilago ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kuhudhuria ibada hii pia ili muweze kuwaombea wenzetu walotangulia mbele ya haki.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge; mnatangaziwa Waheshimiwa wabunge wote mnatangaziwa kuwa *Tanzania Education Publishers Limited* bado wanaendelea na maonesho ya kuuza

vitabu *Cudo's President Magufuli* na Heko Rais Magufuli katika maeneo ya Bunge. Maonesho hayo yanafanyika kati ya Jengo la Utawala na Jengo la Habari. Waheshimiwa Wabunge mnaobwa kutembelea maeneo hayo ili kwanza mjipatие nakala za vitabu hivi lakini wanavyo na vitabu vingine, mpare fursa ya kuwatembelea.

Baada ya kusema haya Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

Azimio la Bunge la Bunge la Kuridhia Mkataba wa kuuliza Uendelezaji, Ulizalisha, Ulilimbikizaji wa Silaha za Kibailojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (*The Convention on Prohibition of Development Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and their Destruction*) wa mwaka 1972

Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The Charter on Statistics*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI MA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanchama wa Umoja wa Mataifa ambao una jukumu la kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibailojia na sumu pamoja na uangamizaji wake. Mkataba uliandaliwa, kujadiliwa na kuafikiwa na nchi mbalimbali na baadae kuanza kusainiwa tarehe 10 Aprili, 1972.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilisaini Mkataba Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibailojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake tarehe 16

Agosti, 1972 London, Uingereza. Silaha za kibaolojia na sumu ni mionganoni mwa silaha za maangamizi ya halaiki (*weapons of mass destruction*) ambazo zinajumisha pia silaha za kemikali na *nuclear*. Silaha hizi za maangamizi ya halaiki zinaweza kusabisha vifo vingi vya viumbe hai na pia kuleta uharibifu kwa kiwango kikubwa wa miundo mbinu iliyojengwa na binadamu kama majengo, barababa, madaraja na miundo asili kama ardhi na milima na baioanuai kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, silaha za kibalojia zinapatikana kwa kurutubisha vimelea yaani *bacteria*, *virus* na *fungus* na kutumika kama silaha sinazoweza kubabisha madhara makubwa kwa binadamu, wanyama na mimea ikiwa pamoja na vifo na uharibufu wa uoto wa asili na mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vimelea na sumu zitumikazo kama silaha zinaweza kumikiliwa na nchi, watu binafsi zikiwemo kamapuni na hata Taasisi Zisizo za Kiserikali (*Non-State Actors*) wakiwemo magaidi. Baadhi ya njia zinazotumika kubeba silaha wakati wa kutekeleza hujuma au uhalifu ni pamoja na kutumia mabomu, makombora, mzinga, ndege, magari, matenki ya kunyunyizia na vifungashio kama vile mifuko na bahasha zinazotumika kuhifadhi barua. Aidha, vimelea na sumu vinaweza kusambazwa au kusambaa kwa kupitia hewa, maji, vyakula, wanyama mimea na wadudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Maktaba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake (*The Convention on Prohibition of Development Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and their Destruction*) ni kupinga na kukataza matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na matumizi mabaya ya viambata vyake ili kuiweka dunia katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya vimelea na sumu kama silaha yalianza tangu kale, kwa mfano *fungus* za aina ya *claviceps purpures* zilitumika kama sumu ambayo

iliwekwa katika vizima vya maji vya maadui. Kimsingi mkataba inaboresha itifaki ya awali iliyokuwa inajulikana kama *The Protocol for the Prohibition of the Use in War of Asphyxiating, Poisonous or Other Gases, and of Bacteriological Methods of Warfare* ya mwaka 1925.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipengele muhimu vya mkataba huu ni pamoja na vifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Kwanza inatoa maelezo yanayotaka yanayotaka kila nchi mwanachama isijihushe na uendelezaji uzalishaji, ulimbikizaji au upatikanaji na uhifadhi wa silaha za kibaolojia na sumu. Ibara ya Pili, inatoa maelezo yanayotaka nchi mwanachama kuharibu au kubadili matumizi ya silaha za kibaolojia na sumu kuwa matumizi salama ndani ya miezi tisa baada ya kuridhia mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tatu inakataza nchi mwanachama kujihusisha kusafirisha au kusaidia nchi nyingine au Jumuiya za Kimataifa kutengeneza au kupata viambato sumu silaha, vifaa na nyenzo za kusafirishia silaha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Nne pamoja na mambo mengine inataka nchi mwanachama wa mkataba kulingana na utaratibu wa katiba na nchi yake kuchukua hatua muhimu kuzuia na kukataza uendelezaji uzalishaji ulimbikizaji, umiliki na utunzaji wa viambato sumu vifaa na njia za usafirishaji wa vitu hivyo ndani ya mipaka yake na maeneo inayoyadhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tano inahimiza nchi wanachama wa mkataba kushirikiana kutatua matatizo yanayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Sita pamoja na masuala mengine inaweka utaratibu wa nchi mwanachama kuwasilisha malalamiko katika Baraza la Usalama la Umoja

wa Mataifa endapo itabaini kuwa nchi nyingine mwanachama inakiuka wajibu wake kulingana na vipengele veya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Saba inataka nchi mwanachama kusaidia nchi nyingine itakayoomba kupewa msaada kulingana na Mwongozo wa Umoja wa Mataifa (*United Nations Charter*) na pia endapo Baraza la Usalama litakuwa limeridhika kwamba nchi mwombaji imeathiriwa kutokana na kukiukwa kwa mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Nane inaweka utaratibu wa kutafsiri vipengele veya Mkataba, tafsiri ambayo haitazuia au kuiondoa nchi katika kutekeleza majukumu ya itifaki ya awali iliyokuwa inajulikana kama *The Protocol for the Prohibition of the Use in War of Asphyxiating, Poisonous or Other Gases, and of Bacteriological Methods of Warfare* ya mwaka 1925.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tisa inazitaka nchi wanachama wa mkataba kubadilishana taarifa zinazohusu vifaa, mitambo, sayansi na teknolojia kwa ajili ya matumizi salama ya teknolojia za kibaolojia na sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Kumi inaeleza utaratibu wa nchi mwanachama wa kujitoa pindi inapoona kuna tukio lisilo la kawaida kuhusiana na mkataba kwamba limeathiri maslahi ya nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilisaini Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake tarehe 16 Agosti, 1972 London, Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pamoja na kusaini mkataba huo tarehe 16 Agosti, 1972 hadi sasa haijauridhia. Hadi kufikia Septemba, 2018 jumla ya nchi wanachama 182 zilikuwa zimeridhia mkataba huu na nchi tano zilikuwa hazijauridhia, nchi hizo ni Haiti, Misri, Somalia, Syria na Tanzania. Aidha, mkataba ulianza kutumika rasmi tarehe 26

Machi, 1975 baada ya nchi 22 kutuma hati za kuridhia kwa wahifadhi wa mkataba (*depository*).

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kuridhia Mkataba huu ni pamoja na kuimarika kwa ulinzi na usalama wa nchi kwa kushirikiana na nchi nyininge kwa katika kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji na utumiaji wa silaha za kibaolojia na sumu, kupata ufadhili wa mafunzo na mialiko ya kitaalam kutoka Mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile *United Nations Office for Disarmament Affairs*, kwa kuwa yako tayari kusaidia nchi zinazoendelea ili ziweze kutekekeza matakwa ya mkataba. Matumizi salama ya teknolojia za kibaolojia yatatoa fursa ya kuboresha taasisi zitakazosimamia shughuli mbalimbali ikiwemo, uchunguzi na udhibiti wa usahihi wa bidhaa za kibaolojia na sumu. Kupitia maendeleo ya sayansi na vimelea na bidhaa za kibaololojia Tanzania itapata fursa mbalimbali na kutumia tafiti za wanyama, mimea, udongo na mazingira kujihakikishia usalama kupitia mfumo wa kubadilishana taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania itapata taarifa za magonjwa mbalimbali, vyanzo vyake, usambaaji jinsi ya kujikinga na kudhibiti na kusimamia ubora wa maabara za Tanzania ili kufikia kiwango cha kimataifa katika uchunguzi wa bidhaa za kibaolojia na hivyo kuaminiwa na kuletewa sampuli kwa ajili ya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake yaani *The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on Their Destruction, 1972*kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa;

KWA KUWA nchi wanachama katika mukutano wake uliofanyika tarehe 10 Aprili, 1972 ziliazimia kuwa na Mkataba

wa Kuzuia, Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake;

KWA KUWA mkataba huu ulianza kutumika rasmi tarehe 26 Machi, 1975 na hadi kufikia Septemba, 2018 nchi 182 ambazo ni asilimia 97 katи ya nchi 187 zilizosaini mkataba huu ziliwa zimeuridhia;

KWA KUWA kwa muda mrefu kumekuwepo na madhara makubwa yanayosababishwa na matumizi ya silaha za kibaolojia na sumu yakiwemo mauaji ya makusudi ya raia wengi, magonjwa kwa viumbi hai, uharibifu wa mazingira na athari nyingine kwa jamii na uchumi kwa ujumla;

KWA KUWA nchi, watu binafsi na taasisi mbalimbali zimekuwa zikiendelea kutengeneza kumiliki na kutumia silaha za kibaolojia na sumu na kuendelea kusababisha madhara na kuiweka dunia katika hali tete kiusalama;

KWA KUWA kutohana na hali tete kiusalama nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zilionna kuna umuhimu wa kuungana ili kwa pamoja kuchukua hatua za kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake;

KWA KUWA katika kufikia azma hiyo nchi wanachama ziliana kusaini mkataba wa kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake ambapo Tanzania ilisaini mnamo tarehe 16 Agosti, 1972.

KWA KUWA, Mkataba huu wa Kimataifa ambao umekuwa ukitekelezwa na nchi mbalimbali, unahitaji kuridhiwa na Bunge ili uweze kutekelezwa na nchi yetu kikamilifu;

NA KWA KUWA kwa kushirikiana na nchi nyingine katika kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake nchi yetu itanufaika kama ifuatavyo:-

- (a) Kupata fursa ya kubadilishana taarifa za madhara yanayosababishwa na matumizi ya silaha hizi zikiwemo taarifa za magonjwa mbalimbali;
- (b) Kupata uwezo wa kubaini mapema matukio yanayotokana na matumizi ya silaha za Kibaolojia na Sumu na Viambato vyake;
- (c) Fursa ya kupata mafunzo na mialiko ya kitaalamu kwa ajili ya kujenga uwezo wa kukabiliana na majanga yanayosababishwa na silaha hizo;
- (d) Fursa ya kupata teknolojia mpya kuititia sayansi ya vimelea na bidhaa za kibaolojia na tafiti za wanyama, mimeea na mazingira,
- (e) Kupata uwezo zaidi wa kudhibiti na kusimamia ubora wa maabara za uchunguzi wa bidhaa mbalimbali za kibaolojia; na
- (f) Kuweza kupiga hatua katika kutekeleza Kanuni za Afya za Umoja wa Mataifa za Mwaka 2005 zinazoweka masharti ya kuzitaka nchi wanachama kulinganisha matukio na magonjwa yote yanayoathiri afya ya wananchi wake.

NA KWA KUWA kwa kuridhia mkataba huu nchi yetu itatakiwa kutoa michango ya uanachama ambayo ni kiasi cha dola za Marekani 100 kwa mwaka ambacho ni kiasi kidogo ukilinganishwa na manufaa yatakayopatikana;

KWA HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa hayo yanayotokana na mkataba huu, na pia umuhimu wake kwa usalama wa Taifa, naliomba Bunge hili katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu na kwa mujibu wa lbaraya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 liazimie kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake uitwao *The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on Their Destruction, 1972*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofî)*

**AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA KUZUIA UENDELEZAJI,  
UZALISHAJI, ULIMBIKIZAJI WA SILAHA ZA KIBAILOJIA NA  
SUMU PAMOJA NA UANGAMIZAJI WAKE (THE CONVENTION  
ON PROHIBITION OF DEVELOPMENT, PRODUCTION AND  
STOCKPILING OF BACTERIOLOGICAL (BIOLOGICAL) AND  
TOXIN WEAPONS AND ON THEIR DESTRUCTION), WA MWAKA  
1972 – KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambalo lina jukumu la kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake. Mkataba uliandaliwa, kujadiliwa na kuafikiwa na nchi mbalimbali na baadaye kuanza kusalniwa tarehe 10 Aprili 1972. Tanzania ilisaini Mkataba wa kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake tarehe 16 Agosti, 1972 London-Uingereza. Silaha za Kibaiolojia na Sumu ni miongoni mwa silaha za maangamizi ya halaiki (Weapons of Mass Destruction-WMD) ambazo zinajumuisha pia silaha za kikemikali na kinyuklia. Silaha hizi za maangamizi ya halaiki zinaweza kusababisha vifo vingi vya viumbe hai na pia kuleta uharibifu kwa kiwango kikubwa wa miundombinu iliyojengwa na binadamu kama majengo, barabara na madaraja; na miundo asili kama ardhi na milima; na bayoanuwai kwa ujumla wake. Silaha za kibaiolojia zinapatikana kwa kurutubisha vimelea (bakteria, virusi, fangasi) na kutumika kama silaha zinazoweza kusababisha madhara makubwa kwa binadamu, wanyama na mimea ikiwa ni pamoja na vifo na uharibifu wa uoto wa asili na mimea. Vimelea na sumu zitumikazo kama silaha zinaweza kumilikiwa na nchi, watu binafsi zikiwemo kampuni na hata taasisi zisizo za kiserikali (non-state actors) wakiwemo magaidi (*terrorists*). Baadhi ya njia zinazotumika kubeba silaha wakati wa kutekeleza hujuma au uhalifu ni pamoja na kutumia mabomu, makombora, mizinga, ndege, magari, matenki ya kunyonyizia na vifungashio kama vile mifuko na bahasha zinazotumika kuhifadhia barua. Aidha, vimelea na

sumu zinaweza kusambazwa au kusambaa kwa kuptitia hewa, maji, vyakula, wanyama, mimea na wadudu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Madhumuni ya Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (Convention on the Prohibition of the Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on their Destruction-BTWC ni kupinga na kukataza matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na matumizi mabaya ya viambato vyake ili kuiweka Dunia katika hali ya usalama. Matumizi ya vimelea na sumu kama silaha yalianza tangu kale, kwa mfano fangasi za aina ya "Claviceps purpurea" zilitumika kama sumu ambayo iliwekwa katika visima vya maji vya maadui. kimsingi unaboresha Itifaki ya awali iliyokuwa inajulikana kama *the Protocol for the Prohibition of the Use In War of Asphyxiating, Poisonous or Other Gases, and of Bacteriological Methods of Warfare* ya mwaka 1925.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Vipengele muhimu vya Mkataba ni pamoja na:-

**Moja**, Ibara ya I inatoa maelezo yanayotaka kila nchi mwanachama isijihusishe na uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji au upatikanaji na uhifadhi wa silaha za kibaiolojia na sumu

**Mbili**, Ibara ya II inatoa maelezo yanayotaka nchi mwanachama kuharibu au kubadili matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu kuwa matumizi salama ndani ya miezi tisa baada ya kuridhia mkataba.

**Tatu**, Ibara ya III inakataza nchi mwanachama kujihusisha kusafirisha au kusaidia nchi nyingine au jumuiya za kimataifa kutengeneza au kupata viambato, sumu, silaha, vifaa na nyenzo za kusafirishia silaha hizo.

**Nne**, Ibara ya IV pamoja na mambo mengine inataka nchi mwanachama wa Mkataba kulingana na utaratibu wa Katiba ya nchi yake kuchukua hatua muhimu kuzuia na

kukataza uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji, umiliki na utunzaji wa viambato, sumu, vifaa na njia za usafirishaji wa vitu hivyo ndani ya mipaka yake na maeneo inayoyadhibiti.

**Tano**, Ibara ya V inahimizaNchi wanachama wa Mkataba kushirikiana kutatua matatizo yanayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

**Sita**, Ibara ya VI pamoja na masuala mengine inaweka utaratibu wa nchi mwanachama kuwasilisha malalamiko katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa endapo itabaini kuwa nchi nydingine mwanachama inakiuka wajibu wake kulingana na vipengele nya mkataba.

**Saba**, Ibara ya VII inataka nchi mwanachama kusaidia nchi nydingine itakayoomba kupewa msaada kulingana na Mwongozo wa Umoja wa Mataifa "United Nations Charter" na pia endapo Baraza la Usalama litakuwa limeridhika kwamba nchi mwombaji imeathiriwa kutokana na kukiukwa kwa Mkataba huu.

**Nane**, Ibara ya VIII inaweka utaratibu wakutafasirivipengele nya Mkataba. Tafasiri ambayo haitazuia au kuiondoa nchi katika kutekeleza majukumu ya itifikasi ya awali iliyokuwa inajulikana kama "*the Protocol for the Prohibition of the Use in War of Asphyxiating, Poisonous or Other Gases, and of Bacteriological Methods of Warfare*" ya mwaka 1925.

**Tisa**, Ibara ya X inazitaka nchi wanachama wa Mkataba kubadilishana taarifa zinazohusu vifaa, mitambo, sayansi na teknolojia kwa ajili ya matumizi salama ya teknolojia za kibaiolojia na sumu.

**Kumi**, Ibara ya XIII inaeleza utaratibu wa nchi mwanachama wa kujitoa pindi inapoona kuna tukio lisilo la kawaida kuhusiana na Mkataba kwamba limeathiri maslahi ya nchi husika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**,Tanzania ilisaini Mkataba wa kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na

sumu pamoja na uangamizaji wake tarehe 16 Agosti, 1972 London-Uingereza. Tanzania pamoja na kusaini Mkataba huo tarehe 16 Agosti, 1972 hadi sasa haijauridhia. Hadi kufikia Septemba, 2018 jumla ya nchi wanachama 181 zilikuwa zimeridhia Mkataba huu na nchi 6 zilikuwa hazijauridhia. Nchi hizo ni Haiti, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Misri, Somalia, Syria na Tanzania. Aidha, Mkataba ulianza kutumika rasmi tarehe 26 Machi, 1975 baada ya nchi ishirini na mbili (22) kutuma hati za kuridhia kwa Wahifadhi wa Mkataba *Depositary*.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, matokeo ya kuridhia mkataba huu ni pamoja na kuimarika kwa ulinzi na usalama wa nchi kwa kushirikiana na nchi nyingine katika kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji na utumiaji wa silaha za kibaiolojia na sumu; kupata ufadhili wa mafunzo na mialiko ya kitaalam kutoka mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile "United Nations Office for Disarmament Affairs", kwa kuwa yako tayari kusaidia nchi zinazoendelea ili ziweze kutekeleza matakwa ya Mkataba; matumizi salama ya teknolojia za kibaiolojia yatatoa fursa ya kuboresha taasisi zitakazosimamia shughuli mbalimbali ikiwemo uchunguzi na udhibiti wa usahihi wa bidhaa za kibaiolojia na sumu; kupitia maendeleo ya sayansi ya vimelea na bidhaa za kibaiolojia Tanzania itapata fursa mbalimbali na kutumia tafiti za wanyama, mimea, udongo na mazingira kujihakikishia usalama; kupitia mfumo wa kubadilishana taarifa Tanzania itapata taarifa za magonjwa mbalimbali, vyanzo vyake, usambaaji, jinsi ya kujikinga; na kudhibiti na kusimamia ubora wa maabara za Tanzania ili kufikia kiwango cha kimataifa katika uchunguzi wa bidhaa za kibaiolojia na hivyo, kuaminiwa na kuletewa sampuli kwa ajili ya uchunguzi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, baada ya maeleo haya, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji Wake (Convention on the Prohibition of the Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on their Destruction-BTWC) kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Umoja wa Mataifa;

**KWA KUWA** Nchi Wanachama katika Mkutano wake uliofanyika tarehe 10 Aprili, 1972 zilizimia kuwa na Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibailojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake;

**KWA KUWA** Mkataba huu ulianza kutumika rasmi tarehe 26 Machi, 1975, na hadi kufikia Septemba, 2018 nchi 181 ambazo ni asilimia 97 katи ya nchi 187 zilizosaini mkataba huo ziliwuwa zimeuridhia;

**KWA KUWA** kwa muda mrefu kumekuwapo na madhara makubwa yanayosababishwa na matumizi ya silaha za Kibailojia na Sumu yakiwemo mauaji ya makusudi ya raia wengi, magonjwa kwa viumbe hai, uharibifu wa mazingira na athari nyingine kwa jamii na uchumi kwa ujumla;

**KWA KUWA** nchi, watu binafsi na taasisi mbalimbali zimekuwa zikiendelea kutengeneza, kumiliki na kutumia silaha hizi za Kibailojia na Sumu na kuendelea kusababisha madhara na kuiweka Dunia katika hali tete kiusalama;

**KWA KUWA** kutokana na hali hii tete kiusalama, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ziliona kuna umuhimu wa kuungana ili kwa pamoja kuchukua hatua za kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za Kibailojia na Sumu pamoja na uangamizaji wake;

**KWA KUWA** katika kufikia azma hiyo nchi wanachama zilianza kusaini Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibailojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake, ambapo Tanzania ilisaini mnamo tarehe 16 Agosti, 1972;

**KWA KUWA** Mkataba huu wa kimataifa ambao umekuwa ukitekelezwa na nchi mbalimbali unahitaji kuridhiwa na Bunge ili uweze kutekelezwa na nchi yetu kikamilifu;

**NA KWA KUWA**, kwa kushirikiana na nchi nyingine katika kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibailojia na sumu pamoja na uangamizaji wake, nchi yetu itanufaika kama ifuatavyo:-

- (a) Kupata fursa ya kubadilishana taarifa za madhara yanayosababishwa na matumizi ya silaha hizi zikiwemo taarifa za magonjwa mbalimbali;
- (b) Kupata uwezo wa kubaini mapema matukio yanayotokana na matumizi ya silaha za Kibaiolojia na sumu na viambato (precursors) vyake;
- (c) Fursa ya kupata mafunzo na mialiko ya kitaalam kwa ajili ya kujenga uwezo wa kukabiliana na majanga yanayosababishwa na silaha hizo;
- d) Fursa ya kupata teknolojia mpya kupitia sayansi ya vimelea na bidhaa za Kibaiolojia na tafiti za wanyama, mimea na mazingira;
- (e) Kupata uwezo zaidi wa kuthibiti na kusimamia ubora wa maabara za uchunguzi wa bidhaa mbalimbali za kibaiolojia; na
- (f) Kuweza kupiga hatua katika kutekeleza kanuni za afya za Umoja wa Mataifa za Mwaka 2005 zinazoweka masharti ya kuzitaka Nchi Wanachama kukinga matukio na magonjwa yote yanayoathiri afya ya wananchi wake.

**NA KWA KUWA** kwa kuridhia Mkataba huu nchi yetu itatakiwa kutoa michango ya wanachama ambayo ni kiasi cha Dola za Marekani 100 kwa mwaka ambacho ni kiasi kidogo ikilinganishwa na manufaa yatakayopatikana;

**KWA HIYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu na pia umuhimu wake kwa usalama wa Taifa, Bunge hili katika Mkutano wa 13 na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 linaazimia kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji,

Ulimbikizaji wa Silaha za Kibailojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake uitwao "*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on their Destruction*".

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. (*Makofii*)

Waheshimiwa hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati, ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Hassan Azzan Zungu, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu Pamoja Uangamizaji wake wa mwaka 1972 (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on Their Destruction, 1972*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji na Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake wa Mwaka 1972 [*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on Their Destruction, 1972*].

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyongeza ya Nane ya kifungu cha 7(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inazipa Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, jukumu la kushughulikia miswada ya sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Hivyo, kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kimeelekeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kusimamia Wizara tatu za Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na jukumu la Kikanuni kuhusu kushughulikia mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 12 Novemba, 2018, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi (Mbunge) na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake. Vilevile Kamati ilipewa maelezo kuhusu vipengele vyake muhimu na faida za kuridhia mkataba huo. Baada ya maelezo hayo Kamati ilipata fursa ya kutafakari na kujadili kwa kina hoja hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya machapisho mbalimbali kuhusu mkataba, kwa kuzingatia wajibu wa Kamati katika kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, Kamati ilipitia machapisho mbalimbali kuhusu mkataba huo ili kupata uelewa kuhusu dhana ya uendelezaji, uzalishaji na ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilipitia maandiko kuhusu jitihada zilizofanywa kimataifa katika kuhakikisha udhibiti wa matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu ikiwemo

kusainiwa kwa mkataba wa silaha za kibailolojia. Aidha, Kamati ilijiridhisha kuhusu tarehe ambayo Tanzania ilisaini mkataba huo, idadi ya nchi zilizosaini, idadi na nchi zilizokwishardhia pamoja na idadi na nchi ambazo hazijasaini wala kuridhia. Aidha, Kamati ilijiridhisha kuhusu faida zitakazopatikana kutokana na Tanzania kuridhia mkataba huo na hasara zinazoweza kupatikana kwa kutouridhia mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia machapisho mbalimbali kama ilivyoelezwa hapo juu, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza chimbuko la dhana ya uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, silaha za kibaiolojia zilitambulika rasmi kuwa moja kati ya silaha za maangamizi ya halaiki (*Weapons of Mass Destruction- WMD*) baada ya Marekani kushambulia Miji ya Hiroshima na Nagasaki kwa mabomu ya atomiki yaliyotengenezwa kwa urani (*uranium*) mwezi Agosti, 1947 Silaha hizo za kibaiolojia hutumika kusambaza kwa makusudi magonjwa kwa binadamu, wanyama na mimea kupitia vimelea (virusi, bakteria au fangasi) kwa lengo la kusababisha madhara makubwa na wakati mwingine vifo na uharibifu wa uoto wa asili na mimea kwa adui ambaye hajajipanga kabisa kuvamiwa kwa njia hiyo. Vimelea hivyo husambazwa kwa kupitia hewa, maji, vyakula, wanyama, mimea na wadudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu zinaonesha kuwa silaha za kibailolojia zilianza kutengenezwa na kutumika tangu miaka ya 1346 ambapo matukio mbalimbali yamerekodiwa ikiwa ni pamoja na Uingereza kugawa mablanketi yenye virusi vya tetekuwanga kwa wananchi wa India wakati wa vita kati ya India na Ufaransa mwaka 1767; na Japan kusambaza bakteria wa homa ya tumbo kwenye hifadhi kuu ya maji yanayotumiwa na Jeshi la Shirikisho la Kisovieti mpakani mwa Mongolia mwaka 1939.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa vimelea vitumikavyo kama silaha za kibailojia na sumu vinaweza kumilikiwa si tu na nchi bali na watu au taasisi binafsi wakiwemo magaidi, jambo ambalo linaongeza uwezekano wa kutokea kwa mashambulio ya aina hiyo katika zama hizi ambazo matukio ya ugaidi yanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na madhara makubwa yatokanayo na matumizi ya silaha za kibailojia na sumu, kumekuwa na jitihada mbalimbali za kupinga matumizi ya silaha hizo kuititia itifaki ya mikataba mbalimbali ya Shirikisho la Kimataifa (*League of Nations*) na Umoja wa Mataifa (*United Nations*) kama inavyoelezwa hapa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitahada za kuzuia matumizi ya silaha za kibailojia na sumu zinaonekana kuanzia kwenye mikataba ya *The Hague* ya mwaka 1899 na 1907 maarufu kama *The Hague Conventions/The Hague Peace Conferences of 1899 and 1907*. Mikataba hii ndio iliyoleta ya kwanza kutambua uhalifu wa kivita (*war crimes*) katika sheria za kimataifa. Mikataba hii pia pamoja na mambo mengine iliweka taratibu za uendeshaji wa vita ikiwa ni pamoja na kulinda raia na mali zao wakati wa vita, kwa kuzingatia *liaber code*. Hata hivyo, mikataba hiyo haikuainisha udhibiti wa silaha ikiwemo silaha za kibailojia na sumu wakati wa vita ingawa ilifanikiwa kuweka mifumo ya kitaasisi ya kutatua migogoro ya kimataifa kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mikataba hiyo haikuainisha udhibiti wa matumizi ya silaha za kibailojia, Shirikisho la Kimataifa mnamo tarehe 17 Juni, 1925 lilipitisha Itifaki ya Geneva (*Geneva Protocol*) ya kuzuia matumizi ya silaha za kibailojia na sumu katika vita baina ya mataifa (*The Protocol for the prohibition of the use in War Asphyxiating, Poisonous or other Gases and of Bacteriological methods of Warfare*). Itifaki hii ilianza kutumika tarehe 8 Februari, 1928 kabla ya Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, itifaki hii haikuzuia uendelezaji, uzalishaji na ulimbikizaji wa silaha za kibailojia na sumu.

Mheshimiwa Naibu Hivyo, kutokana na upungufu huo, tarehe 10 Aprili, 1972, Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on Their Destruction*) unaojulikana kama *The Biological Weapons Convention (BWC)*. Mkataba huu unakataza kabisa uendelezaji, uzalishaji na ulimbikizaji wa silaha hizo isipokuwa kwa matumizi salama hususan kinga au dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya rasimu ya mkataba huo kuridhiwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (*UN General Assembly*) mwaka 1972 baadhi ya nchi zilipinga kuwepo kwa mkataba unaojitegemea kuhusu silaha za kibaiolojia, pendekezo lilitolewa na Shirikisho la Kisovieti kwa niaba ya nchi saba za kundi la kijamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo baada ya majadiliano marefu, Marekani na Shirikisho la Kisovieti waliwasilisha mapendekezo tofauti lakini yenye maudhui yanayofanana kuhusu udhibiti wa silaha za kibaiolojia kwenye Mkutano wa *Disarmament Committee* wa Umoja wa Mataifa. Kamati hiyo iliridhia mapendekezo hayo na kuyawasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambao uridhia rasimu ya mkataba huo tarehe 16 Disemba, 1971.

Mheshimiwa Spika, kusainiwa kwa mkataba wa kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake; Kamati ilijiridhisha kuhusu muda/kipindi ambacho Mkataba huu ulisainiwa. Kamati ilibaini kuwa mkataba wa kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on their Destruction*) ulisainiwa tarehe 10 Aprili, 1972 na kuanza kutumika rasmi tarehe 26 Machi, 1975 ambapo hadi kufikia mwezi Septemba 2018, nchi wanachama wa Umoja wa

Mataifa 182 zilikuwa zimeridhia. Aidha, Kamati ilibaini kuwa ni nchi 10 tu za Umoja wa Mataifa ambazo hazikusaini Mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilisaini mkataba huo tarehe 12 Agosti, 1972 Jijini London, Uingereza ikiwa ni miaka 46 iliyopita na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi tano ambazo zilisaini mkataba huo lakini hadi sasa hazijauridhia. Nchi hizo ni pamoja na Haiti, Misri, Somalia na Syria ambazo baadhi yake zimekuwa na matatizo ya kivita ikilinganishwa na Tanzania, jambo ambalo linaweza kuifanya Tanzania kudhaniwa kuwa haina sababu ya msingi ya kutouridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa zipo nchi ambazo hazikusaini Mkataba huo lakini zilijunga baadaye na kuuridhia Mkataba huo (*accession/ratification*) kutokana na umuhimu wake. Nchi hizo ni pamoja na Jamaica mwaka 1975, Kenya mwaka 1976, Libya mwaka 1982, Burkina Faso mwaka 1991, Albania mwaka 1992 na Croatia na Estonia mwaka 1993.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu msingi wa Tanzania kucheleva kuridhia mkataba huo. Kwa sababu hiyo, Serikali ilitoa maelezo kuwa ucheleweshwaji huo unatokana na nia njema ya Serikali ya kujiridhisha kuhusu umuhimu wa kuridhia mkataba.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, awali mkataba huu ulikuwa ukitiliwa mashaka kuwa unawanufaisha mataifa makubwa ambayo mengi yao yameshatengeneza silaha za kibaiolojia. Serikali illithibitishia Kamati kuwa imejiridhisha kwamba manufaa yatakayopatikana kwa kuridhia mkataba huo ni makubwa, jambo ambalo Kamati ililiafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati imebaini kuwa zipo faida ambazo Tanzania itazipata kwa kuridhia mkataba huo. Faida hizo ni pamoja na:-

Moja, kupata fursa ya kuwa mshiriki kamili katika mijadala ya kimataifa inayohusu udhibiti na usimamizi wa matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu;

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, kuwa sehemu ya uhamasishaji wa matumizi sahihi na salama ya silaha za kibaiolojia na sumu. Aidha, nchi yetu itaweza kubadilishana vifaa, teknolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha za kibaiolojia na sumu kwa matumizi salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kunufaika kwa kupata ufadhili wa fedha na kiutaalamu kutoka mashirika ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa na Umoja wa Ulaya, na mataifa yaliyondelea kiteknolojia, mambo ambayo yataiwezesha nchi yetu kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya silaha za kibaiolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kunufaika na tafiti mbalimbali za viumbe (wanyama na mimea) udongo na mazingira zinazofanywa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa walioridhia mkataba huu; na

Tano, kupata uwezo wa kubaini mapema matukio yanayotokana na matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu na viambato vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kupitia mfumo wa kubadilishana taarifa. Tanzania itaweza kutambua vyanzo, usambaaji na jinsi ya kujikinga na magonjwa mbalimbali yanayoweza kusababishwa na matumizi yasiyo sahihi ya silaha za kibaolojia na sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kupata fursa ya kuboresha maabara za uchunguzi wa bidhaa za kibaiolojia na kufikia viwango vya kimataifa, jambo ambalo litaiwezesha kupokea sampuli kwa ajili ya uchunguzi. Mwisho, kupata fursa ya kutoa taarifa kuhusu uvunjifu wa masharti ya mkataba huu dhidi ya nchi wanachama kupitia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kuhusu hasara zinazoweza kupatikana endapo Tanzania haitaridhia mkataba huu. Kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa silaha za kibaiolojia kutumiwa na taasisi au watu binafsi ikiwemo magaidi katika ulimwengu wa sasa, kwa kuridhia mkataba huu, Tanzania itaweza kupata msaada kutoka katika wanachama wa mkataba endapo shambulio lolote la kibaiolojia litaipata nchi yetu. Kamati ilijiridhisha kwamba, Tanzania haiwezi kupata msaada wa aina yoyote endapo hatutaridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni ushauri wa Kamati, baada ya kujadili kwa kina hoja ya Serikali kuhusu Azimio la kuridhia mkataba wa kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na sumu pamoja na uangamizaji wake, Kamati inatoa ushauri ufuataao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Serikali ione umuhimu wa kuwasilisha Bungeni mikataba na itifaki zote zenye manufaa na tija kwa Taifa ambazo zimeshainiwa ili ziweze kuridhiwa kwa ajili ya utekelezaji wake;

Mbili, Serikali itumie vizuri fursa ya kuendeleza kitaaluma na kuboresha taasisi zitakazosimamia shughuli mbalimbali za utafiti, uchunguzi na udhibiti wa bidhaa za kibaiolojia na sumu, kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 10 ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru kipekee Wajumbe wa Kamati kwa michango mizuri wakati wa kuchambua hoja ya Serikali. Michango yao

imewezesha kuikamilisha taarifa hii kwa wakati. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina na naomba nisiyasome kwa sababu ya muda, naomba majina hayo yote yaingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wabunge cha *Parliamentarians for Global Action* kwa kukubali mwaliko na kushiriki Kikao cha Kamati cha kuchambua hoja ya Serikali. Mchango wake umekuwa wenye tija katika kuiwezesha kamati hii kufanya uchambuzi wake kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Mbunge na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa uwasilishaji na ufanuzi wa kina alioutoa wakati Kamati ikichambua mkataba huu. Aidha, nawashukuru wataalamu wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Florence Turuka ambao ufanuzi wao pia umeiwezesha Kamati kuchambua na kujiridhisha kuhusu faida za kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili na naomba Bunge lako tukufu liridhie mkataba huu kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja. (*Makof*)

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA  
NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA  
KURIDHIA MKATABA WA KUZUIA UENDELEZAJI,  
UZALISHAJI, ULIBIKIZAJI WA SILAHA ZA  
KIBAILOJIA NA SUMU PAMOJA NA  
UANGAMIZAJI WAKE WA MWAKA 1972  
– KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

(THE CONVENTION ON PROHIBITION OF DEVELOPMENT,  
PRODUCTION AND STOCKPILING OF BACTERIOLOGICAL  
(BIOLOGICAL) AND TOXIN WEAPONS AND ON THEIR  
DESTRUCTION, 1972)

---

**1.0                  UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulibikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake wa Mwaka 1972 (The Convention on prohibition of development, production and stockpiling of bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on their Destruction, 1972).

**Mheshimiwa Spika**, Nyongeza ya Nane ya Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, inazipa Kamati za Kisikta, ikiwemo Kamati hii, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Hivyo, Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeelekeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kusimamia Wizara tatu (3) za Mambo ya Ndani ya Nchi; Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na jukumu la Kikanuni kuhusu kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 12 Novemba, 2018, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Mb, na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Mkataba wa kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake. Vilevile, Kamati ilipewa maelezo kuhusu Vipengele vyake Muhimu na faida za kuridhia Mkataba huo. Baada ya maelezo hayo, Kamati ilipata fursa ya kutafakari na kujadili kwa kina Hoja hiyo ya Serikali.

## **2.0 MAPITIO YA MACHAPISHO MBALIMBALI KUHUSU MKATABA**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia wajibu wa Kamati katika kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, Kamati ilipitia Machapisho mbalimbali kuhusu Mkataba huo ili kupata uelewa kuhusu dhana ya Uendelezaji, Uzalishaji na Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na sumu pamoja na Uangamizaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipitia maandiko kuhusu jitihada zilizofanywa Kimataifa katika kuhamkisha udhibiti wa matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu ikiwemo kusainiwa kwa Mkataba wa Silaha za Kibailolojia. Aidha, Kamati ilijiridhisha kuhusu tarehe ambayo Tanzania ilisaini mkataba huo, Idadi ya nchi zilizosaini, Idadi na Nchi zilizokwisharidhia pamoja na Idadi na Nchi ambazo hazijasaini wala kuridhia. Aidha, Kamati ilijiridhisha kuhusu faida zitakazopatikana kutokana na Tanzania kuridhia Mkataba huo na hasara zinazoweza kusatikana kwa kutouridhia Mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia Machapisho mbalimbali kama ilivyoolezwa hapo juu, Kamati ilibaini yafuatayo:-

## **2.1 Chimbuko la dhana ya Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake**

**Mheshimiwa Spika**, Silaha za Kibaiolojia zilitambulika rasmi kuwa moja kati ya silaha za maangamizi ya halaiki (Weapons of Mass Destruction- WMD) baada ya Marekani kushambulia Miji ya Hiroshima na Nagasaki kwa mabomu ya atomiki yaliyotengenezwa kwa urani (uranium), mwezi Agosti, 1945<sup>1</sup>. Silaha hizo za Kibaiolojia hutumika kusambaza kwa makusudi magonjwa kwa binadamu, Wanyama na mimea kupitia vimelea (virusi, bakteria, au fangasi) kwa lengo la kusababisha madhara makubwa na wakati mwingine vifo na uharibifu wa uoto wa asili na mimea kwa 'adui' ambaye hajajipanga kabisa kuvamiwa kwa njia hiyo. Vimelea hivyo husambazwa kwa kupitia hewa, maji, vyakula, Wanyama, mimea na wadudu.

**Mheshimiwa Spika**, Kumbukumbu zinaonesha kuwa silaha za kibailojia zilianza kutengenezwa na kutumika tangu miaka ya 1346 ambapo matukio mbalimbali yamerekodiwa ikiwa ni pamoja na Uingereza kugawa mablanketi yenye virusi vya tetekuwanga kwa wananchi wa India wakati wa vita katika ya India na Ufaransa mwaka 1767; na Japan kusambaza bacteria wa homa ya tumbo kwenye hifadhi kuu ya maji yanayotumiwa na Jeshi la Shirikisho la Kisovieti mpakani mwa Mongolia mwaka 1939.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa vimelea vitumikavyo kama silaha za kibailojia na sumu vinaweza kumilikiwa si tu na nchi bali na watu au taasisi binafsi wakiwemo Magaidi, jambo ambalo linaongeza uwezekano wa kutokea kwa mashumbulio ya aina hiyo katika zama hizi ambazo matukio ya ugaidi yanaongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na madhara makubwa yatokanayo na matumizi ya silaha za kibailojia na sumu,

---

<sup>1</sup>Croddy and Wirtz, Weapons of Mass Destruction, An Encyclopaedia of Worldwide policy, Technology and History, 2005

silaha hizo kuititia Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Shirikisho la Kimataifa (League of Nations) na Umoja wa Mataifa (United Nations) kama inavyoelezwa hapa chini.

## **2.2 Jitihada za Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kibailojia na Sumu**

**Mheshimiwa Spika**, Jitihada za kuzuia uzalishaji na matumizi ya silaha za kibailojia na sumu zinaonekana kuanzia kwenye Mikataba ya *The Hague* ya Mwaka 1899 na 1907 maarufu kama *The Hague Conventions/The Hague Peace conferences of 1899, 1907*<sup>2</sup>. Mikataba hii ndio iliyokuwa ya kwanzu kutambua uhalifu wa kivita (war crimes) katika Sheria za Kimataifa. Mikataba hii, pamoja na mambo mengine, iliweka taratibu za uendeshaji wa vita ikiwa ni pamoja na kulinda Raia na mali zao wakati wa vita, kwa kuzingatia *lieber code*<sup>3</sup>. Hata hivyo, Mikataba hiyo haikuainisha udhibiti wa silaha ikiwemo silaha za kibailojia na sumu wakati wa vita ingawa ilifanikiwa kuweka mifumo ya kitaasisi ya kutatua migogoro ya kimataifa kwa amani<sup>4</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa mikataba hiyo haikuainisha udhibiti wa matumizi ya silaha za kibailojia, Shirikisho la Kimataifa, mnamo tarehe 17 June, 1925 lilipitisha Itifaki ya Geneva (Geneva Protocol) ya Kuzuia matumizi ya Silaha za kibailojia na Sumu katika vita baina ya Mataifa (The Protocol for the prohibition of the use in War Asphyxiating, Poisonous or other Gases and of Bacteriological methods of Warfare). Itifaki hii ilianza kutumika tarehe 8 Februari, 1928 kabla ya Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, Itifaki hii haikuua uendelezaji, uzalishaji na ulimbikizaji wa silaha za kibailojia na Sumu<sup>5</sup>. Hivyo, kutohana na upungufu

---

<sup>2</sup>United Nations Institute of Disarmament Research (UNIDIR), The Role and importance of the Hague conferences: A historical Perspective available at [www.unidir.org](http://www.unidir.org)

<sup>3</sup>Lieber code of April 1863, was an instruction signed by US President Abraham Lincoln during American Civil War that dictated how soldiers should conduct themselves in wartime.

<sup>4</sup>United Nations Institute of Disarmament Research (UNIDIR), The Role and importance of the Hague conferences: A historical Perspective, available at [www.unidir.org](http://www.unidir.org)

<sup>5</sup>United Nations Office for Disarmament Affairs, Biological Weapons available at [www.un.org](http://www.un.org)

huo, tarehe 10 Aprili, 1972, Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (The Convention on prohibition of development, production and stockpiling of bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on their Destruction) unaojulikana kama *the Biological Weapons Convention*<sup>6</sup> (BWC). Mkataba huu unakataza kabisa uendelezaji, uzalishaji na ulimbikizaji wa silaha hizo isipokuwa kwa matumizi salama hususan kinga au dawa.<sup>7</sup>

**Mheshimiwa Spika**, Kabla ya Rasimu ya Mkataba huo kuridhiwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN General Assembly) mwaka 1972, baadhi ya nchi zilipinga kuwepo kwa Mkataba unaojitegemea kuhusu Silaha za kibaiolojia pendekezo lilitolewa na Shirikisho la Kisovieti kwa niaba ya nchi saba za kundi la kijamaa<sup>8</sup>. Hata hivyo baada ya mjadala mrefu, Marekani na Shirikisho la Kisovieti waliwasilisha mapendekezo tofauti lakini yenye maudhui yanayofanana kuhusu udhibiti wa silaha za kibaiolojia kwenye Mkutano wa *Disarmament Committee* ya Umoja wa Mataifa. Kamati hiyo iliridhia mapendekezo hayo na kuyawasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambao uridhia rasimu ya Mkataba huo tarehe 16 Disemba, 1971.

### **2.3 Kusainiwa kwa Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuhusu muda/ kipindi ambacho Mkataba huu ulisainiwa. Kamati ilibaini kuwa Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (The Convention on prohibition of development, production and stockpiling of bacteriological (Biological) and Toxins

---

<sup>6</sup>United Nations Office for Disarmament Affairs, Biological Weapons available at [www.un.org](http://www.un.org)

<sup>7</sup>Reaching critical Will, Biological Weapons, available at [www.reachingcriticalwill.org](http://www.reachingcriticalwill.org)

<sup>8</sup>United Nations: The Biological Weapons Convention: An introduction, 2017

Weapons and on their Destruction) ulisainiwa tarehe 10 Aprili, 1972 na kuanza kutumika rasmi tarehe 26 Machi, 1975 ambapo hadi kufikia Mwezi Septemba 2018, nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa 182 zilikuwa zimeridhia. Aidha Kamati ilibaini kuwa ni nchi 10 tu za Umoja wa Mataifa ambazo hazijasaini Mkataba huo<sup>9</sup>

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ilisaini Mkataba huo tarehe 12 Agosti, 1972 Jijini London, Uingereza ikiwa ni **miaka 46 iliyopita** na kuifanya Tanzania kuwa mionganini mwa nchi tano (5) ambazo zilisaini Mkataba huo lakini hadi sasa hazija uridhia. Nchi hizo ni pamoja na Haiti, Misri, Somalia na Syria ambazo baadhi yake zimekuwa na matatizo ya kivita ikilinganishwa na Tanzania, jambo ambalo linaweza kuifanya Tanzania kudhaniwa kuwa haina sababu ya msingi ya kutouridhia Mkataba huo.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa zipo nchi ambazo hazikusaini Mkataba huo lakini zilijunga baadae na kuuridhia Mkataba huo (Accession/Ratification) kuto kana na umuhimu wake. Nchi hizo ni pamoja na Jamaica- 1975, Kenya 1976, Libya- 1982, Burkina Faso na Swaziland 1991, Albania na Uganda 1992, na Croatia na Estonia 1993<sup>10</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu msingi wa Tanzania kucheleva kuridhia Mkataba huo. Kwa sababu hio, Serikali ilitoa maelezo kuwa, ucheleweshwaji huo unatokana na nia njema ya Serikali ya kujiridhisha kuhusu umuhimu wa kuridhia Mkataba. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, awali Mkataba huu ulikuwa ukitiliwa mashaka kuwa unawanufaisha Mataifa Makubwa ambayo mengi yao yameshatengeneza silaha za kibaiolojia. Serikali iliithibitishia Kamati kuwa imejiridhisha kwamba manufaa yatakayopatika kwa kuridhia Mkataba huo ni makubwa, jambo ambalo Kamati illiafiki.

<sup>9</sup>Chad, Comoros, Djibouti, Eritrea, Israel, Kiribati, Micronesia, Namibia, South Sudan, Tuvalu

<sup>10</sup>Arms Control Association, Biological Weapons Convention Signatories and State Parties, 2018 Available at [www.armstrong.org](http://www.armstrong.org)

## 2.4 Faida za kuridhia Mkataba

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati imebaini kuwa zipo faida ambazo Tanzania itazipata kwa kuridhia Mkataba huu. Faida hizo ni pamoja na:-

- i) Kupata fursa ya kuwa Mshiriki kamili katika mijadala ya kimataifa inayohusu udhibiti na usimamizi wa matumizi ya Silaha za kibaiolojia na sumu;
- ii) Kuwa sehemu ya uhamasishaji wa matumizi sahihi na salama ya silaha za kibaiolojia na sumu. Aidha, nchi yetu itaweza kubadilishana Vifaa, teknolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha za kibaolojia na sumu kwa matumizi salama;
- iii) Kunufaika kwa kupata ufadhili wa fedha na kiutaalamu kutoka Mashirika ya Kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa na Umoja wa Ulaya, na Mataifa yaliyondelea kiteknolojia, mambo ambayo yataiwezesha nchi yetu kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya silaha za kibaiolojia;
- iv) Kunufaika na tafiti mbalimbali za viumbe (Wanyama na mimea) udongo na mazingira zinazofanywa na nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa walioridhia Mkataba huu;
- v) Kupata uwezo wa kubaini mapema matukio yanayotokana na matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu na viambato vyake;
- vi) Kupitia Mfumo wa kubadilishana Taarifa, Tanzania itaweza kutambua vyanzo, usambaaji na jinsi ya kujikinga na magonjwa mbalimbali yanayoweza kusababishwa na matumizi yasiyo sahihi ya silaha za kibaojia na sumu.
- vii) Kupata fursa ya kuboresha maabara za uchunguzi wa bidhaa za kibaiolojia na kufikia viwango vya Kimataifa jambo ambalo litaiwezesha kupokea sampuli kwa ajili ya uchunguzi; na

viii) Kupata fursa ya kutoa taarifa kuhusu uvunjifu wa masharti ya Mkataba huu dhidi ya Nchi wanachama kupitia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

## **2.5 Hasara za kutoridhia Mkataba huu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuhusu hasara zinazoweza kupatikana endapo Tanzania haitaridhia Mkataba huu. Kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa silaha za kibaiolojia kutumiwa na Taasisi au watu binafsi ikiwemo magaidi katika ulimwengu wa sasa, kwa kuridhia Mkataba huu, Tanzania itaweza kupata msaada kutoka katika Mataifa wanachama wa Mkataba endapo shambulio lolote la kibaiolojia litaipata nchi yetu. Kamati ilijiridhisha kuwa, Tanzania haiwezi kupata msaada wa aina hiyo endapo hatutaridhia Mkataba huu.

## **3.0 USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kujadili kwa kina hoja ya Serikali kuhusu Azimio la kuridhia Mkataba wa kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- i) Serikali ione umuhimu wa kuwasilisha Bungeni Mikataba na Itifaki zote zenye manufaa na tija kwa Taifa ambazo zimeshainiwa ili ziweze kuridhiwa kwa ajili ya utekelezaji wake; na
- ii) Serikali itumie vizuri fursa ya kuendeleza kitaaluma na kuboresha Taasisi zitakazosimamia shughuli mbalimbali za utafiti na uchunguzi na udhibiti wa bidhaa za kibaiolojia na sumu, kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 10 ya Mkataba.

## **4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii.

**Aidha**, napenda kuwashukuru kipekee Wajumbe wa Kamati kwa michango mizuri wakati wa kuchambua Hoja ya Serikali. Michango yao imeweza kuijamilisha Taarifa hii kwa wakati. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

- 1) Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb- **MWENYEKITI**
- 2) Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb- **M/ MWENYEKITI**
- 3) Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
- 4) Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
- 5) Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
- 6) Mhe. Mhe. Victor Mwambalaswa, Mb
- 7) Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
- 8) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
- 9) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
- 10) Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
- 11) Mhe. Cosato David Chumi, Mb
- 12) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
- 13) Mhe. Shally Joseph Raymond, Mb
- 14) Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
- 15) Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
- 16) Mhe. Bonna Mosses Kaluwa, Mb
- 17) Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
- 18) Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
- 19) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
- 20) Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb
- 21) Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
- 22) Mhe. Janeth Maurice Massaburi, Mb
- 23) Mhe. Augostino Manyanda Masele, Mb
- 24) Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
- 25) Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mb

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mhe. Jason Rweikiza, Mb na Mwenyezekiti wa Taifa wa Chama cha Wabunge cha *Parliamentarians for Global Action*, kwa kukubali mwaliko na kushiriki Kikao cha Kamati cha Kuchambua Hoja ya Serikali. Mchango wake umekuwa wenye tija katika kuiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wake kwa ufasaha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Mb, Waziri wa Ulinzi na JKT kwa uwasilishaji na ufanuzi wa kina aliontao wakati Kamati ikichambua Mkataba huu. Aidha, nawashukuru wataalamu wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Florence Turuka ambao ufanuzi wao umeiwezesha Kamati kuchambua na kujiridhisha kuhusu faida za kuridhia Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono Azimio hili na naomba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba huu kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Salum Mwinyi Rehani, Mb  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO**  
**YA NJE, ULINZI NA USALAMA**  
14 Novemba, 2018

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K. n. y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGGA TAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za

Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji Wake (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (biological) and Toxin Weapons and Their Destruction*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zimesaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa. Mikataba hii ni pamoja na ile inayolinda haki za binadamu, utawala bora, masuala ya kidemokrasia, mazingira na kadhalika. Pamoja na hayo Tanzania imekuwa ikiunga mkono juhudhi mbalimbali zinazofanywa duniani kuhakikisha kuwa kila raia anaishi kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa karibuni jitihada hizi zimeanza kuingia dosari kubwa. Ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa mikataba kama hili inayolenga usalama wa raia, haki za kuishi na masuala yote ya amani itaheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio hili limekuja wakati muafaka ambapo baadhi ya nchi duniani zinakabiliwa na matatizo mengi ya kiusalama yanayotokana na kusambaa kwa magonjwa yanayotengenezwa kimkakati na vifo kwa kutumia bakteria, virusi hatarishi kwa binadamu, wanyama, mimea, mazingira pamoja na sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna aina nyingi za bakteria, sumu au virusi ambavyo vinaweza kutegenezwa kwa kutumia vifaa vya kimaabara ambavyo kimsingi vinaweza kuleta madhara makubwa kwenye jamii. Silaha hizi za kibaiolojia zinaweza kusababisha vifo vya mamilioni ya watu ndani ya muda mfupi sana kutokana na uwezo wake wa kuharibu mishipa ya damu, moyo, neva za fahamu, kushambulia mifumo ya upumuaji na kadhalika.

Vilevile silaha zile zenye vimelea vya sumu huweza kuwekwa ardhi kwa muda wa miaka mingi na hivyo kuhatarisha maisha viumbi hai wa eneo hilo kila wanapozaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, silaha hizi za sumu za kibaiolojia husafirishwa kwa njia rahisi japokuwa ni silaha zinazohitaji uangalifu mkubwa kwani madhara yake ni makubwa sana. Kutokana na utengenezaji wa silaha hizi za kibaiolojia ni vyema ikafahamika kwamba kiasi kidogo cha sumu hizi kinaweza kusababisha pia magonjwa ya mlipuko na ya kuambukiza endapo uhifadhi wake haukuwa mzuri. Ipo mijadala mikubwa inayoendelea duniani kuhusu baadhi ya magonjwa yanayoua sana kama Ebola na UKIMWI ikilenga kutafuta ukweli iwapo magonjwa haya yametengenezwa na aina fulani za bakteria au virusi ambavyo ni moja ya silaha za kibaiolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa vimelea vya sumu hizi za kibaiolojia zinaweza kuwekwa katika vyanzo vya maji, wanyama waliobeba vimelea wa bakteria au virusi, mizoga ya wanyama, hewa, mimea na kadhalika. Kwa mfano, mwaka 1940 nchi ya Japan ilipeleka mchele wa msaada na ngano zilizochanganywa na vimelea vya ugonjwa wa tauni nchini China ambapo maelfu ya wananchi walidhurika. Vilevile tafiti ya kutengeneza silaha hizi za kibaiolojia nchini Japan mwaka 1937 wafungwa zaidi ya 10,000 walifariki kwa kuwekewa vimelea hatari vyenye sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tutakumbuka sakata la ugonjwa wa kimeta duniani ambapo vimelea vya bakteria waletao madhara kwenye mapafu hususani kwa mifugo vilisambazwa kwa njia ya unga au poda kwa kutumia njia za usambazaji wa barua na hivyo maelfu ya binadamu waliathirika na vimelea vya ugonjwa huu. Mwaka 2001 Shirika la Upelezi la Marekani lilibaini aina hiyo ya bakteria katika mji wa New Jersey. Hii ni baadhi tu ya mifano ya matukio hatari ambayo yanaweza kusababishwa na silaha za kibailojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana kwamba kuendelea kukua kwa teknolojia, mwingiliano wa watu duniani ambayo huhatarisha pia usalama wa mipaka ya nchi, kuibuka kwa vikundi mbalimbali vya uhalifu na ugaidi, chokochoko baina ya nchi na nchi, vinaweza kuwa kati ya

vichocheo muhimu vya utengenezaji wa silaha hizi za kibaolojia au silaha za sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa na taarifa mbalimbali ambazo zinatoa tuhuma kwa mataifa makubwa duniani kuwa sehemu ya utengenezaji wa silaha hizi za kibaolojia hususani zile zenye teknolojia kubwa za kimaabara na za utengenezaji wa madawa. Taarifa hizi zinatoa angalizo kwa mataifa mengine kuchukua hatua za kukabiliana na jambo hili ambalo tayari linaleta tishio kubwa kwa usalama wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zetu hizi changa kiuchumi na kiteknolojia si rahisi sana silaha hizi kutengenezwa japo ni rahisi sana kwa silaha hizi kuingizwa na kutumiwa vibaya kwa kutumiwa na watu au vikundi mbalimbali vinavyohatarisha usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania ilisaini mkataba huu tangu tarehe 10 Aprili, 1972 lakini haukuridhiwa. Kwa hiyo kuridhiwa kwa mkataba huu ni fursa kwa nchi yetu kujadili, kupata wataalamu mbalimbali duniani ambao wanajua kwa undani masuala haya ya silaha za kibaolojia na hata kupata wataalamu wa kuja kufundisha wataalamu wetu kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo kuridhiwa kwa mkataba huu kunatoa tahadhari na fursa zaidi kwa Serikali kuhakikisha inaandaa na kuboresha mifumo yake ya kiulinzi, na endapo kunaripotiwa silaha za aina hii au kumetokea madhara yanayosababishwa na aina yoyote ya silaha za kibaolojia basi mifumo hiyo iwe imara kukabiliana na janga lolote la aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 1(2) ya Azimio hili inazitaka nchi wanachama kujuzuia kwa namna yoyote ile kujihusisha na uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji au kujipatia au kuhifadhi silaha, vifaa au namna ambayo inaweza kutumika katika matumizi yoyote ya hatari au katika matumizi ya silaha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio hili linakataza matumizi yoyote ya silaha za kibailojia pasipo kuainisha matumizi yapi yanaruhusiwa na yapi hayaruhusiwi au si sahihi. Tofauti na taarifa iliyowasilishwa kwenye kamati kuhusu azimio hili katika ukurasa wake wa tano sehemu ya 4(2) ambacho kinælezea faida ya kuridhia mkataba huu. Sehemu hii inasema kama ifuatavyo; "Kuwa sehemu ya uhamashajaji wa matumizi sahihi na salama ya silaha za kibailojia na sumu. Aidha nchi yetu itaweza kubadilishana vifaa, teknolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha za kibailojia na sumu kwa minajili ya kiusalama."

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linabidi liangaliwe kwa umakini ili kuondoa mashaka au jambo lolote linaloweza kuja kuigharimu nchi yetu huko baadae endapo itagundulika kwa namna yoyote inazalisha, inaendeleza, inalimbikiza au kujipatia silaha za namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo iwapo nchi yoyote ina silaha za namna hiyo inapaswa kuziangamiza au kuzibadilishia matumizi mapema iwezekanavyo ndani ya muda wa miezi tisa baada ya kuanza kutumika kwa mkataba huu na si vinginevyo. Hivyo basi, Serikali iweke wazi adhma yake ya kutaka fursa ya kubadilishana vifaa, teknolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha hizi za kibailojia kama ilivyoelezwa katika ripoti iliyotolewa kwa Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, pamoja na nchi yetu kuridhia mikataba mbalimbali bado imekuwa nyuma katika kutunga sheria ambazo zinasimamia mikataba hii. Mara nyingi nchi yetu huishia katika hatua ya pili ya utekelezaji wa mikataba hii ambapo hatua ya kwanza ni kuweka saini kuridhia na ya tatu ni utekelezaji wa sheria kwa kutunga sheria za ndani. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inategemea kuona Serikali ikitunga sheria itakayolinda utekelezaji wa mkataba huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.  
(*Makof*)

HOTUBA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU  
AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA KUZUIA  
UENDELEZAJI, UZALISHAJI, ULIMBIKIZAJI WA SILAHA ZA  
KIBAILOJIA NA SUMU PAMOJA NA UANGAMIZAJI WAKE;  
(The Convention on Prohibition of Development,  
Production and Stockpiling of Bacteriological (biological)  
and Toxin Weapons and their Destruction BTWC) – **KAMA**  
**ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) na Nyongeza ya Nane,  
Kanuni ya 7(1) (b) ya Kanuni za Bunge la Toleo la Januari,  
2016)

---

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imekuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zimesaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa. Mikataba hii ni pamoja na ile inayolinda haki za binadamu, utawala bora, masuala ya kidemokrasia, mazingira n.k. Pamoja na hayo Tanzania imekuwa ikiunga mkono juhudhi mbalimbali zinazofanywa duniani kuhakikisha kuwa kila raia anaishi kwa amani na usalama.

**Mheshimiwa Spika**, hapa karibuni jitihada hizi zimeanza kuingia dosari kubwa. Ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa mikataba kama hii inayolenga usalama wa raia, haki za kuishi na masuala yote ya amani itaheshimiwa.

## 2. MAUDHUI YA AZIMIO LA MKATABA HUU

**Mheshimiwa Spika**, azimio hili limekuja wakati muafaka ambapo baadhi ya nchi duniani zinakabiliwa na matatizo mengi ya kiusalama yanayotokana na kusambaa kwa magonjwa yanayotengenezwa kimkakati na vifo kwa kutumia bakteria, virusi hararishi kwa binadamu, wanyama, mimea na mazingira pamoja na sumu.

**Mheshimiwa Spika**, kuna aina nyingi za bakteria, sumu au virusi ambavyo vinaweza kutegenezwa kwa kutumia vifaa

vya kimaabara ambavyo kimsingi vinaweza kuleta madhara makubwa kwenye jamii. Silaha hizi za kibailojia zinaweza kusababisha vifo vya mamilioni ya watu ndani ya muda mfupi sana kutokana na uwezo wake wa kuharibu mishipa ya damu, moyo, neva za fahamu, kushambulia mifumo ya upumuaji n.k. Vilevile, silaha zile zenye vimelea vya sumu na huweza kuwekwa ardhi kwa muda wa miaka mingi na hivyo kuhtarisha maisha viumbehai wa eneo hilo kila wanapozaliwa.

**Mheshimiwa Spika**, silaha hizi za sumu za kibailojia husafirishwa kwa njia rahisi japokuwa ni silaha zinazohitaji uangalifu mkubwa kwani madhara yake ni makubwa sana, baadhi yake ni mfano wa anthrax au kimeta na kuharibika kwa urahisi (quick decay). Kutokana na utengenezaji wa silaha hizi za kibailojia ni vyema ikafahamika kuwa kiasi kidogo cha sumu hizi kinaweza kusababisha pia magonjwa ya mlipuko na ya kuambukiza endapo uhifadhi wake haukuwa mzuri. Ipo mijadala mikubwa inayoendelea duniani kuhusu baadhi ya magonjwa yanayoua sana kama ebola, ukimwi ikilenga kutafuta ukweli iwapo magonjwa haya yametengenezwa na aina fulani za bakteria au virusi ambavyo ni moja ya silaha za kibailojia.

**Mheshimiwa Spika**, usambazaji wa vimelea vya sumu hizi za kibailojia zinaweza kuwekwa katika vyanzo vya maji, wanyama waliopeba vimelea wa bakteria au virusi, mizoga ya wanyama, hewa, mimea, n.k Mfano, Mwaka 1940, nchi ya Japan ilipeleka mchele wa msaada na ngano zilizochanganyika na vimelea vya ugonjwa wa tauni nchini China na Manchuria ambapo maelfu ya wananchi walidhurika. Vilevile, katika tafiti ya kutengeneza silaha hizi za Kibailojia nchini Japan mwaka 1937 wafungwa zaidi ya 10,000 walifariki kwa kujaribiwa kuwekewa vimelea hatari vyenye sumu.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo tutakumbuka sakata la ugonjwa wa kimeta (anthrax) duniani ambapo vimelea vya bakteria waletao mathara kwenye mapafu hususani kwa mifugo vilisambazwa kwa njia ya unga/poda kwa kutumia

nja za usambazaji wa barua na hivyo maelfu ya binadamu waliathirika na vimelea vya ugonjwa huu. Mwaka 2001, Shirika la Upelezi la Marekani (FBI) lilibaini aina hiyo ya bakteria katika mji wa New Jersey. Hii ni baadhi tu ya mifano ya matukio hatari ambayo yanaweza kusababishwa na silaha za kibailojia.

**Mheshimiwa Spika**, hii ina maana kwamba kuendelea kukua kwa teknolojia, muingiliano wa watu duniani ambayo huhatarisha pia usalama wa mipaka ya nchi, kuibuka kwa vikundi mbalimbali vya uhalifu na ugaidi, chokochoko baina ya nchi nanchi, vinaweza kuwa kati ya vichocheo muhimu vya utengenezaji wa silaha hizi za kibaolojia au silaha za sumu.

**Mheshimiwa Spika**, pamekuwa na taarifa mbalimbali ambazo zinatoa tuhuma kwa mataifa makubwa duniani kuwa shehemu ya utengenezaji wa silaha hizi za kibailojia hususani zile zenye teknolojia kubwa za kimaabara na za utengenezaji wa madawa.Taarifa hizi zinatoa angalizo kwa mataifa mengine kuchukua hatua za kukabiliana na jambo hili ambalo tayari linaleta tishio kubwa kwa usalama wa dunia.

**Mheshimiwa Spika**, katika nchi zetu hizi changa kiuchumi na teknolojia si rahisi sana silaha hizi kutengenezwa japo ni rahisi sana kwa silaha hizi kuingizwa na kutumiwa vibaya kwa kutumia watu au vikundi mbalimbali vinavyohatarisha usalama.

**Mheshimiwa Spika**, serikali ya Tanzania ilisaini mkataba huu tangu tarehe 10 April, 1972 lakini haukuridhiwa. Kwa hiyo kuridhiwa kwa mkataba huu ni fursa kwa nchi yetu kujadili, kupata wataalamu mbalimbali duniani ambao wanajua kwa undani masuala haya ya silaha za kibaolojia, na hata kupata wataalamu wa kuja kufundisha wataalamu wetu kuhusiana na jambo hili.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hilo kuridhiwa kwa mkataba huu kunatoa tahadhari na fursa zaidi kwa serikali kuhakikisha inaandaa na kuboresha mifumo yake ya kiulinzi na endapo kunaripotiwa silaha za aina hii au kumetokea madhara yanayosababishwa na aina yoyote ya silaha za kibailojia basi mifumo hiyo iwe imara kukabiliana na janga lolote la aina hiyo (*detention systems*).

**Mheshimiwa Spika**, katika lbara ya 1(2) ya azimio hili inazitaka nchi wanachama kujizua kwa ***namna yoyote ile kujihuisha*** na uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji au kujipatia au kuhifadhi silaha, vifaa au namna ambayo inaweza kutumika katika matumizi yoyote ya hatari au katika matumizi ya silaha.

**Mheshimiwa Spika**, azimio hili linakataza ***matumizi yoyote ya silaha*** za kibailolojia pasipo kuanlisha matumizi yapi yanaruhusiwa na yapi hayaruhusiwi au sio sahihi, tofauti na taarifa iliyowasilishwa kwenye kamati kuhusu azimio hili katika ukurasa wa 5 sehemu ya 4 kifungu kidogo cha pili ambacho kinaelezea faida ya kuridhia mkataba huu. Sehemu hii inasema ***“kuwa sehemu ya uhamasisaji wa matumizi sahihi na salama ya silaha za kibailolojia na sumu. Aidha nchi yetu itaweza kubadilishana vifaa, teknolojia, malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha za kibailolojia na sumu kwa minajili ya kiusalama”***. Hili linabidi liangaliwe kwa umakini ili kuondoa mashaka au jambo lolote linaloweza kuja kuigharimu nchi yetu huko baadae endapo itagundulika kwa namna yoyote inazalisha, inaendeleza, inalimbikiza au kujipatia silaha za namna hii.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo iwapo nchi yoyote ina silaha za namna hiyo inapaswa kuziangamiza au kuzbadilishia matumizi mapema iwezekanavyo ndani ya muda wa miezi tisa baada ya kuanza kutumika kwa mkataba huu na si vinginevyo. Hivyo basi, serikali iweke wazi adhma yake ya kutaka fursa ya kubadilishana vifaa, teknolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha hizi za kibailolojia kama ilivyoelezwa katika ripoti iliyotolewa kwa wajumbe wa kamati.

### 3. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nchi yetu kuridhia mikataba mbalimbali bado imekuwa nyuma katika kutunga sheria ambazo zinasimamia mikataba hii. Mara nyingi nchi yetu huishia katika hatua ya pili ya utekelezaji wa mikataba hii ambapo hatua ya kwanza ni kuweka saini (signing), kuridhia (ratification) na tatu ni utekelezaji wa sheria kwa kutunga sheria za ndani (domestication). Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inategemea kuona serikali ikitunga sheria itakayolinda utekelezaji wa mkataba huu.

Naomba kuwasilisha,

.....  
**MASOUD A. SALIM(MB)**

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA  
ULINZI NA JESHI LAKUJENGA TAIFA**

**14.11.2018**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika ujulikanao kama *The African Charter on Statistics*.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake George Simbachawene, Mbunge wa Kibwakwe kwa ushauri walioutoa wakati wa kujadili azimio hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba azimio hili limezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati. Msingi wa azimio hili ni mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika wa mwaka 1991 ambao Tanzania iliuridhia tarehe 10 Januari,

1992 na Sheria ya Kuanzisha Umoja wa Afrika ya mwaka 2000 ambayo Tanzania iliridhia tarehe 6 Aprili 2001. Lengo kuu la nyaraka hizi mbili ni kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi za Afrika na utangamano wa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza lengo hili nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ziliona upo umuhimu wa kuwa na mfumo wa pamoja wa kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu ili kuwawezesha watunga sera na wataalam wa mipango kuwa na uelewa mpana wa viashiria vyaa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, tarehe 4 Februari, 2009 Wakuu wa Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa lengo la kuweka mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za kiuchumi, kijamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya Taifa, Kanda na Bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2017 mkataba huu ulikuwa umesainiwa na nchi 32 ikiwemo Tanzania ambayo ilisaini tarehe 23 Machi, 2012. Vilevile mnamo tarehe 31 Oktoba, 2018 Baraza la Mapinduzi la Zanzibar iliridhia mapendekazo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha mkataba huu Bungeni ili uweze kuridhiwa. Aidha, nchi 22 ya nchi hizo 32 zilikuwa zimeridhia mkataba huo na nchi kumi zilikuwa bado hazijardhia ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Takwimu wa Afrika umegawanyika katika sehemu kuu mbili ambapo sehemu ya kwanza ina sura tano na sehemu ya pili ina kipengele sita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya Kwanza yenye kipengele cha kwanza inahusu tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya mkataba huu; Sura ya Pili yenye kipengele cha pili inabainisha malengo ya mkataba ambapo

miongoni mwa malengo hayo ni pamoja na mkataba huu kutumika kama nyenzo ya muundo wa kisera katika maendeleo ya takwimu Afrika hususan katika uzalishaji usimamizi na usambazaji wa takwimu kitaifa, kikanda na kimataifa na kuimarisha mifumo ya takwimu ya nchi wanachama kwa kuhakikisha kwamba misingi ya uzalishaji, usimamizi na usambazaji wa takwimu inafuatwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya Tatu yenyе kipengele cha tatu inahusu misingi sita ya mkataba huu ambayo ni uhuru wa kitaaluma, ubora wa takwimu, mamlaka ya kutoa takwimu na upatikanaji wa rasilimali; usambazaji wa takwimu, kulinda taarifa za mtu binafsi, vyanzo vya taarifa na watoa taarifa na mwisho ni uratibu na ushirikiano wa mamlaka za takwimu kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya Nne na Sura ya Tano yenyе vipengele vya nne hadi 11 vinabainisha taratibu za utekelezaji wa mkataba katika nchi wanachama. Sehemu hizi zinabainisha umuhimu wa nchi wanachama kuweka sera, mifumo ya kitakwimu, kisheria na kitaasisi inayoendana na Mkataba wa Takwimu wa Afrika. Aidha, nchi hizo zinatakiwa kuhakikisha zinatekeleza ipasavyo mkataba huu ndani ya nchi zao pamoja na kuweka mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kikanda na Bara la Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sura hii kuitia vipengele vya nane hadi 11 vinabainisha uhusiano ndani ya mfumo wa takwimu wa Afrika ambapo wahusika katika mfumo wa takwimu wa Afrika watatakiwa kuhakikisha mfumo wa takwimu unaratibiwa katika ngazi zao ili kutoa takwimu bora kwa wadau wote na zenye uhalisia wa Bara la Afrika. Vilevile sura hii inabainisha wigo wa matumizi ya mkataba ambapo mkataba huu utatumika katika shughuli zote zinazohusu maendeleo ya kitakwimu ikiwa ni pamoja na kuratibu usambazaji wa taarifa za kitakwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya mkataba yenyе vipengele vya 12 hadi 17 pamoja na mambo mengine inabainisha mambo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza vipengele vya 12 hadi 15 na kipengele cha 17 pamoja na mambo mengine vinabainisha kuhusu mamlaka ya kutafsiri mkataba huu ambapo Mahakama ya Umoja wa Afrika au Mkutano wa Wakuu wa nchi wanachama ndio wenye mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha vipengele hivi vinaweka taratibu za kusaini na kuridhia mkataba huu ambapo utasainiwa na kuridhiwa kwa mujibu wa Katiba za nchi husika na utaanza kutumika siku 30 baada ya kuridhiwa na nchi 15. Vilevile Mwenyekiti wa Tume ya Afrika anawajibika kusajili mkataba huu Umoja wa Mataifa mara tu baada ya kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, kipengele cha 16 kinabainisha taratibu za marekebisho ya mikataba ambapo mkataba huu unatoa fursa kwa nchi wanachama kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya mkataba kwa kutoa taarifa ya kimaandishi kwa Mwenyekiti wa Tume ya Afrika ambaye atawajulisha wananchama wengine ndani ya siku 30 baada ya kupokea mapendekezo husika. Mapendekezo ya marekebisho hayo yataidhinishwa na wakuu wa nchi na kuridhiwa na nchi wanachama kwa taratibu zao za Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapendekezo ya kuridhiwa kwa mkataba huu, Serikali itawasilisha maombi maalum (*reservation*) ili kuiwezesha Tanzania kutotoa taarifa za takwimu ambazo nchi itaona zina usiri na hivyo utolewaji wake unaweza kuathiri maslahi ya taifa iwapo taarifa husika zitahitajika chini ya mkataba huu. Utaratibu huu unatambuliwa kimataifa kupitia sehemu ya pili ya Itifaki ya Vienna Convention on the Law of Treaties uliosainiwa mwaka 1969 ambapo Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizoridhia kutumia mkataba huu tangu tarehe 12 Aprili, 1976.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maelezo haya, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa nchi za Umoja wa Afrika (*AU*);

KWA KUWA wakuu wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika katika mkutano uliyofanyika tarehe 4 Februari, 2009 waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa lengo la kuweka mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za kiuchumi, kijamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya taifa, kanda na Bara zima la Afrika;

KWA KUWA hadi mwezi Juni 2017 nchi 22 ambayo ni asilimia 69 kati ya nchi 32 zilizosaini zilikuwa zimeridhia mkataba huo ambao uliana kutumika rasmi tarehe 8 Februari, 2015;

KWA KUWA Tanzania ni mojawapo ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika iliyosaini mkataba huo tarehe 23 Machi, 2012 lakini ni mionganoni mwa nchi ambazo hazijaridhia mkataba huu

KWA KUWA mkataba huu kuititia Ibara ya 14 na 15 unabainisha kwamba nchi wanachama zinapaswa kuridhia mkataba huu ili kupata nguvu za kisheria na kwamba baada ya nchi wanachama kusaini unapaswa kuridhiwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi husika na kuanza kutumika siku 30 baada ya kuridhiwa na nchi 15;

KWA KUWA Tanzania kwa kuridhia mkataba huu itafaidika na mambo yafuatayo:-

(a) Kuwa na ulinganifu ulio bora zaidi wa viashiria vya kiuchumi na kijamii baina ya nchi za Afrika; na hii ni kutokana na kuwepo kwa mfumo imara wa uzalishaji wa takwimu rasmi zinazokidhi viwango vinavyokubalika katika Mfumo wa Takwimu wa Afrika (*The African Statistical System*).

(b) Kuongezeka kwa ubora wa takwimu rasmi za Serikali na hatimaye kuongezeka kwa matumizi ya takwimu

hizo kitaifa na kimataifa, hali ambayo itachochaea uwekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini, kuongezaeka kwa mapato ya Serikali na ajira.

(c) Watakwimu nchini kuendelea kujengewa uwezo zaidi wa mbinu za kisasa za matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa takwimu rasmi zitakazohitajika katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals*) ya mwaka 2030 na ajenda ya Afrika ya mwaka 2063 kwa kutumia ushirikiano uliopo mionganoni mwa nchi wanachama wa Afrika (*South South Cooperation*); na

(d) Kuendelea kufaidika na misaada ya kibajeti na kitaalam katika kuboresha na kuimarishta tasnia ya takwimu itakayotolewa kwa Bara la Afrika na wadau mbalimbali wakiwemo wa maendeleo, sekta binafsi na wengine ikijumuisha misaada nafuu ya kuboresha mifumo ya takwimu katika ngazi mbalimbali za utawala hapa nchini.

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na mkataba huu na pia umuhimu wake kwa maendeleo ya taifa, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Tatu, na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika uitwao *The African Charter on Statistics* bila kulazimika kutoa taarifa za takwimu ambazo zitaathiri maslahi ya Taifa.

Baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako tukufu lijadili na kuridhia Azimio nililoliwasilisha ili kuiwezesha nchi yetu kunufaika na Mkataba wa Takwimu wa Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA  
DKT. PHILIP ISDOR MPANGO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI  
AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA TAKWIMU WA AFRIKA  
(THE AFRICAN CHARTER ON STATISTICS) – KAMA  
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupidisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika ujulikanao kama “**The African Charter on Statistics**”.

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kwa ushauri walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Azimio hili limezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati. Msingi wa azimio hili ni Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika wa mwaka 1991 ambao Tanzania iliuridhia tarehe 10 Januari, 1992 na Sheria ya Kuanzisha Umoja wa Afrika ya mwaka 2000 ambayo Tanzania illiridhia tarehe 6 Aprili, 2001. Lengo kuu la nyaraka hizi mbili ni kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi za Afrika na utangamano wa kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutimiza lengo hilo, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ziliona upo umuhimu wa kuwa na mfumo wa pamoja wa kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu ili kuwawezesha watunga sera na wataalam wa mipango kuwa na uelewa mpana wa viashiria vya uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo mnamo tarehe 4 Februari, 2009 Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (The African Charter on Statistics) kwa lengo la kuweka mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za kiuchumi, kijamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na

kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya Taifa, Kanda na Bara zima la Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Juni 2017 Mkataba huo ulikuwa umesainiwa na Nchi 32 ikiwemo Tanzania ambayo ilisaini tarehe 23 Machi 2012. Vile vile, mnamo tarehe 31/10/2018 Baraza la Mapinduzi la Zanzibar lilitidhia mapendeleko ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha Mkataba huu Bungeni ili uweze kuridhiwa. Aidha, Nchi 22 kati ya Nchi hizo 32 zilikuwa zimeridhia Mkataba huo na nchi 10 zilikuwa bado hazijauridhia ikiwemo Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Takwimu wa Afrika umegawanyika katika sehemu kuu mbili ambapo Sehemu ya Kwanza ina Sura 5 na Sehemu ya Pili ina vipengele Sita kama ifuatavyo;

**Sura ya Kwanza** yenyе Kipengele cha kwanza inahusu tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya Mkataba huu.

**Sura ya Pili yenyе kipengele cha 2** inabainisha malengo ya Mkataba ambapo mionganini mwa malengo hayo ni pamoja na mkataba huu kutumika kama nyenzo ya muundo wa kisera katika maendeleo ya takwimu Afrika hususan katika uzalishaji, usimamizi na usambazaji wa takwimu kitaifa, kikanda na kimataifa; Na kuimarisha mifumo ya takwimu ya nchi wanachama kwa kuhakikisha kwamba misingi ya uzalishaji, usimamizi na usambazaji wa takwimu inafuatwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika, Sura ya Tatu** yenyе kipengele cha Tatu inahusu Misingi Sita ya Mkataba huu ambayo ni Uhuru wa kitaaluma; Ubora wa Takwimu; Mamlaka ya Kutoa Takwimu na Upatikanaji wa Rasilimali; Usambazaji wa Takwimu; Kulinda Taarifa za Mtu Binafsi, Vyanzo vyya Taarifa na Watoa Taarifa na mwisho ni Uratibu na Ushirikiano wa mamlaka za Takwimu kwa nchi wanachama.

**Mheshimiwa Spika, Sura ya Nne na Tano** yenyе vipengele vya Nne hadi Kumi na moja vinabainisha taratibu za utekelezaji wa mkataba katika Nchi wanachama. Sehemu hizi zinabainisha umuhimu kwa Nchi Wanachama kuweka sera, mifumo ya kitakwimu, kisheria na kitaasisi inayoendana na Mkataba wa Takwimu wa Afrika. Aidha, Nchi hizo zinatakiwa kuhakikisha zinatekeleza ipasavyo Mkataba huu ndani ya Nchi zao pamoja na kuweka mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kikanda na bara la Afrika kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Sura hii kupitia vipengele vya Nane hadi kumi na moja vinabainisha uhusiano ndani ya mfumo wa Takwimu wa Afrika ambapo wahusika katika mfumo wa Takwimu wa Afrika watatakiwa kuhakikisha mfumo wa takwimu unaratibiwa katika ngazi zao ili kutoa takwimu bora kwa wadau wote na zenye uhalisia wa bara la Afrika. Vilevile, Sura hili inabainisha wigo wa matumizi ya mkataba ambapo mkataba huu utatumika katika shughuli zote zinazohusu maendeleo ya kitakwimu ikiwa ni pamoja na kuratibu usambazaji wa taarifa za kitakwimu.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya mkataba yenyе vipengele vya Kumi na Mbili hadi kumi na Saba pamoja na mambo mengine inabainisha yafuatayo:

(i) Vipengele vya Kumi na Mbili hadi Kumi na Tano na kipengele cha 17 pamoja na mambo mengine vinabainisha kuhusu mamlaka ya kutafsiri mkataba huu ambapo Mahakama ya Umoja wa Afrika au mukutano wa wakuu wa nchi wanachama ndiyo wenye mamlaka hiyo. Aidha, vipengele hivi vinaweka taratibu za kusaini na kuridhia mkataba huu ambapo utasainiwa na kuridhiwa kwa mujibu wa Katiba za Nchi husika na utaanza kutumika siku thelathini (30) baada ya kuridhiwa na Nchi kumi na tano (15). Vilevile, Mwenyekiti wa Tume ya Afrika anawajibika kusajili mkataba huu Umoja wa Mataifa mara tu baada ya kuanza kutumika.

(ii) Kipengele cha Kumi na Sita kinabainisha taratibu za marekebisho ya mkataba ambapo mkataba huu unatoa fursa kwa nchi Wanachama kuwasilisha mapendekezo ya

marekebisho ya Mkataba kwa kutoa taarifa ya kimaandishi kwa Mwenyekiti wa Tume ya Afrika ambaye atawajulisha wanachama wengine ndani ya siku thelathini baada ya kupokea mapendekezo husika. Mapendekezo ya marekebisho hayo yataidhinishwa na Wakuu wa Nchi na kuridhiwa na nchi wanachama kwa taratibu zao za Kikatiba.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja mapendekezo ya kuridhiwa kwa mkataba huu, Serikali itawasilisha maombi maalum (**Reservation**) ili kuiwezesha Tanzania kutotoa taarifa za takwimu ambazo nchi itaona zina usiri na hivyo utolewaji wake unaweza kuathiri maslahi ya Taifa, iwapo taarifa husika zitahitajika chini ya mkataba huu. Utaratibu huu unatambuliwa kimataifa kupitia Sehemu ya Pili ya Itifaki ya **Vienna Convention on the Law of Treaties** uliosainiwa mwaka 1969 ambapo Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizoridhia kutumia mkataba huu tangu tarehe 12 Aprili, 1976.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia maelezo haya, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika yaani "**The African Charter on Statistics**" kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Nchi za Umoja wa Afrika (AU);

**KWA KUWA** Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, katika Mkutano uliofanyika, tarehe 4 Februari, 2009 waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (The African Charter on Statistics) kwa lengo la kuweka Mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za kiuchumi, kijamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya Taifa, Kanda na Bara zima la Afrika;

**KWA KUWA** hadi Mwezi Juni, 2017 nchi 22 (asilimia 69) kati ya Nchi 32 zilizosaini zilikuwa zimeridhia Mkataba huo ambaoulianza kutumika rasmi tarehe 8 Februari, 2015;

**KWA KUWA** Tanzania ni mojawawapo ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika iliyosaini Mkataba huo tarehe 23 Machi, 2012 lakini ni mionganoni mwa nchi ambazo hazijaridhia Mkataba huu;

**KWA KUWA** Mkataba huu kupitia lbara ya 14 na 15 unabainisha kwamba, Nchi Wanachama zinapaswa kuridhia Mkataba huu ili kupata nguvu za kisheria na kwamba baada ya nchi wanachama kusaini, unapaswa kuridhiwa kwa mujibu wa Katiba za Nchi husika na kuanza kutumika siku thelathini (30) baada ya kuridhiwa na Nchi kumi na tano (15).

**NA KWA KUWA** Tanzania kwa kuridhia Mkataba huu itafaidika na mambo yafuatayo:-

- (a) Kuwa na ulinganifu ulio bora zaidi wa viashiria vya klichumi na kijamii baina ya nchi za Afrika. Hii ni kutoptera na kuwepo kwa mfumo imara wa uzalishaji takwimu rasmi zinazokidhi viwango vinavyokubalika katika Mfumo wa Takwimu wa Afrika (Africa Statistical System);
- (b) Kuongezeka kwa ubora wa takwimu rasmi za Serikali na hatimae kuongezeka kwa matumizi ya takwimu hizo kitaifa na kimataifa hali ambayo itachochea uwekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na ajira;
- (c) Watakwimu nchini kuendelea kujengewa uwezo zaidi wa mbinu za kisasa za matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa takwimu rasmi zitakazohitajika katika kufuutilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa, Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals-SDG's) ya mwaka 2030 na Agenda ya Afrika ya Mwaka 2063 kwa kutumia ushirikiano uliopo mionganoni mwa Nchi Wanachama wa Afrika (South South Cooperation); na
- (d) Kuendelea kufaidika na misaada ya kibajeti na kitaalam katika kuboresha na kuimarisha tasnia ya takwimu

itakayotolewa kwa Bara la Afrika na wadau mbali mbali wakiwemo wa maendeleo, sekta binafsi na wengine ikijumuisha misaada nafuu ya kuboresha mifumo ya takwimu katika ngazi mbalimbali za utawala hapa Nchini.

**KWA HIYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu na pia umuhimu wake kwa maendeleo ya Taifa, Bunge hili katika Mkutano wa kumi na Tatu, na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika uitwao "The African Charter on Statistics" bila kulazimika kutoa taarifa za takwimu ambazo zitaathiri maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuridhia Azimio nililowasilisha ili kuiwezesha nchi yetu kunufalka na Mkataba wa Takwimu wa Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

PIM  
WFM

**DODOMA**

Novemba, 2018.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Makamu Mwenyekiti.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa mujibu wa matakwa ya Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mwaka 2009 nchi wanachama wa Umoja wa Afrika waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa lengo la kuweka mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za uchumi, jamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya taifa, kanda na Bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi mojawapo kati ya nchi 32 zilizosaini mkataba huo tarehe 23 Machi 2012; na mpaka sasa nchi 22 zimeridhia Mkataba huo (sawa na asilimia 69) na umeanza kutumika rasmi tarehe 8 Februari, 2015. Hivyo hatua ya kuridhia mkataba huu ni kupata nguvu ya kisheria kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Azimio kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na kuunga mkono Azimio hili ambalo kimsingi litasaidia kuweka mfumo wa pamoja wa kuratibu na kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi kwa ajili ya watumiaji wa ndani na nje ya Bara la Afrika. Nchi zote duniani zinazopiga hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zinategemea upatikanaji wa takwimu sahihi ambazo uchakataji wake unasaidia watunga sera na wataalamu wa mipango kushauri ipasavyo kuhusu maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; Kamati imepitia na kujadili vipengele 17 vya Azimio hili ambavyo vimeweka misingi sita ya Azimio hili yaani uhuru wa kitaaluma, ubora wa takwimu, mamlaka ya kutoa takwimu na upatikanaji wa rasimali; usambazaji wa takwimu, kulinda na kutoa taarifa za takwimu, uratibu na ushirikiano baina ya wadau wa takwimu pamoja na utekelezaji wa Mkataba katika nchi wanachama.

Kwa mantiki hii, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta azimio hili ambalo kimsingi litasaidia kuwa na ulinganifu wa takwimu ulio bora baina ya nchi za Afrika katika viashiria vya kiuchumi na kijamii. Hatua hii itasaidia kuongeza ushindani wa maendeleo katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, madini, uzalishaji viwandani, ujenzi, utoaji wa huduma, usafirishaji, mawasiliano na huduma za fedha na hivyo kufikia Malengo ya Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 na Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Dunia ya mwaka 2030 na Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inatambua umuhimu wa takwimu kwa maendeleo ya uchumi na jamii, hatua iliyosababisha kutungwa kwa Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 (*The Statistics Act. Cap 351*) na kufanyiwa marekebisho mwaka 2018. Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa maudhui mazuri yaliyopo katika mkataba huu kwa kiwango kikubwa yamejumuishwa katika Sheria ya Takwimu iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sheria ya sasa kupitia kifungu cha nne cha sheria hiyo, imeanzisha na kuipa Ofisi ya Taifa ya Takwimu mamlaka kamili (*autonomy*) ya kutekeleza majukumu yake kama inavyoelekezwa kwenye mkataba unaopendekezwa kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sheria hiyo imeweka misingi ya kulinda na kuendeleza uadilifu (*integrity*) na kutofungamana (*impartiality*) na mtu ye yeyote au taasisi yenyenye maslahi na takwimu husika. Vilevile sheria hii imeweka utaratibu wa ukusanyaji, uchakataji, utoaji na usambazaji wa takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia azimio hili imeeleza kwa kina malengo ya mkataba unaordhiwa ambayo kimsingi yatasaidia nchi kupiga hatua katika kuzalisha, kusimamia na kusambaza taarifa za takwimu katika ngazi mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Hatua hii itasaidia kuwa na matumizi na uimarishaji bora wa takwimu

zinazotakiwa katika kusimamia uchumi na jamii ndani ya nchi pamoja na ushirikiano wa kikanda Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhiwa kwa Azimio la Mkataba huu wa Takwimu kutasaidia kujenga maadili ya watakwimu pamoja na kuboresha uratibu wa shughuli za takwimu na taasisi za takwimu. Hata hivyo Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kunakuwepo na uwazi, ubora na usahihi wa utolewaji wa taarifa za kitakwimu pamoja na matumizi yake kutoka kwa wadau ambao watapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia azimio hili, watakwimu watakuwa na uhuru wa kitaaluma wa kutekeleza majukumu yao bila ya kuingiliwa na mamlaka ya kisiasa au kundi lolote lenye maslahi na takwimu. Pamoja na hatua hii nzuri ya uhuru wa watakwimu, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa shughuli za watakwimu zinazingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi hii ili misingi ya mkataba huu itekelezwe bila kuwepo na mgongano wa kimaslahi kwa watoaji na watumiaji wa takwimu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuwa kupitia azimio hili ianze kuweka mikakati mbalimbali ya kuondoa au kupunguza changamoto mbalimbali zilizopo katika uzalishaji wa takwimu kama vile uhaba wa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa takwimu, ukosefu wa uhakika wa teknolojia za kisasa, kutofanyika kwa tafiti kwa mujibu wa kalenda za utafiti, pamoja na upungufu wa matumizi ya takwimu za kiutawala. Hatua hii itasaidia kuimarisha na kuratibu uzalishaji na utolewaji wa takwimu bora zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera pamoja na mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kuwa kuridhiwa kwa Mkataba huu wa Takwimu, Tanzania kama nchi mwanachama itawajibika kuhakikisha mamlaka za takwimu zinakuwa na rasilimali za kutosha na za kuaminika ili kuwezesha kutimiza matakwa ya takwimu kitaifa, kikanda

na kwa Bara la Afrika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuanza kufikiria kutenga rasilimali watu, nyenzo na fedha za kutosha ambazo zitatakiwa kutumika kwa uangalifu na hivyo kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka za Takwimu, watakamu na wote wanaojishughulisha na tasnia ya takwimu wanapaswa kuhakikisha uwepo wa ulinzi wa maisha binafsi, siri za kibiasara za watoa taarifa kama vile makampuni, taasisi za umma na kadhalika, usiri wa taarifa zilizotolewa na taarifa hizo zitumike kwa malengo ya takwimu tu. Aidha, taarifa zinazomhusu mtu au taasisi zilizokusanywa kwa ajili ya takwimu kwa namna yoyote ile zisitumike katika mwenendo wa mahakama, hatua za adhabu au kufanya maamuzi ya kiutawala dhidi ya mtoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali, Mkataba huu wa Takwimu utahifadhiwa katika lugha ya rasmi za Kiarabu, Kiingereza, Kireno, na Kifaransa. Kamati inaishauri Serikali kusimamia na kuhakikisha kuwa Mkataba huu unahifadhiwa pia katika lugha ya kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati hapo juu, Kamati inaona kuwa mkataba huu ukiridhiwa utakuwa na manufaa kwa maendeleo ya taifa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kutakuwepo na uhakika wa ulinganifu wa takwimu ulio bora zaidi wa viashiria vya kiuchumi na kijamii baina ya nchi za Afrika kutokana na kuwepo kwa mfumo imara wa uzalishaji takwimu rasmi zinazokidhi viwango inavyokubalika katika mfumo wa Takwimu wa Afrika (*Africa Statistical System*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili kutaongezeka ubora wa takwimu rasmi za Serikali na hatimaye kuongezeka kwa matumizi ya takwimu hizo za kitaifa na kimataifa. Hali hiyo

itachochea uwekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini kuongezeka kwa mapato ya Serikali na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, watakwimu nchini watajengewa uwezo zaidi wa mbinu za kisasa za matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa takwimu rasmi zitakazohitajika katika kufuatilia na kutathimini viashiria vyatki chumi na kijamii kwa kutumia ushirikiano ulipo miungoni mwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne nchi itaendelea kufaidika na misaada ya kibajeti na kitaalam katika kuboresha na kuimarisha tasinia ya takwimu itakayotolewa katika Bara la Afrika na wadau mbalimbali wakiwemo wa maendeleo, sekta binafsi na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tano nchi itakuwa na fursa ya kupata misaada ya kibajeti na kitaalam katika kuboresha na kuimarisha mifumo ya kitakwimu katika ngazi mbalimbali za utawala nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa fursa kuwasilisha taarifa hi ya Kamati. Vilevile naomba nimshukuru Dkt. Philip Mpango - Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijiji, Mbunge na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao waliota kwa Kamati. Pia napenda kumshukuru Dkt. Albina Chuwa Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takkumu ya Taifa pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ulioutoa katika kipindi chote cha kuchambua na kupitia azimio hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa umahili wao katika kupitia na kujadili azimio hili na kuweza kuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba watambuliwe kama walivyo kwenye hotuba hii kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Godfrey Godwin, Ndugu Emmanuel Robby, Ndugu Lilian Masabala na Ndugu Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata napenda pia kuwashukuru Wanasheria Ofisi ya Bunge, Ndugu Mossy Lukuvi, Ndugu Matamus Fungo, Ndugu Nesta Kawamala, Ndugu Stephano Mbutu, Ndugu Thomas Shawa na Ndugu Maria Mdulugu kwa kutoa ushauri wao wa kisheria uliosaidia kukamisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Kamati imetafakari kwa kina manufaa yatokanayo na mkataba huu pamoja na umuhimu wake kwa maendeleo ya Taifa na hivyo inalishauri Bunge lako tukufu liazimie na kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kama ulivyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono azimio hili. (*Makofii*)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BAJETI KUHUSU AZIMIO  
LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA TAKWIMU WA AFRIKA  
(THE AFRICAN CHARTER ON STATISTICS) – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0      UTANGULIZI**

**1.1      Mheshimiwa Spika**, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter*

on Statistics) kwa mujibu wa matakwa ya Ibara 63(3)(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**1.2 Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba mwaka 2009 Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa lengo la kuweka Mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za uchumi, jamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya Taifa, Kanda na Bara zima la Afrika.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni nchi mojawapo kati ya nchi 32 zilizosaini mkataba huo tarehe 23 Machi 2012; na mpaka sasa nchi 22 zimeridhia Mkataba huo (sawa na asilimia 69) na umeanza kutumika rasmi tarehe 08 Februari, 2015. Hivyo hatua ya kuridhia mkataba huu ni kupata nguvu ya kisheria kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Azimio kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**1.4 Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na kuunga mkono Azimio hili ambalo kimsingi litasaidia kuweka mfumo wa pamoja wa kuratibu na kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi kwa ajili ya watumiaji wa ndani na nje ya Bara la Afrika. Nchi zote duniani zinazopiga hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zinategemea upatikanaji wa takwimu sahihi ambazo uchakataji wake unasaidia watunga sera na wataalamu wa mipango kushauri ipasavyo kuhusu maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.

## **2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA TAKWIMU WA AFRIKA (*THE CHARTER ON STATISTICS*).**

**Mheshimiwa spika**, Kamati imepitia na kujadili vipengele 17 vya Azimio hili ambayo vimeweka misingi Sita ya Azimio hili yaani; uhuru wa kitaaluma, ubora wa takwimu, mamlaka ya kutoa takwimu na upatikanaji wa rasimali, usambazaji

wa takwimu, kulinda na kutoa taarifa za takwimu, uratibu na ushirikiano baina ya wadau wa takwimu pamoja na utekelezaji wa Makataba katika Nchi Wanachama. Kwa mantiki hii Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

**2.1 Mheshimiwa Spika**, kamati inapongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili ambalo kimsingi litasaidia kuwa na ulinganifu wa takwimu ulio bora baina ya nchi za Afrika katika viashiria vya kiuchumi na kijamii. Hatua hii itasaidia kuongeza ushindani wa maendeleo katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, madini, uzalishaji viwandani, ujenzi, utoaji wa huduma, usafirishaji, mawasiliano na huduma za fedha na hivyo kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na malengo endelevu ya Maendeleo ya Dunia ya Mwaka 2030 na Agenda ya Afrika ya Mwaka 2063.

**2.2 Mheshimiwa Spika**, Tanzania inatambua umuhimu wa takwimu kwa maendeleo ya uchumi na jamii hatua iliyosababisha kutungwa kwa Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2015 (The Statistics Act. Cap 351) na kufanyiwa marekebisho mwaka 2018. Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa maudhui mazuri yaliyopo katika Mkataba huu kwa Kiwango kikubwa yamejumuishwa katika Sheria ya Takwimu iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2018. Kwa mfano Sheria ya Sasa kuititia kifungu cha Nne (4) cha Sheria hiyo, imanzisha na kuipa Ofisi ya Taifa ya Takwimu mamlaka kamili (*autonomous*) ya kutekeleza majukumu yake kama inavyoelekezwa kwenye Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Sheria hiyo imeweka misingi ya kulinda na kuendeleza uadilifu (*integrity*) na kutofungamana (*impartiality*) na mtu yoyote au taasisi yenye maslahi na takwimu husika. Vilevile Sheria hii imeweka utaratibu wa ukusanyaji, uchakataji, utoaji na usambazaji wa takwimu.

**2.3 Mheshimiwa Spika**, Serikali kuititia Azimio hili imeeleza kwa kina malengo ya Mkataba unaoridhiwa ambayo kimsingi yatasaidia nchi kupiga hatua katika kuzalisha, kusimamia

na kusambaza taarifa za takwimu katika ngazi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Hatua hii itasaidia kuwa na matumizi na uimarishaji bora wa takwimu zinazotakiwa katika kusimamia uchumi na jamii ndani ya nchi pamoja na ushirikiano wa kikanda barani Afrika.

**2.4 Mheshimiwa Spika**, kuridhiwa kwa azimio la Mkataba huu wa Takwimu kutasaidia kujenga maadili ya watakwimu pamoja na kuboresha uratibu wa shughuli za takwimu na taasisi za takwimu. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kunakuwepo na uwazi, ubora na usahihi wa utolewaji wa taarifa za kitakwimu pamoja na matumizi yake kutoka kwa wadau ambao watapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi.

**2.5 Mheshimiwa Spika**, kuititia Azimio hili, Watakwimu watakuwa na uhuru wa kitaaluma wa kutekeleza majukumu yao bila ya kuingiliwa na mamlaka ya kisasa au kundi lolote lenye maslahi na Takwimu. Pamoja na hatua hii nzuri ya uhuru wa Watakwimu, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa shughuli za Watakwimu zinazingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi ili misingi ya Mkataba huu itekelezwe bila kuwepo na mgongano wa kimaslahi kwa watoaji na watumiaji wa takwimu ndani na nje ya nchi.

**2.6 Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuwa kuititia Azimio hili ianze kuweka mikakati mbalimbali ya kuondoa au kupunguza changamoto mbalimbali zilizopo katika uzalishaji wa takwimu kama vile uhaba wa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa takwimu, ukosefu wa uhakika wa teknolojia za kisasa, kutofanyika kwa tafiti kwa mujibu wa kalenda za utafiti, pamoja na upungufu wa matumizi ya takwimu za kiutawala. Hatua hii itasaidia kuimarisha na kuratibu uzalishaji na utolewaji wa takwimu bora zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera pamoja na mipango ya maendeleo.

**2.7 Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa kuridhiwa kwa Mkataba huu wa Takwimu, Tanzania kama Nchi mwanachama itawajibika kuhakikisha Mamlaka za

takwimu zinakuwa na rasilimali za kutosha na za kuaminika ili kuwezesha kutimiza matakwa ya takwimu kitaifa, kikanda na kwa Bara la Afrika. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuanza kufikiria kutenga rasilimali watu, nyenzo na fedha za kutosha ambazo zitatakiwa kutumika kwa uangalifu na hivyo kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

**2.8 Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka za Takwimu, watakwimu na wote wanaojishughulisha na tasnia ya takwimu wanapaswa kuhakikisha uwepo wa ulinzi wa maisha binafsi, siri za kibiasara za watoa taarifa kama vile makampuni, taasisi za umma n.k, usiri wa taarifa zilizotolewa na taarifa hizo zitumike kwa malengo ya takwimu tu. Aidha, taarifa zinazomhusu mtu au taasisi zilizokusanywa kwa ajili ya takwimu kwa namna yoyote ile zisitumike katika mwenendo wa mahakama, hatua za adhabu au kufanya maamuzi ya kiutawala dhidi ya mtoa taarifa.

**2.9 Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali, Mkataba huu wa Takwimu utahifadhiwa katika lugha ya rasmi ya Kiarabu, Kiingereza, Kireno, na Kifaransa. Kamati inashauri Serikali kusimamia na kuhakikisha kuwa Mkataba huu unahifadhiwa pia katika lugha ya Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati hapo juu, Kamati inaona kuwa Mkataba huu ukiridhiwa utakuwa na manufaa kwa maendeleo ya Taifa kuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni kama ifuatavyo:-

- i) Kutakuwepo na uhakika wa ulinganifu wa takwimu ulio bora zaidi wa viashiria vyta kiuchumi na kijamii baina ya nchi za Afrika; Kutohana na kuwepo kwa mfumo imara wa uzalishaji takwimu rasmi zinazokidhi viwango vinavyokubalika katika mfumo wa Takwimu wa Afrika (*Africa Statistical System*);
- ii) Kutaongezeka ubora wa takwimu rasmi za Serikali na hatimaye kuongezeka kwa matumizi ya takwimu hizo kitaifa na kimataifa. Hali hiyo itachochea uwekezaji wa

ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na ajira;

iii) Watakwimu nchini watajengewa uwezo zaidi wa mbinu za kisasa za matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa takwimu rasmi zitakazohitajika katika kufuatilia na kutathimini viashiria vya kiuchumi na kijamii kwa kutumia ushirikiano uliopo miongoni mwa nchi wanachama;

iv) Nchi itaendelea kufaidika na misaada ya kibajeti na kitaalam katika kuboresha na kuimarisha tasnia ya takwimu itakayotolewa katika Bara la Afrika na wadau wa mbalimbali wakiwemo wa maendeleo, sekta binafsi na wengine; na

v) Nchi itakuwa na fursa ya kupata misaada ya kibajeti na kitaalamu katika kuboresha na kuimarisha mifumo ya takwimu katika ngazi mbalimbali zautawala Nchini.

### 3.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa miongozo yako na kunipa fursa kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Naibu Spika kwa miongozo yake. Vilevile, napenda nimshukuru Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Pia napenda kumshukuru Dkt. Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa katika kipindi chote cha kuchambua na kupitia Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kupitia na kujadili Azimio hili na

kuweza kuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo;

- 1.Mhe. George B. Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
- 2.Mhe. Mashimba M.Ndaki, Mb – Makamu Mwenyekiti
- 3.Mhe. David Ernest Silinde, Mb
- 4.Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
- 5.Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
- 6.Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
- 7.Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
- 8.Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
- 9.Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
- 10.Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
- 11.Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
- 12.Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
- 13.Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb
- 14.Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
- 15.Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
- 16.Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb
- 17.Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
- 18.Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
- 19.Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
- 20.Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
21. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
- 22.Mhe. Andrew John Chenge, Mb
- 23.Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb
- 24.Mhe. Shally J. Raymond, Mb
- 25.Mhe. Hussein M. Bashe, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndgg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala, Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda pia kuwashukuru Wanasheria wa Ofisi ya Bunge Ndg. Mossy Lukuvi, Matamus Fungo, Nesta Kawamala, Stephano Mbutu, Thomas Shawa na Maria Mdulugu kwa kutoa ushauri wao wa kisheria uliosaidia kukamilisha kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, Kamati imetafakari kwa kina manufaa yatokanayo na Mkataba huu pamoja na umuhimu wake kwa maendeleo ya Taifa na hivyo inashauri Bunge lako tukufu liazmie na kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kama ilivyowasilishwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.

Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb.

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

14 Novemba, 2018

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti, sasa nimwite mseji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) na Nyongeza ya Nane Kanuni ya 7(1)(b) ya Kanuni za Bunge toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Halima Mdee kuhusu azimio la Bunge la kuridhia mkataba wa takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza, mkataba wa Afrika kuhusu masuala ya takwimu ulipitishwa na mukutano wa kawaida wa wakuu wa nchi na Serikali wa

Umoja wa Afrika tarehe 3 Februari, 2009. Katika hali ya kushangaza ni miaka tisa baadae ndipo Serikali inawasilisha katika Bunge lako tukufu azimio kwa ajili ya Bunge kuridhia Mkataba huu kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na mambo mengine, ibara hiyo inalipa Bunge lako tukufu mamlaka ya kuridhia mikataba ya kimataifa inayosainiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mkataba huu yameelezwa katika dibaji ya mkataba kuwa ni kuhuisha takwimu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa malengo ya Umoja wa Afrika yanatekelezwa na kufikiwa pamoja na kuhakikisha kuwa ombwe la uhitaji au upatikanaji wa takwimu kwa kulinganisha na uwepo wa takwimu kwa sasa linazibwa ili kuwepo na urahisi wa wadau kuweza kupata takwimu kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mkataba huu ni mwongozo wa kisera kwa Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kufanya maamuzi kwa maslahi ya umma. Ni katika msingi huo kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha kuwa tunakuwa na mfumo na utaratibu bora wa kusimamia na kutumia takwimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu pili ya mkataba ni uchambuzi; ibara ya tatu ya mkataba inaweka misingi mikuu kwa ajili ya taasisi zinazojihusisha na takwimu ikiwemo uwazi, ukweli, uwajibikaji pamoja na uhuru katika utendaji kazi wa taasisi hizo. Misingi hii ni muhimu hasa kwa nchi yetu ambapo tumeshuhudia baadhi ya taasisi zikiwa hazina nguvu na badala yake zinategemea maelekezo kutoka juu. Ni muhimu kwa taasisi zetu kueleza na kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya kusaidia mamlaka za kufanya maamuzi ikiwemo Bunge kuhakikisha kuwa maamuzi yanafanyika kulingana na hali halisi iliyopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya nne inatoa haki ya kupatikana kwa takwimu bila vikwazo vyoyote. Aidha, sheria za nchi washirika zinatakiwa kuhakikisha kuwa masharti ya sheria zake zinatoa haki hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani

inatambua kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ndiyo yenyeye mamlaka ya kusimamia masuala ya takwimu nchini lakini pia tunatambua kuwa ofisi hiyo inashirikiana na taasisi nyingine za Serikali kuhakikisha kuwa kunakuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na sintofahamu kwa muda mrefu sasa ambapo Benki Kuu ya Tanzania inatakiwa kutoa taarifa za hali ya uchumi ambapo mara kadhaa wadau wamekuwa wakilalamika kuwa taarifa hizo zimekuwa hazitolewi kwa wakati au hazitolewi kabisa kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mkataba huu unatoa haki ya kupata takwimu na Benki Kuu ambayo ni mdau muhimu kwa ajili ya takwimu za kiuchumi inatoa takwimu kama wanavyotaka kinyume na sheria inavyotaka, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa bila kuwa na nia ya dhati ya kisiasa na kisheria mkataba huu hautatekelezwa kikamilifu na Serikali hii ya awamu ya tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya tano inatoa jukumu kwa mamlaka za takwimu kuhakikisha kuwa zinawalinda watoa takwimu pamoja na kuhakikisha kuwa wanaelezwa mapema kabla ya kutoa taarifa kuwa taarifa wanazozitoa zitakuwa siri. Kambi Rasmi ya Upinzani haina tataizo na kifungu hiki kwa kuwa huu ni msingi muhimu katika kufanya tafiti kwa ajili ya kukusanya taarifa za takwimu. Hii ni kwa sababu bila mtoa takwimu kulindwa kutakuwa na shida ya upatikanaji wa takwimu kwa sababu hakutakuwa na uhuru katika kutoa taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu; mkataba wa takwimu na sheria zetu hapa nchini. Mwaka 2015 Bunge lako tukufu lilitunga Sheria ya Takwimu Sura ya 351 ambapo pamoja na mambo mengine sheria hiyo ilitungwa nyakati hizo hizo pamoja Sheria ya Makosa ya Mtandao ambazo kwa sasa zimekuwa mwiba mkali sana katika kudhibiti vyombo vyaa habari pamoja na uhuru wa wananchi kutoa maoni kwa mujibu wa ibara ya 18 ya Katiba ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 25 pamoja na 37 vya Sheria ya Takwimu vililalamikiwa sana hasa na wadau wa vyombo vya habari pamoja na vyama vya siasa kuwa vitazuia kabisa uhuru wa kutoa na kupokea habari pamoja na kutoa maoni kwa sababu vimeweka makatazo kadhaa pamoja na adhabu kwa wanaokiuka vifungu hivyo ambapo wahanga wakubwa ni wadau hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka mmoja baadae baada ya Serikali ya Awamu ya Tano baada ya kuingia madarakani ilitunga Sheria ya Huduma kwa Vyombo vya Habari ambapo na yenyele pamoja na kulalamikiwa na wadau imeendelea kuwa mwiba mchungu hasa kwa wanasiasa wa upinzani kupewa mashtaka ya uchochezi kwa mujibu wa kifungu cha 52 na 53 cha sheria hiyo yanayohusisha takwimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapungufu ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015, katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge hili Serikali iliwasilisha tena Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambapo pamoja na sheria zingine Sheria ya Takwimu ilikuwa moja ya sheria zilizofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya ya sheria yamevuta mjadala mkubwa nchini ikiwa ni pamoja na wadau wa maendeleo kutishia kuzuia misaada ya kibajeti kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ielete mbele ya Bunge lako tukufu kuhusu athari za marekebisho ya kifungu cha 24 kwa kuongeza kifungu cha 24(a) na (b). Naomba kunukuu baadhi ya ushauri wetu katika maoni hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; marekebisho yanayopendekezwa kufanyaika kwenye Sheria ya Takwimu yamejikita katika kudhitibi tafiti zitakazokuwa zinafanyaika na kuwanyima wananchi nafasi ya kujua matokeo halisi ya tafiti hizo.

Mbili, kwamba mapendekezo ya marekebisho ya sheria yanapoteza dhana ya kufanya utafiti (*social science research*) na matokeo yake kuwafikia wananchi husika wa tafiti hiyo kwani kabla ya kuanza kutumika au kuwafikiwa wananchi, mtao takwimu anatakiwa aombe kibali kwa Mtakwimu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwamba kifungu kipyaa cha 24(a) kwenye Sheria ya Takwimu kinatoa masharti kuwa kabla ya taarifa ya takwimu kutolewa ni lazima kibali kitolewe na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Nne, kwamba marekebisho hayo yanamlazimisha mtafiti yejote kabla ya kutoa matokeo ya utafiti wake afanye mashauriano na Ofisi ya Takwimu. Kambi ya Upinzani iliona kuwa katika mashauriano haya kuna uwezekano mkubwa mtafiti kurekebisha matokeo ya utafiti wa takwimu ili ziandane na matakwa ya Ofisi ya Takwimu au kufutwa kwa utafiti husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la utafiti na hatimaye takwimu kutolewa ni kutafuta suluhisho la tatizo na si kushindana na Serikali, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inashangazwa na wasiwasi wa Serikali katika masuala ya Takwimu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Takwimu zina mapungufu ambayo hawatakiwi Watanzania kuyafahamu na hivyo kukiuka azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2018 yana lengo la kuwafanya watendaji wa Serikali mara zote wawe kwenye *comfort zone* yaani wasiweze kuwajibika. Tukumbuke kwamba wanaofanya kazi hiyo ni binadamu na makosa ni sehemu ya maisha na ndiyo maana mkataba huu ibara ya nne unatoa nafasi ya kufanya marekebisho ya takwimu ambazo zinaweza kutolewa kwa makosa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wa maendeleo wameona mapungufu ya Sheria ya Takwimu pamoja na marekebisho ya sheria hiyo ya mwaka 2018 ambapo baadhi yao wametishia kuondoa fedha za misaada ya kibajeti kwa

Serikali na hatimaye kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa hili ni jambo kubwa ambapo Serikali inatakiwa kuchukua hatua za dharura pamoja na kuwa tuliwashauri wafute vifungu hivyo ambavyo vinakiuka uhuru wa kutoa na kupokea habari pamoja na kupoteza na kaharibu dhana na umuhimu wa utafiti na takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne; hitimisho, ili azimio hili liwe na manufaa kwetu kama nchi ni vema Serikali ikawasilisha sheria nyininge ya takwimu na kufuta ile ya mwaka 2015 na marekebisho yake ya mwaka 2018 ili ziendane na masharti ya mkataba huu pamoja na kufuta vifungu ambavyo kwa namna moja ama nyininge vinakiuka misingi ya haki za binadamu ikiwemo ya kupata na kupokea habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Ahsante. (*Makofii*)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO  
MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE KUHUSU AZIMIO LA  
BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA TAKWIMU WA AFRIKA  
YAANI THE AFRICAN CHARTER ON STATISTICS - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**[*(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) na Nyongeza ya Nane,  
Kanuni ya 7(1)(b) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari,  
2016]*]**

**1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Afrika kuhusu masuala ya takwimu ulipitishwa na Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika tarehe 03 Februari, 2009. Katika hali ya kushangaza ni miaka tisa baadae ndipo Serikali inawasilisha katika Bunge lako tukufu azimio kwa ajili ya Bunge kuridhia Mkataba huu kwa mujibu wa Ibara ya

63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na mambo mengine; ibara hiyo inalipa Bunge lako tukufu mamlaka ya kuridhia mikataba ya Kimataifa inayosainiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Malengo ya Mkataba huu yameelezwa katika Dibaji ya Mkataba kuwa ni kuhuisha takwimu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa malengo ya Umoja ya Afrika yanatekelezwa na kufikiwa pamoja na kuhakikisha kuwa ombwe la uhitaji au upatikanaji wa takwimu kwa kulinganisha na uwepo wa takwimu kwa sasa linazibwa ili kuwe na urahisi wa wadau kuweza kupata takwimu kirahisi.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Mkataba huu ni mwongozo wa kisera kwa Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kufanya maamuzi kwa maslahi ya umma. Ni katika msingi huo, kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha kuwa tunakuwa na mfumo na utaratibu bora wa kusimamia na kutumia takwimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

## 2. UCHAMBUZI WA MKATABA

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 3 ya Mkataba inaweka misingi mikuu kwa ajili ya taasisi zinazojihusisha na takwimu ikiwemo uwazi, ukweli, uwajibikaji pamoja uhuru katika utendaji kazi wa taasisi hizo. Misingi hii ni muhimu hasa kwa nchi yetu ambapo tumeshuhudia baadhi ya taasisi zikiwa hazina nguvu na badala yake “**zinategemea maelekezo kutoka juu**”. Ni muhimu kwa taasisi zetu kueleza na kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya kusaidia mamlaka za kufanya maamuzi likiwemo Bunge kuhakikisha kuwa maamuzi yanafanyika kulingana na hali halisi iliyopo.

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya 4 inatoa haki ya kupatikana kwa takwimu bila vikwazo vyoyote aidha Sheria za nchi washirika zinatakiwa kuhakikisha kuwa masharti ya Sheria zake zinatoa haki hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia masuala ya Takwimu nchini lakini pia tunatambua kuwa Ofisi hiyo inashirikiana na taasisi nyingine za Serikali kuhakikisha

kuwa kunakuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na sintofahamu kwa muda mrefu sasa ambapo Benki Kuu ya Tanzania inatakiwa kutoa taarifa za hali ya uchumi ambapo mara kadhaa wadau wamekuwa wakilalamika kuwa taarifa hizo zimekuwa hazitolewi kwa wakati au hazitolewi kabisa kwa umma. Kama Mkataba huu unatoa haki ya kupata takwimu na Benki Kuu ambayo ni mdau muhimu kwa ajili ya takwimu za kiuchumi inatoa takwimu kama wanavyotaka kinyume na sheria inavyotaka, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa bila kuwa na nia ya dhati ya kisiasa na kisheria mkataba huu hautatekelezwa kikamilifu na Serikali hii ya awamu ya tano.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 05 inatoa jukumu kwa mamlaka za takwimu kuhakikisha kuwa zinawalinda watoa takwimu pamoja na kuhakikisha kuwa wanaelezwa mapema kabla ya kutoa taarifa kuwa taarifa wanazozitoa zitakuwa siri. Kambi Rasmi ya Upinzani haina tataizo na kifungu hiki kwa kuwa huu ni msingi muhimu katika kufanya tafiti kwa ajili ya kukusanya taarifa za takwimu. Hii ni kwa sababu bila mtoe takwimu kulindwa kutakuwa na shida ya upatikanaji wa takwimu kwa sababu hawatakuwa huru kutoa taarifa hizo.

### **3. MKATABA WA TAKWIMU NA SHERIA ZETU**

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2015 Bunge lako tukufu lilitunga Sheria ya Takwimu Sura ya 351ambapo pamoja na mambo mengine Sheria hiyo ilitungwa nyakati hizo hizo pamoja Sheria ya Makosa ya Mtandao ambazo kwa sasa zimekuwa mwiba mkali katika kudhibiti vyombo vya habari pamoja na uhuru wa wananchi kutoa maoni kwa mujibu wa ibara ya 18 ya Katiba ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 25 pamoja na 37 vya Sheria ya Takwimu vililalamikiwa sana hasa na Wadau wa Vyombo vya Habari pamoja na Vyama Vya Siasa kuwa vitazuia kabisa uhuru wa kutoa na kupokea habari pamoja na kutoa maoni kwa sababu vimeweka makatazo kadhaa pamoja na

adhabu kwa wanaokiuka vifungu hivyo ambapo wahanga wakubwa ni wadau hao.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka mmoja baadae baada ya Serikali ya awamu ya tano kuingia madarakan iitungwa Sheria ya Huduma kwa Vyombo vyta Habari ambayo na yenye we pamoja na kulalamikiwa na wadau imeendelea kuwa mwiba mchungu hasa kwa wanasiwa wa Upinzani kupewa mashtaka ya uchochezi kwa mujibuwa kifungu cha 52 na 53 cha Sheria hiyo yanayohusisha takwimu.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mapungufu ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015, katika mkuu wa 12 wa Bunge hili Serikali iliwasilisha tena muswada wa marekebisho ya Sheria mbalimbali ambapo pamoja na Sheria zingine Sheria ya Takwimu ilikuwa moja ya Sheria zilizofanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho hayo ya Sheria yamevuta mjadala mkubwa nchini ikiwa ni pamoja na wadau wa maendeleo kutishia kuzuia misaada ya kibajeti kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Serikali ilieleza mbele ya Bunge lako tukufu kuhusu athari za marekebisho ya kifungu cha 24 kwa kuongeza kifungu cha 24A na B, naomba kunukuu baadhi ya ushauri wetu katika maoni hayo kama ifuatavyo;

(1) Marekebisho yanayopendekezwa kufanya kwenye sheria ya takwimu yamejikita katika kudhitibi tafiti zitakazokuwa zinafanya na kuwanyima wananchi nafasi ya kujuu matokeo halisi ya tafiti hizo.

(2) Kwamba, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria yanapoteza dhana ya kufanya utafiti "Social Science Research" na matokeo yake kuwafikia wananchi husika wa tafiti hiyo. Kwani kabla ya kuanza kutumika au kuwafikiwa wananchi, Mtao Takwimu anatakiwa aombe kibali kwa Mtakwimu Mkuu.

(3) Kwamba, kifungu kipyaa cha 24A kwenye sheria ya Takwimu kinatoa masharti kuwa kabla ya taarifa ya takwimu kutolewa nilazima kibali kitolewe na ofisi ya Taifa ya Takwimu.

(4) Kwamba, marekebisho hayo yanamlazimisha mtafiti yeoyote kabla ya kutoa matokeo ya utafiti wake afanye mashauriano na Ofisi ya Takwimu. Kambi Rasmi ya Upinzani iliona kuwa katika mashauriano hayo kuna uwezekano mkubwa Mtafiti kurekebisha matokeo ya utafiti na takwimu ili ziandane na matakwa ya Ofisi ya Takwimu au kufutwa kwa utafiti husika.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la utafiti na hatimaye takwimu kutolewa ni kutafuta suluhisho la tatizo na sio kushindana na Serikali, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inashangazwa na wasiwasini wa Serikali katika masuala ya Takwimu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Takwimu zina mapungufu ambayo hawatakiwi watanzania wayafahamu na hivyo kukiuka azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2018 yana lengo la kuwafanya watendaji wa Serikali wake mara zote wawe kwenye "**comfort zone**" yaani wasiweze kuwajibika. Tukumbuke kwamba wanaofanya kazi hiyo ni binadamu na makosa ni sehemu ya maisha, na ndiyo maana Mkataba huu ibara ya 4 unatoa nafasi ya kufanya marekebisho ya takwimu ambazo zinaweza kutolewa kwa makosa.

**Mheshimiwa Spika**, Wadau wa maendeleo wameona mapungufu ya Sheria ya Takwimu pamoja na marekebisho ya Sheria hiyo ya mwaka 2018 ambapo baadhi yao wametishia kuondoa fedha za misaada ya kibajeti kwa Serikali na hatimaye kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa hili ni jambo kubwa ambapo Serikali inatakiwa kuchukua hatua za dharura pamoja na kuwa tuliwashauri wafute vifungu hivyo ambavyo vinakiuka uhuru wa kutoa na kupokea habari

pamoja na kupoteza na kaharibu dhana na umuhimu wa utafiti na takwimu.

#### 4. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Ili azimio hili liwe na manufaa kwetu kama nchi ni vema Serikali ikawasilisha Sheria nyingine ya takwimu na kufuta ile ya mwaka 2015 na marekebisho yake ya mwaka 2018 ili ziendane na masharti ya mkataba huu pamoja na kufuta vifungu ambavyo kwa namna moja ama nyingine vinakiuka misingi ya haki za binadamu ikiwemo ya kupata na kupokea habari.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema, naomba kuwasilisha.

---

**Halima James Mdee (Mb)**

WAZIRI KIVULI NA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA  
UPINZANI- WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

14 Novemba, 2018

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumeshasikia maoni ya Kamati ambayo ilifanya kazi kwa niaba yetu, kwa maana ya Kamati zote mbili, lakini pia tumesikia maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu maazimio yote mawili. Sasa nimepata majina hapa kwa ajili ya wachangiaji kwenye mikataba yote miwili. Tutaanza uchangiaji wetu kama ifuatavyo:-

Tutaanza na Mheshimiwa Ally Saleh, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Philip Mbogo.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi nimechaguliwa na Kambi nizungumzie juu ya muswada unaohusu silaha za kibaiolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jana tu kulikuwa na suala nafikiri la Mheshimiwa Neema Mgaya juu ya mkataba au azimio la demokrasia chaguzi na utawala bora ambapo

alisema kwamba tulishiriki katika kupidisha azimio hilo miaka sita nyuma lakini mpaka leo hatujaridhia mkataba huo. Ninaanza hapo kwa sababu nimekuwa nikisema mara kadhaa kwamba kama nchi tumekuwa tukikaa nyuma sana katika kuridhia mikataba ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikisema kuna mikataba muhimu ambayo kama nchi tumekuwa hatuingii kwa wakati. Moja ya mkataba ambao naweza kukumbuka haraka ni Mkataba wa Kimataifa Juu ya Wafanyakazi wa Nyumbani (*International Conventions on Domestic Worker*). Tanzania kama nchi tumekuwa tukilalamika kwamba wafanyakazi wetu wengi wakienda nje ya nchi hawapati *treatment* ambayo inayostahiki kama inavyotakiwa, lakini sisi wenyewe hatujaingia katika mikataba na hapa hatujaingia katika maazimio ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili linatokana na mkataba wa kwanza wa mwaka wa 1925 ambao ulikuwa zaidi uki-deal/na suala la *biologically weapons* lakini baadae hii ya sasa mkataba huu wa mwaka 1972 ukaongeza na *toxic weapons*. Sasa sisi kama nchi tulishiriki tangu hatua ya kwanza mwaka 1972, lakini imetuchukua miaka 46 sasa kuja kuridhia azimio hili. Kwa hiyo, nahisi kwamba hii inatuweka nyuma na kama sasa tunazungumzia juu ya faida ambazo zinaweza kupatikana, *contract* ambazo zimepatikana lakini imetuchukua miaka 46 kuamua kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninaamini kwamba kama nchi kama Taifa tuna mikataba mingine mingi tu ambayo tunapaswa tuingia ambapo kama huu mkataba gharama yake ni dola 100 tu kwa mwaka, lakini faida unayopata ni kubwa sana, lakini pia tunaingia katika mtandao ambao ungeweza kutusaidia. Tushukuru kwamba kwa wazi kabisa hatuonekani kama tumetatzwa na suala hili, lakini kama niliviyosema katika Kambi ya Upinzani ingewezekana vitu kama hivi kuweza kutokezea kwa sababu ya maradhi mengine mbalimbali ambayo yangeweza yakageuzwa kuwa silaha katika eneo hili kama vile Kimeta na mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nafikiri kuna haja ya kama Taifa kulitazama suala hili kwa sababu suala la sisi kufafananishwa na Syria na Haiti au na Somalia katika nchi ambazo mpaka sasa hivi hazijaridhia mkataba huu kwa kweli haileti sura nzuri kwa Tanzania. Hatuwezi kama Taifa kufananishwa na Syria, Haiti au Somalia kwamba sisi leo ndiyo tunaridhia mkataba huu. Kwa hiyo, mimi nafikiri kuchelewa kwetu kusiwe tatizo kwa sababu ya hapa tulipoanza; kwa sababu suala la kutengeneza *biological weapons* ni suala la biashara kubwa inayohusisha kampuni kubwa na *rogue countries*, na pesa nydingi zinapitia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara hii inafanana na ile biashara ya *narcotic* au *human trafficking*. Hizi pamoja na *biological weapons* ndizo biashara kubwa; na ndiyo maana utakuta mara nydingi ni siri kubwa; na wanasyansi wenu wanawenza wakatumiwa au wataalam wenu wanawenza wakatumiwa au kupitisha silaha au kutengeneza silaha na kama alivyosema *stockpiling*. Sasa hivi dunia ina silaha hizi kwa wingi sana; nchi kubwa duniani nchi zilizojitokeza katika maeneo haya zimeweka silaha hizi zikitaka kujikinga. Hata hivyo, pamoja na kuambiwa kwamba wazirudishe katika matumizi ya faida bado imekuwa ni ngumu kwa sababu kila mmoja anajiweka katika nafasi ya kutaka kujilinda kwa ajili ya likitokezea la kutokezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo sisi tushukuru kama taifa kwamba hadi hivi sasa pengine hatujaweza kutumika katika njia hiyo pamoja na kwamba pengine tungeweza kutumika kwa sababu ya kutokuwa katika eneo lile. Hivi karibuni tuliona namna ambavyo inaweza kuwa hatari, kule Marekani kulisambazwa silaha za kibaiolojia kupitia barua ambapo walipelekewa watu mbalimbali. Inasemekana wengi waliolengwa walikuwa ni wanachama wa *democratic* na inaaminika kwamba yule ambaye alisambaza zile barua ana-*belong* katika chama tofauti. Kwa hiyo ni vitu ambavyo vinaweza vikaenda mpaka *person to person*, mtu na mtu, si tu kwamba vinakwenda katika Taifa, lakini pia zinaweza zikaelekezwa kwa mtu na mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio makubwa yanayokumbukwa duniani mbali na yale yaliyotajwa na Kambi ya Upinzani mojawapo ni lile liliotokea kama miaka 20 nyuma sumu ya sarin ilipomwagwa katika kituo cha treni Japan. Jambo ambalo linatuzindua na sisi kwamba vitu kama hivyo vinawenza vikafanyika katika mikutano mikubwa ya watu kama kwenye viwanja vyta mpira, vituo vyta mabasi na vituo vyta treni. Kwa hiyo, ni suala ambalo huwezi kusema haliwezi kutokea lakini ni vizuri uwe tayari. Naamini kwamba kwa kuwa sasa tumekuwa washiriki hatutakosa mikutano, hatutakosa kufuatilia yale ambayo yametupita kama nchi *we will very fast learn*, nini wenzetu wamefanya na namna ya kujikinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetarajia pia kama walivyosema Kambi ya Upinzani sasa tuone *domestication of law*, tuone sheria inakuja ambayo itakazia Azimio hili itakayozuia vitu kama hivyo visitokee kwa kuweka vizingiti tokea hatua ya mwanzo. Pia kuzuia tusitumike kama *conduit* kama ambavyo inadaiwa tunatumika katika *conduit* yingine kwa mfano kwenye mihadarati inadaiwa kwamba Tanzania ni moja katika *conduit* hiyo, kwa hiyo, tusiweze kutumiwa. Tusifikiri kwamba kama nchi hatuwezi kutumiwa na watu wengine kwa sababu watu uovu wapo mionganoni mwetu kwa hivyo tunaweza kutumiwa kama nchi au kama mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Azimio hili linaelezea mambo makuu mengi sana lakini mojawapo ni sisi kuchukua hatua kwa watu ambao tunaweza kushirikiana nao au wanaweza kututumia kutoa ripoti. Hiyo *reporting system* ikiwa nzuri itaweza kutusaidia kwa sababu kama tutakuwa na wajibu wa kiuanachama ni lazima tuwe tunautumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, mimi nashukuru kwamba Azimio hili limekuja na naliunga mkono na natumaini Wabunge wengi kwa ujumla au sote kwa ujumla tutaliunga mkono kwa sababu lina maslahi makubwa na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Philip Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab na Mheshimiwa Said Kubenea ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwanza naomba nianze kuipongeza Serikali kwa kuonyesha jinsi gani sasa inachukua hatua katika utekelezaji wa masuala yake. Japokuwa Azimio limechelewa lakini sasa linatekelezwa, kwa hiyo, anayejisahihisha anastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri kwanza kwa kukubali maoni na ushauri ambao umetolewa na Kamati na ameweza kuingiza katika hili Azimio la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa takwimu katika uendeshaji wa nchi au taasisi kiujumla ni muhimu sana. Huwezi ukapanga bajeti bila kuwa na takwimu, huwezi ukapanga mpango wa maendeleo bila kuwa na takwimu na mambo mengine mbalimbali huwezi ukayatengeneza bila kuwa na takwimu. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali kwa kuleta hili Azimio na natumaini kama nchi tutakwenda kufaidika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, jambo la kwanza ambalo tutakwenda kufaidika na kama Mheshimiwa Waziri ambavyo ameeleza ni suala la masoko. Tunakwenda kwenye nchi ya viwanda kwa hiyo tunatengeneza viwanda ambavyo vitatengeneza bidhaa za aina mbalimbali sasa kwa kuwa na *charter* hii ya *statistics* ya Afrika tutaweza kuanza na soko letu lillilo ndani ya Afrika na kuuza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa suala la uwekezaji, kama nchi tutatoa takwimu zetu na tutaweza kuvutia wawekezaji walio kwenye maeneo mengine na sisi pia tutaweza kuangalia uwekezaji katika nchi nyingine. Kwa mfano, Benki ya CRDB imeweza kufungua matawi Rwanda

na sehemu zingine za Afrika, hiyo ilifanyika kutokana na takwimu. Kwa hiyo, hii itatusaidia pia kama nchi, taasisi na makampuni tuliyonayo katika nchi yetu kuwekeza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuingia katika Azimio hili, fursa yetu kama Tanzania nchi ambayo tumezungukwa na nchi takribani saba ambazo hazina bahari (*landlocked*) maana yake itatupa taarifa ambazo zitatuwezesha na sisi kuboresha kazi zetu za ndani kama vile upanuzi wa bandari na mambo mengine ili kuweza kutoa *service* kwenye nchi ambazo ni *landlocked*. Kwa hiyo, kwa kuwa na Azimio hili litatupa upana mzima wa kuweza kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia uwepo wa Azimio hili tunatakiwa tutunge sera, taratibu, sheria na tuwe na mipango. Kwa hiyo, natumaini sasa kama Serikali itakwenda kutekeleza mambo yote ambayo yanatakiwa yatengenezwe ambayo yataendelea kulisukuma hili Azimio katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Kamati ya Bajeti kuhusiana na kuongeza lugha ya Kiswahili katika masuala ya takwimu. Tukiangalia Tanzania tunatumia Kiwashili, Kenya wanatumia Kiswahili, Uganda kwa asilimia kubwa wanatumia Kiswahili, Rwanda wanatumia Kiswahili, Burundi, Congo, kuna Wamalawi wengi wanatumia Kiswahili na Wazambia. Kwa hiyo, kwa sababu lugha ya Kiswahili na yenyewe imekuwa na idadi kubwa ya watu wanaoitumia, tuombe katika kifungu kinachoruhusu mabadiliko basi Serikali ipeleke mabadiliko na najua kwamba ndani ya siku 30, Mwenyekiti wa hii anawasilisha katika nchi ambazo ni wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la takwimu litazidi kuimarisha Umoja wa Afrika kama zilivyo nchi za Ulaya. Nchi za Ulaya wana Umoja wao na wako *strong*. Tunatumaini na sisi tutakuwa imara na tutakuwa na takwimu ambazo

tunapeana habari mbalimbali za kimaendeleo na kuweza kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumziwa suala la Sheria ya Takwimu katika nchi yetu ya Tanzania kwamba inabania masuala mengine. Naomba tutambue kwamba takwimu zinasaidia katika kufanya maamuzi, katika kupanga mipango kwa hiyo haiwezekani mtu mwingine wa kawaida tu akatoa takwimu ambapo ye ye hayuko kwenye mamlaka husika. Kwa hiyo, lazima tuzingatia hilo na imeshatokea kwenye mitandao watu wanatoa takwimu za wao tu kujifikirisha, zinakuwa za *propaganda* na hazizingatii msingi inayotakiwa. Ukitoa takwimu ambazo siyo sahihi unaweza ukahatarisha hata amani ya nchi, unaweza ukasema wamekufa watu 1,000 kumbe wamekufa watu 10. Kwa hiyo, nipingane na wale wanaosema kwamba kufanya mabadiliko ya Sheria ya Takwimu siyo sahihi kama ambavyo Kambi Rasmii ya Upinzani imeweza kutueleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu sasa *National Bureau of Statistics* ikaboreshwe na iwezeshwe zaidi ili sasa Azimio hili liweze kutekelezwa ipasavyo kwa sababu ndiyo wenye wajibu mkubwa na wanaosimamia na kukusanya takwimu mbalimbali. Kwa hiyo, tuombe Serikali waende wakawezeshe maana wana upungufu wa wataalam na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi pia kuona kwamba kuingia kwenye hili Azimio tunakuwa na *technology transfer* maana yake tutapeana ujuzi kati ya hizi nchi wanachama ambao tumesaini haya maazimio. Kwa hiyo, itatujengea uwezo zaidi na wataalam wetu watakwendwa kuisaidia nchi yetu. Kwa sababu tunasema *information is power*, bila ya kuwa na *information* huwezi ukafanya maendeleo na huwezi ukafanya mambo mengine ya msingi katika maendeleo ya wananchi na kiuchumi kiujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono Azimio hili na naomba Wabunge wote tukubaliane. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab atafuatiwa na Mheshimiwa Said Kubenea na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba ajandidate.

**MHE. BALOZI. ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana ya Azimio la Mkataba wa Takwimu katika Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili ni muhimu sana na lilitakiwa lije mapema sana hata kabla hatujapitisha Mabadiliko ya Sheria ya Takwimu tuliyoyapitisha hapa Bungeni mwaka huu mwanzoni. Bila takwimu huwezi kuweka mipango yoyote ile, huwezi kupanga bajeti yoyote ile na huwezi kufanya maendeleo yoyote bila kuangalia ni kitu gani ambacho unacho kitakwimu na kitu gani ambacho unataka kukifanya. Kwa hiyo, takwimu ni kitu ambacho kinasaidia sana kuweza kujitathmini pia na kuweza kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo, ya kijamii na ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana Azimio hili kuletwa hasa kwa wakati huu kwa sababu kwanza umuhimu wake unaweza kusaidia sana kuratibu mambo ya takwimu katika Bara letu la Afrika na pia unaweza kusaidia sana kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu katika Bara la Afrika pamoja na wenzetu. Kwa hiyo, Azimio hili ni muhimu sana na limekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo hasa la Azimio hili ni kuhakikisha kwamba kweli takwimu ambazo zinapatikana ni sahihi na tunaweza kushirikiana na wenzetu kujua mambo mengi ya maendeleo. Kwa hiyo, Azimio hili linatoa ushawishi kwa mambo mengi na linasaidia sana kutengeneza sera (*policy*) za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia Azimio hili linataja mambo sita tu muhimu ambayo ni ya msingi sana. Mambo hayo ni haya yafuatayo:-

(i) Linataja mambo ya uhuru wa kitaaluma, kwamba ni lazima pawepo na uhuru kwenye kuandaa takwimu hizi na wataalam wetu lazima wawepo pale na ziandaliwe kitaaluma kabisa. (*Makofii*)

(ii) Linaangalia ubora wa takwimu zenyewe, kwamba takwimu zenyewe ni laizma ziwe sahihi.

(iii) Linaangalia pia mamlaka ambayo inatakiwa kutoa takwimu, mamlaka ambayo inatakiwa kutoa taarifa pamoja na rasilimali za takwimu hizo.

(iv) Linaangalia zaidi kwenye usambazaji wa takwimu wenyewe ukoje. Kwa hiyo, unaona umuhimu wake jinsi ulivyo.

(v) Linaangalia na kulinda taarifa ambazo anatoa yule mtu kama ni mtu binafsi au vyanzo vyovyote vya taarifa na watoa taarifa wote. Kwa hiyo, ile takwimu inakusanywa na inam-*protect* yule mtu ambaye anatoa ile taarifa.

(vi) Linaangalia utaratibu mzima wa ushirikiano kwamba tutashirikiana vipi katika Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana sisi tumefanya mabadiliko kwenye Sheria yetu mwaka huu 2018, Sheria ya mwaka 2015. Kwenye mabadiliko yale ambayo tulipitisha hapa Bungeni mambo yote haya ya msingi tumeyaonyesha. Kwa hiyo, utaona kwamba tumejaribu ku-*cover* mambo yote ambayo yanaonekana ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Azimio lote kwa ujumla wake utaona lengo ni kuhakikisha kwa kweli tunaleta ushirikiano. Kwa hiyo, kama lengo ni tunaleta ushirikiano kwenye Bara la Afrika basi tuhakikishe wanachama wote ambao wamesaini mkataba huu katika Bara la Afrika basi wanaridhia mkataba huu maana bila kuridhia itakuwa ni tatizo. Kwa sababu utaona kwamba nchi ambazo zimekwishardhia ni 22 na ambao wamesaini mkataba huu ni 32. Kwa hiyo, ni vizuri kwenye mikutano hiyo ya Afrika

kuhakikisha kwamba tunahamasisha ili na wenzetu wengine waweze kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nalionna ni huu upashanaji wa habari kwamba ni lazima tuwe na vyombo vyaa kisasa, ni lazima pawepo na *standard*, unaweza kukuta sisi tunavyo vyombo vizuri lakini unaweza kukuta nchi kama Burundi au *DRC* hawana au hawako kwenye matayarisho mazuri sasa watu kama wale utawafanyaje? Kwa hiyo, panatakiwa pawepo na vyombo ambavyo vinakuwa ni *standard* kwenye mikutano hiyo ya Bara la Afrika, viongozi wetu waangalie namna gani wanaweza kuweka vyombo hiyyo ambavyo vinaweza kusaidia kutoa habari kwa wepesi na kwa usahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utaona kwamba kwenye mikutano hii ya Afrika, Mawaziri wa Fedha waliwahi kukutana na kuazimia kwamba kila mwaka kwenye bajeti zao ni lazima watenge fungu ambalo ni 0.15 kusaidia mambo ya takwimu katika Bara la Afrika. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri wetu ahakikishe kwamba fungu hilo kweli linatolewa na linapangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza sana Taasisi yetu ya Kitaifa ya Takwimu ambayo tulipata fursa ya kuitembelea, kwa kweli wako vizuri. Kwa kweli wamejipanga, wana vyombo vizuri, wana jengo zuri na wana wataalam wazuri. Kwa hiyo, Azimio hili likipitishwa na Bunge hili tutakuwa mfano katika Bara la Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono sana Azimio hili, lilichelewa sana kuletwak lakini ni muhimu sana. Sisi kama Tanzania hatuwezi kubaki wenyewe ni lazima tushirikiane na nchi nyingine, tujitathmini na tujipime.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Said Kubenea atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Ntabaliba, kama muda utakuwa bado unaturuhusu atafuatia Mheshimiwa Silafi Jumbe Maufi.

**MHE. SAED A. KUBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeliona Azimio na nimesikia kauli ya Serikali ya kutaka Bunge hili Tukufu liridhie mkataba huo. Azimio ambalo Serikali imelileta Bungeni ukilisoma lenyewe na uksikiliza na ukiangalia matendo ya Serikali katika Bunge hili unaona kabisa wameleta kitu ambacho wenyewe hawakiamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Takwimu, kifungu cha 24(a) na (b) ambacho tullkipitisha katika Bunge hili Tukufu kinazuia mtu binafsi, chombo cha habari, taasisi au kampuni kufanya utafiti mbadala. Serikali inasema lengo kuu la zio hilo ni kukataa upotoshaji lakini ukweli ni kwamba takwimu zinapingwa kwa takwimu, huwezi kupinga takwimu kwa mambo ambayo yako nje ya takwimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina tatizo kubwa sana la takwimu zinazotolewa na Serikali yenyele na nitatoa mfano. Mwaka 2010 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza wapiga kura wa nchi hii walikuwa milioni 23 na zaidi. Baada ya vyama vya siasa, vyombo vya habari na wadau wengine kupinga takwimu za Tume ya Uchaguzi, aliyekuwa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, Bwana Rajabu Kiravu alitangaza wapiga waliokuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapigakura walikuwa watu milioni 21. Kwa hiyo, watu milioni 2 wameondolewa baada ya kelele kelele za watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, siku ya kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Lewis Makame alisema wapiga kura wote walikuwa watu milioni 19. Kwa hiyo, kulikuwa na milioni 23 ya kwanza, ikawepo milioni 21 ya pili na hatukuambiwa kwamba wale watu milioni 2 wengine

waliondokaje. Siku ya mwisho Jaji Lewis Makame wakati anamtangaza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa mshindi wa Urais wa mwaka 2010 alisema wapiga kura waliokuwemo kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura walikuwa milioni 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo kwa sheria hii akitokea mtu akafanya utafiti wake na watu walitumia takwimu za Tume ya Takwimu ya Taifa ambayo inasema karibu asilimia 60 ya Watanzania wote wako chini ya umri wa miaka 18. Sasa kama Watanzania wako milioni 45 na kama taarifa ya Tume ya Takwimu ya Taifa inasema waliopo chini ya miaka 18 wako karibu asilimia 60 maana yake huwezi kupata wapiga kura wanaozidi milioni 22. Hiyo ni kwamba umeandikisha watu wote nchi nzima hakuna matu ambaye hakuandikishwa. Sasa ni lazima ziwepo takwimu mbadala ambazo zitasaldia Serikali kupatikana kwa taarifa sahihi kuliko taarifa za kupikapika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Takwimu Mheshimiwa Adadi ameuelezea vizuri tu huo mkataba, anasema mkataba unaelezea uhuru wa kitaaluma. Sasa chombo cha habari na hapa nitoe mfano wa *TBC* iliyahi kutangaza kwa kutumia Takwimu za Tume ya Takwimu kwamba asilimia 4 nadhani kuna uhaba wa chakula na asilimia 4 ya watu wamepata tatizo la chakula lakini taarifa ilikuwa ni asilimia 5. Sasa ile kukosea tu taarifa ya takwimu *TBC* ilikuwa inaingia kwenye matatizo. Hawa watu ni binadamu, Katiba yetu lbara ya 18 inatoa uhuru kwa kila mtu kupata habari na kutoa habari. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma vizuri sheria mbalimbali kuna adhabu zinatolewa kwa vyombo vya habari vilivyokosea takwimu watu wanafungwa, wanapigwa faini na hiyo ipo katika kifungu cha 37(4) na (5) cha Sheria ya Adhabu kwa vyombo vya habari. Nafikiri kuridhia mkataba ni jambo jema sana lakini ni lazima wakati tunataka kuridhia mikataba na sisi kama Bunge tujiridhishe sheria tunazotunga kweli zinakidhi matakwa ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma kwenye mtandao mmoja wa kijamii, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango alikuwa ananukuliwa akisema kwamba Serikali imelegeza masharti ya utoaji wa takwimu baada ya mazungumzo na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa /IMF. Hii inaonyesha kwamba sheria zetu tunatungiwa na watu wa nje hatutungi kwa maslahi yetu. Kama maneno hayo Mheshimiwa Dkt. Mpango aliyasema na hii ilikuwa Oktoba, 2018 na sheria tumebadilisha Agosti leo tumenyimwa fedha au tuko hatarini kunyimwa fedha na wafadhili kwa kupitisha Sheria chafu ya Takwimu, tunakwenda wapi? Hawa watu walikuja kwenye Kamati ya Katiba na Sheria tulisuguana kweli lakini *finally* wanasema tuna maelekezo kutoka juu lazima hii sheria ipite. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hill ni chombo cha wananchi na kwa mujibu wa Katiba Bunge ndiyo chombo kikuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitakachowakilisha wananchi. Serikali inapoleta sheria Bungeni, mikataba hii ni vizuri tukaridhia kwa sababu sisi siyo kisiwa ni lazima twende na dunia inavyokwenda na tutawalaumu sana kama tutakuwa tunapitisha sheria tunakwenda kwenye mikataba inafungwa halafu sisi haturidhii hiyo mikataba lakini ni muhimu sheria zetu zilinde uhuru na Taifa letu. Mwalimu Nyerere alipokwenda kuomba uhuru wa Tanganyika alitaka tuwe huru siyo tu uhuru wa bendera, uhuru wa mawazo na uhuru wa kuamua mambo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa tunataka uhuru wa bendera tungechukua bendera ya Tanganyika tungekuwa tunapepe bado tungetawaliwa na Gavana lakini tulitaka uhuru. Mwalimu alisema ni lazima tulinde utu wetu, ni lazima tulinde Taifa letu na Taifa letu haliwezi kulindwa kama watu wachache wanatengeneza sheria ambayo inaenda kuumiza watu wengi. Hiyo ni sawasawa na Serikali ya Makaburu ambayo ilikuwa inatunga sheria za kikaburu kukandamiza wazalendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu na Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango nafikiri anaelewa umuhimu wa kutoa takwimu kwa haraka na kwa wakati. Benki Kuu ikichelewa kutoa takwimu lazima tutatafuta takwimu mbadala tutaoa kesi tutaendelea nazo baadaye. Hiyo ikitokea watu wakikamatwa kwa kutoa takwimu Taifa linaharibika, linachafuka katika uso wa dunia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umeisha, kengele mbili zimegonga.

**MHE. SAED A. KUBENEÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Azimio la Takwimu Afrika uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu nimpe taarifa Mheshimiwa Kubenea pale huu ni mkataba wa takwimu ambao una malengo yafuatayo: unashughulikia mambo ya uchumi; kijamii; na mazingira. Hayo mambo ya uchaguzi haukuwa unahusika nazo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Waziri wa Fedha na Serikali kwa kuridhia mkataba huu lakini nipongeze Kamati ya Bajeti kwa kuuchambua mkataba huu. Tumeelezwa sababu mbili kwa nini mkataba huu umekuja. Kwanza mwaka 1991 Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika ulisainiwa na Tanzania tuliridhia tarehe 10 Januari, 1992. Sababu ya pili ya kuja kwa mkataba huu ni kwamba Sheria Kuanzisha Umoja wa Afrika ambayo ilisainiwa mwaka 2000 na tuliridhia tarehe 6 Aprili, 2001. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye sasa kwa kuwa tumeridhia hizo mbili watu wa takwimu wakasema ni vizuri tuwe na takwimu za Afrika ambazo zitawenza kuleta ulinganifu wa nchi mbalimbali kwa mambo ya kiuchumi na kijamii. Afrika nzima inayo malengo ya mpaka 2063 uchumi wake uwe umekua, himilivu na umetengamaa. Kwa hiyo, tunalo lengo la Afrika mwaka 2063 tuwe tumefikia hatua fulani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Ofisi za Takwimu sasa zikaona ni lazima kuwe na takwimu ambazo ni linganifu. Nipongeze Ofisi yetu ya Takwimu ya Tanzania walirekebisha Sheria yao ya mwaka 2015 tuliyopitisha mwaka 2018 imeingiza haya mambo yote ambayo yako kwenye mkataba huu. Kwa hiyo, sisi tuko mbele sheria imesha-*take on board* mambo haya, naipongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa wale ambaao hamkuupitia sana mkataba huu, kwa upande wa uchumi tunataka *data* zifuatazo: pato la Taifa, mfumuko wa bei, uzalishaji sekta ya kilimo, madini, viwanda, umeme, ujenzi, huduma na mawasiliano. Tunataka kujua mapato na matumizi ya nchi mbalimbali, ujazi wa fedha katika nchi mbalimbali na bei za nchi tofauti, hizi ndiyo takwimu kubwa ambazo Ofisi ya Takwimu inabidi itupatie. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upande wa jamii tunataka kujua idadi ya watu, Tanzania ina watu wangapi, Congo ina watu wangapi, Burundi ina watu wangapi, inatakiwa *data* zile ziwe *harmonized*, ziwe za Kiafrika zisiwe za kinchi. Pia tunataka tujue elimu, mambo ya afya, utawala na mambo ya mazingira. Kwa hiyo, ni jambo kubwa sana hauwezi ukali-*narrow* ukaanza kujadili uchaguzi kwamba watu fulani walienda kupiga kura, ni jambo kubwa linamzidi kiwango cha kulielewa vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili linataka kwanza wanasiasa wawe mbali na chombo hiki na sasa hivi Ofisi yetu ya Takwimu imeanza kuwa na *autonomy* ambalo ni jambo jema tunaanza kutekeleza sasa Azimio hili. Taarifa ambazo wanazikusanya kwa ajili ya usiri hazitatumika Mahakama

yoyote. Kwa hiyo, watakachokuwa wanakitoa ni cha siri lakini hauwezi kuzitumia takwimu zile kwenda Mahakamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha na nchi ya Tanzania tunatakiwa tufanye nini? Kwanza, Ofisi yetu ya Takwimu inabidi tuiongezee rasilimali fedha kwa sababu tunaingia kwenye mkataba ambapo lazima twende na wakati na *time table* ya kukusanya *data*. Kwa hiyo, lazima wapate fedha za kutosha kwenye bajeti ya 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunahitaji rasilimali watu, watu ni wachache, ofisi ile ni kubwa, haya mambo ni makubwa kwa sababu tumengia kushindana na nchi za Afrika. Tumewekewa kiwango cha kuweza kutenga bajeti, ni mategemeo yetu kwamba 2019/2020 Mheshimiwa Waziri atakuwa ametenga fedha za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda tu kuipongeza Kamati ya Bajeti na Wizara wametupa ushirikiano mzuri tumeuchambua vizuri. Kwa hiyo, naunga mkono Azimio hili la Takwimu. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi kama muda utakuwa bado unaturuhusu Mheshimiwa Salum Rehani ajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia Maazimio haya. Nataka kuchangia kwenye Azimio la Silaha za Maangamizi hasa hizi za kibaiolojia ambapo tunatakiwa turidhie Azimio hili kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania si kisiwa na kwa mujibu wa taarifa ambazo tumezipata hapa kutoka kwa

Waziri, Kamati pamoja na Kambi ya Upinzani, sote tumeeleza haja na takwa vilevile la kutaka kuridhia Azimio hili. Kwa nini tunaridhia? Tunaridhia kwa sababu kwanza limesainiwa muda mrefu lakini halijaridhiwa. Pili, tunaridhia ili nasi sasa tuweze kuungana na nchi zaidi ya 180 ambazo tayari zimesharidhia na zinafaidika na yale yanayotokea kwa kuweza kujikinga na silaha hizi za maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia sasa hivi imekumbwa na tataruki mbalimbali na moja ya tataruki ni magaidi kuweza kutumia nafasi za kushambulia maeneo mbalimbali ya nchi kwa maslahi yao. Sayansi vilevile nayo imegeuka moja ya silaha kubwa ambayo inatumiwa na watu mbalimbali duniani. Kwa mfano, tukiangalia watu wanaweza kuona maji ni kwa ajili kunywa na kusafiria lakini kigaidi maji ni sehemu moja ambayo inaweza kutumika kuweza kuangamiza watu wengi duniani na kundi kubwa la vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo taarifa zinasema kwamba Israeli na Misri hawajardhia mkataba, kila mmoja anamtegea mwenziwe kusaini na kuridhia mkataba huu. Kuna tishio kubwa la Mto Nile ambapo kuna *belt* ya *Suez Canal* ambayo kwa Misri ndiyo uchumi wake ulipokuwepo, roho ya uchumi wake uko kwenye *Suez Canal Belt*, wana uzalishaji mkubwa sana. Eneo lile la mto peke yake wana zaidi ya uzalishaji wa pamba zaidi ya tani 600,000 lakini kuna vyakula mbalimbali wanazalisha zaidi ya tani 700,0000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo watu wengi wanaweza kutumia kigaidi ni eneo la Mto Nile kwa kuweza kutia pale *bacteria* au *virus* ambao wanaweza kwenda moja kwa moja kwenye mazao ya wale wananchi na kuweza kuleta athari. Si hivyo tu hata maradhi haya ya surua na mengineyo yalipandikizwa na kutengenezwa na yakatumwa kuititia maji yale na watu wakapata athari katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuititia sayansi silaha hizi za kibaiolojia ni kitu kinachotengenezwa kwenye

maabara na kinaletwa katika maeneo yetu haya ili kilete athari za kiuchumi, kibashara lakini hata za kitamaduni. Kwa hiyo, niwatake Wabunge tukubali turidhie ili yale manufaa ambayo athari zikitokea tutaweza kupata msaada kwa mashirika ya kimataifa ambayo yanashughulika na jambo hili. Vinginevyo, hatari kubwa ambayo inaweza kutukumba litakapotokea hatuna wa kumlilia litakuwa ni letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu, taarifa nyiningine zinasema kwamba hata ugonjwa wa ebola ni ugonjwa ambaao umepandikizwa. Ebola ni *virus* na hakuna dawa na tiba ni moja kati ya *biological weapon* ambayo inaweza kutumika kuathiri nchi yetu hii hapa. Ugonjwa huu utakapoingia sisi kama Tanzania uwezo wetu wa kukabiliana na maradhi magumu kama yale ni mdogo. Tutakapoweza kuridhia Azimio hili jamii ya kimataifa tunawakabidhi na wao waweze kullangalia kwa mtazamo chanya kuliko kusema kwamba sisi tunajiacha peke yetu na tukasema kwamba tutaweza kukabiliana wakati uchumi wetu hauwezi kukabiliana na changamoto za maradhi mbalimbali yalikuwepo hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo, tu wataalam mbalimbali na taarifa nyiningine zinasema hata UKIMWI ni kitu kilichotengenezwa Marekani. Kuna maradhi mengi tu ambayo yanakuja katika maeneo yetu kwa njia hii na wanyama ni sehemu moja ambayo watu wanatumia kuingiza *bacteria*, virusi na fangasi lakini kama nchi vipi tunaweza kujilinda na tunaweza kuwa na sheria ambazo zitaweza kusimamia masuala haya. Nimesikiliza vizuri hotuba ya Kambi ya Upinzani imeeleza baada ya kuridhia tusimamie sheria zitakazoweza kudhibiti uingiaji wa madhara ya silaha za kibaiolojia hapa nchini. Kwa sababu kuridhia ni jambo moja lakini sheria za kudhibiti lazima ziwepo ili nchi hii tuweze kuiweka salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wito wangu ni kwamba tuwe na mipango thabiti ya kuhakikisha kwamba kila kwenye uwezekano wa hasa zile *quarantine point* zetu tulizokuwa nazo *airport*, bandari na maeneo mengine ya

mipaka kuwe na watu wenye taaluma ya kuweza kugundua aidha hizi *chemical* au *biological weapons* zozote zile ambazo zinaweza kuja ndani ya nchi yetu. Tumeona na historia inajieleza barua pepe mbalimbali ambazo zinatumika katika maeneo yetu haya watu wanaletewa lakini wengine wanatumia mpaka vitabu vya dini kuingiza *bacteria*, *virus*, na vitu mbalimbali na kuletwa kama zawadi lakini matokeo yake zinatumika katika njia tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Wabunge hawa waridhie lakini Serikali iweze kuweka sheria ambazo zitawenza kudhibiti madhara hayo na kufanya Tanzania iwe nchi salama na inaweza kufanya shuhguli zake bila kupata athari nyingine zozote. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi. Nitaleta kwenu majina ya wachangiaji ambaao wataanza mchana, Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mheshimiwa Augustino Mayanda Masele na Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

Waheshimiwa Wabunge, pia niwakumbushe tumeletewa Orodha ya Nyongeza ya Shughuli za leo, kwa hivyo hili zoezi nalo tutafanya tutakapokutana. Pia ninayo majina kutoka vyama vyetu kulingana na Kanuni zetu ya wachangiaji wa Azimio hilo lingine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tutaendelea na uchangiaji kwa Wabunge ambaao nilikuwa nimekwishakuwataja, tutaanza nao hao, lakini kabla ya hapo kuna tangazo la mgeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye Jukwaa la Spika, yupo mgeni wa Mheshimiwa Spika, naye ni Mheshimiwa Abdullah Hasnuu Makame, ambaye ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Karibu sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia  
Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia  
na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake wa Mwaka 1972  
(*The Convention on Prohibition of Development, Production  
and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin  
Weapons and their Destruction*) of 1972**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa  
Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*)**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Ruth Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele na Mheshimiwa Jasson Rweikiza ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mezani inayohusu huu Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja naungana na maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa sababu mimi ni mmoja wa wanakamati na naunga mkono maelezo yaliyotolewa na Kamati. Vilevile naunga mkono maoni ambayo yametolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kama nchi nyingine duniani zimesaini na kuridhia mikataba mbalimbali. Baadhi ya mikataba ni ile inayolinda haki za binadamu, utawala bora, demokrasia na mazingira. Ni imani ya Kambi ya Upinzani kwamba Serikali itaheshimu mikataba hiyo na kurekebisha kasoro ambazo zimeanza kujitokeza sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi silaha za maangamizi zimeanza muda mrefu na tunajua kwamba nchi kubwa duniani, zenyе nguvu, ndizo hasa zimetengeneza hizi silaha za maangamizi. Tumeona athari zake zilizotokea kati ya Japan na Marekani kule Nagasaki na Hiroshima ambapo kumetokea madhara makubwa sana. Mpaka leo bado watu wanazaliwa wakiwa vilema kwa sababu ile mionzi ya *nuclear* *ime-distort* zile *DNA* na *genome* za binadamu. Matokeo yake mpaka leo bado watu wanazaliwa vilema, ardhi imeharibika na haifai kabisa hata kwa kilimo. Kwa hiyo, hizi silaha za maangamizi na hivi virusi ni hatari sana kwa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona villevile hata Marekani kule walivyokuwa wanagawa *the anthrax* kwenye bahasha na kutumia watu mbalimbali na madhara yametokea. Tumeona walivyochanganya vitu wakapelekewa Wachina ikaleta tauni. Kwa hiyo, hizi silaha ni mbaya sana kwa binadamu, wanyama na mazingira na ni maangamizi yetu wenyewe sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dhana pia na inaaminika kwamba hata magonjwa haya ya milipuko, Ebola, UKIMWI na maradhi mengine kwamba yanatengenezwa kibailojia. Kama yanatengenezwa kibailojia inaaminika pia kwamba ni kwa faida ya makampuni makubwa ya madawa ya kimataifa ili

watengeneze *billions of money* kama faida kwa kutengeneza dawa za kupambana na magonjwa hayo. Hiyo ni dhana ambayo inazunguka na sijui kama imeshakuwa *proven* kama ni *right*, lakini ni kitu ambacho kinasemwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, kwa sasa kuuridhia mkataba huu ni muda muafaka. Kwa sababu kabla ya hapo ilikuwa Serikali ndiyo ilikuwa inahodhi hivi virusi, ndiyo ilikuwa inatengeneza, lakini sasa kwa jinsi mabadiliko yanavyoendelea kutokea kumetokea vikundi vingine vya kigaidi ambavyo vikishika hizi silaha na *weapons of mass destruction* wataweza kuleta athari kubwa sana katika dunia na kuangamiza dunia, siyo dunia tu na viumbe vyote vilivyo hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa minajili hiyo sasa nakubaliana na Serikali yetu kuridhia mkataba huu kusudi nchi zote ambazo zina hizo silaha kwanza ziziteketeze, kama watateketeza na vilevile zitumike kwa ajili ya usalama wa binadamu na wananchi wote. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba ili na sisi tuwe katika hili *group* kubwa la kimataifa kwa sababu hatuwezi kuwa tofauti na wengine, tunairidhia leo kusudi tujumuike katika jumuiya ya kimataifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kuungana na jumuiya ya kimataifa endapo jambo kama hili litaweza kutokea nchini basi tutaweza kupata msaada wa mara moja kwa ajili ya *ku-mitigate* madhara ambayo yanaweza kutokea na tunaweza tukapata wataalam wa kuweza kusaidia. Kwa hiyo, ni muhimu sisi tukaridhia itifaki hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa angalizo tu kwa Serikali kama wengine ambavyo wameshachangia, Kamati yetu ilichangia na hata katika Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba tunasaini mikataba lakini tunachukua muda sana kuridhia na Serikali inachukua muda sana kutengeneza zile sheria na kanuni za kutekeleza mikataba hiyo. Kwa hiyo, ushauri tunaoutoa sisi Kambi ya Upinzani ni Serikali kuhakikisha kwamba hii mikataba yote ambayo tunaridhia na ambayo tumeshasaini basi sheria na kanuni na

taratibu zinazotakiwa kutekeleza mikataba hii ziweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuweza kuchangia mada hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kusudi niweze kuchangia Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibailojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological and Toxin Weapons and their Disruption*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu ni moja ya mataifa ambayo yanapenda amani, hata hivyo pamoja na kupenda kwetu amani tumejikuta tunapitia kwenye majaribu mbalimbali, ikliwemo vita vya Kagera na vilevile Ubalozi wa Marekani nchini mwetu ulivamiwa na kushambuliwa na magaidi ambao walishambulia nchi yetu pamoja na Kenya. Kwa maana hiyo, nchi yetu iko hatarini kuweza pia kushambuliwa kupitia silaha hizi za maangamizi zinazohusiana na mambo ya sumu, vimelea, bakteria, pamoja na *fungus*, kama ambavyo Waziri alivyojaribu kutufahamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tulipitishwa katika mkataba huu tukaambiwa kwamba ni mkataba uliopitiwa na mataifa mbalimbali chini ya Umoja wa Mataifa mwaka 1972 na sisi tukasaini lakini hatukuweza kuuridhia. Nalishauri Bunge langu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liweze kuridhia mkataba huu kutokana na sababu ambazo nyingi zimeelezwa na kwamba, sisi kama jamii mojawapo ya mataifa ya ulimwengu huu tunayo sababu ya kuchangia na

sisi katika kuhakikisha kwamba dunia yetu inakuwa ni sehemu salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulimwengu huu ni ulimwengu ambao umegeuka kuwa kama kijiji na kwa maana hiyo, maingiliano mbalimbali ambayo yanatuweka pamoja yanatutia katika uwezekano wa kupata madhara kutokana na silaha mbalimbali ambazo mkataba huu unazuia uzalishaji wake na ulimbikizaji wake. Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja ya Azimio hili kuridhiwa na nchi yangu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo katika wakati muafaka baada ya kuwa mataifa zaidi ya 182 yameridhia mkataba huu na kwa maana hiyo, hata sisi hatuwezi kujitenganao. Kwa maana hiyo tunapaswa tu, kama Taifa la wapenda amani tuunge mkono Azimio hili kwa asilimia zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jasson Rweikiza halafu tutaanza kuwaita Mawaziri kwa ajili ya kuhitimisha hoja zao.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili nichangie kwenye mkataba huu wa silaha za sumu na silaha za kibailojia. Naunga mkono kwamba sasa ni wakati muafaka mkataba huu umeletwa tuupitishe hapa Bungeni na tuwe sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa katika kuungana na wenzetu kupambana na silaha hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza niipongeze Serikali kwa kuleta mkataba huu hapa, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwinyi na wasaidizi wake wote, Katibu Mkuu na wataalam wengine. Kwa kweli tumechelewa sana kuuleta kwa sababu ambazo hazieleweki. Kama tuliweka saini mwaka 1972 na leo ni miaka 46 karibia 50 hatujaupitisha kwa kweli tumechelewa sana. Baada ya

mwaka 1972 nchi karibia zote duniani hata wale ambao hawakusaini wameupitisha. Tanzania ni moja ya nchi karibu 10 dunia nzima ambao bado hatujapitisha mkataba huu, tumebacki nyuma sana kwa kweli sio jambo sahihi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu ni wa kuzuia silaha za maangamizi, silaha za sumu na za kibailojia ambazo madhara yake ni makubwa. Hakuna asiyefahamu madhara ya silaha kama hizi. Akitokea mhalifu mmoja akazalisha vile virusi vya magonjwa kama ndui au *anthrax* au vya kuondoa hewa ya *oxygen* duniani halafu tukafa wote dunia nzima ni jambo ambalo tutakuwa tumelifanya kwa uzembe na uzembe huu ni kutokujunga na mkataba huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri tujiunge ili tuwe sehemu ya dunia kupambana na silaha hizi, silaha hizi ni hatari na kutoridhia vilevile ni hatari. Kutoridhia ni hatari kabisa na unabaki nje ya wenzako ambao wanashirikiana kupambana nazo, unakuwa umejitenganao. Kwa maana nyingine ni kwamba wewe unaunga mkono silaha hizi ziwepo, ndiyo maana ya kutojiunga, unaunga mkono ziwepo na unakuwa ni sehemu ya tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zimesemwa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, Kamati na Wabunge wamezisema, sina haja ya kurudia. Moja ambayo haikusemwa ni kwamba tusipojiunga na mkataba huu na tukashambuliwa na adui na silaha hizi hatuwezi kuomba msaada kokote. Hatuwezi kwenda Umoja wa Mataifa, Uingereza, Ulaya, Marekani au popote pale kuomba msaada kwa sababu sio wenzetu tutakuwa sisi tuko nje, tutakufa na hali hiyo tutapambana nayo sisi wenywewe. Kwa hiyo, ni vizuri tuweze kijiungu na mkataba huu haraka iwezekanavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ilijiunga na mkataba mwengine unaofanana na huu wa *Chemical Weapons*, huu ni wa *Biological Weapons*, inakaribiana sana. Kama tulijiunga na Mkataba ule wa *Chemical Weapons* kwa

nini tusijunge na mkataba huu ambao uko karibu sana wa *Biological Weapons? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aibu nyingine ni kwamba zimebaki nchi kama tano tu dunia nzima au kumi ambazo hazijajiunga. Nchi hizo ni Tanzania, Egypt, Somalia, Israel, Syria na nyingine chache. Ukiangalia hizi nchi kama Egypt wana matatizo yao na Israel, wanategesheana nani ajiunge kwanza. Somalia hawakuwa na Serikali muda mrefu sana, walikuwa wanapambana wao kwa wao, wanapigana vita kwa muda mrefu sana ndiyo maana hawakujunga. Syria mpaka leo iko kwenye vita, sisi Tanzania tuna sababu gani ya kutojiunga? Tujunge haraka iwezekanavyo tuwe sehemu ya dunia katika kupambana na silaha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia majirani wote wanaotuzunguka Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda, *DRC*, Zambia, Malawi, Msumbiji, Madagascar kote wamejiunga, bado sisi peke yetu. Kwa kweli, siyo sahihi kuendelea kubaki nje ya utaratibu huu, ni vizuri tukajiunga na mkataba huu haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatari ya kushambuliwa ipo, ukisoma kwenye mitandao na kwenye makala nyingine za kimataifa inasemekana kwamba hawa Alshabaab wakiungana na Boko Haram wanajaribu kutafuta silaha hizi na wanajenga ngome zao kwenye nchi zetu hizi Kenya, Tanzania, Msumbiji ili wazitumie kwa maangamizi ya watu wengi sana. Kwa hiyo, ni vizuri tukajiunga tuwe salama, tuwe na wenzetu tuweze kupambana nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa sababu wote kabisa wameshauri kwamba mkataba huu uridhiwe. Hili ni jambo muhimu sana kwa sababu wakati muafaka umefika wa kufanya hivyo, kwa saabu ya tishio lililopo la silaha hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maoni ya Kamati. Kamati imeungamkono kuridhiwa kwa Azimio hili. Tunashukuru sana kwa kutuunga mkono, lakini wana mapendekezo ambayo wameyatoa. Mapendekezo yao ni kwamba Serikali itumie vizuri fursa ya kuendeleza kitaaluma na kuboresha taasisi zitakazosimamia shughuli mbalimbali za utafiti na uchunguzi na udhibiti wa bidhaa za kibailojia na sumu. Bila shaka hilo litafanyika, tunapokea ushauri huu na baada tu ya kuridhla basi tutaangalia yale maeneo yote ambayo tulisema kwamba yatakuwa faida kwa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taasisi za Umoja wa Mataifa ambazo ziko tayari kutujengea uwezo katika maeneo mbalimbali ya kuweza kushughulika na vimelea hivi hatari kwa njia salama. Kwa hivyo, wameshaonesha utayari wao wa kutusaidia na sisi baada ya kuridhia tutatumia fursa hiyo ili tuweze kunufaika na kuridhia kwa mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani, tunawashukuru pia kwa kuunga mkono kuridhia Mkataba huu au Azimio hili. Vilevile wametoa ushauri kwamba Serikali ihakikishe in andaa na kuboresha mifumo yake ya kiulinzi ya kubaini madhara ya silaha za kibiolojia na sumu yaani *detection systems* ili kuweza kukabiliana na janga hili endapo litatoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikubaliane naye Mheshimiwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba ni muhimu kama Serikali tuandae utaratibu mzuri wa kubaini madhara ya vimelea hivi endapo yatatoka. Hizo *detection system* anazozzungumzia nadhani baada ya kuridhia na

kutunga sheria, basi itakuwa moja ya jukumu la taasisi ambalo litapewa mamlaka ya kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wametushauri kwamba itungwe sheria yaani Azimio hili baada ya kuridhiwa liwe *domesticated* katika sheria zetu za ndani. Hilo tunaunga mkono na ndivyo itakavyofanyika. Kama tunavyotambua kwamba kuna sheria nyingi zinasimamia maeneo haya ni vizuri zikaangaliwa kwa umoja wake ili kuona ni jinsi gani ya kuja na sheria nyingine au kuboresha zilizokuwepo. Kwa sababu ziko Taasisi kwa mfano *National Institute of Medical Research (NMR)* inafanya utafiti unaotumia vimelea kama hivi. Kwa hiyo, taasisi hizo na taasisi zinazofanya utafiti katika mimea na kadhalika, pamoja na wale wanaoshughulika na masuala ya *Atomic Energy* kwa pamoja zitazamwe sheria zile na kuona njia nzuri zaidi ya ku-*domesticate* Azimio hili baada ya kuridhiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko eneo ambalo Kambi ya Upinzani wanatoa angalizo, kwamba moja ya faida za kuridhia, nanukuu walivyosema: "Sehemu ya uhamasishaji wa matumizi sahihi na salama ya silaha za kibaiolojia na sumu. Aidha nchi yetu inaweza kubadilishana vifaa tekinolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji silaha za kibaiolojia na sumu kwa minajili ya kiusalama".

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hapa kuna tatizo la kutafsiri tu ile Ibara ya 4, haizungumzii kabisa katika kutumia silaha hizi kiusalama, inazungumzia kuondokana nazo, kwa zile nchi ambazo wanazo wazibadilishe matumizi au waziharibu, ziwe na matumizi salama, sio tena kutumia kama silaha. Kwa hiyo, hapa kuna tatizo la tafsiri na naomba tu ninukuu Ibara ya 4 inavyosema kwamba: "pamoja na mambo mengine inataka nchi mwanachama wa mkataba kulingana na utaratibu wa Katiba ya nchi yake kuchukua hatua muhimu kuzuia na kukataza uwendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji, umiliki na utunzaji wa viambato sumu, vifaa na njia za usafirishaji wa vitu hivyo ndani ya mipaka yake na maeneo inayoyadhibiti".

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonyesha wazi kabisa kwamba hizi hakuna njia ya kutumia silaha hizi kwa usalama. Kinachotakiwa ni kuziharibu au kubadilisha kabisa matumizi yake zitumike kwa matumizi ambayo ni salama kama ilivyoonyeshwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ally Saleh, yeye amesikitika kwamba mkataba huu umechukua miaka 46 kuridhiwa, imetuweka nyuma sana hususani kwa kuwa hauna gharama yoyote. Tunakubaliana na Mheshimiwa Ally Saleh kwamba mkataba huu umechelewa kuridhiwa lakini ni kwa nia njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mkataba huu kusainiwa, hili tishio ambalo tunaliona sasa hivi halikuwepo, kwa maana hiyo hakukuwa na uharaka huo. Wakati huo huo illikuwa ni vyema kuangalia dunia inavyokwenda. Sasa hivi tunaona kuna kila sababu ya kuridhia kwa sababu silaha hizi zimeshaondoka mikononi mwa mataifa (*state actors*) kwenda *non-state actors*. Kwa maana hiyo kuna hatari ya kutumiwa na magaidi na hili limeshawahi kufanyika maeneo kadhaa, kwa hiyo, nadhani sasa ni wakati muafaka na tukiliridhia basi tutakuwa na sisi ni nchi ya 183 kufanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema tusifananishwe na nchi za Syria, Somalia, Haiti kwa kuchelewa. Ndiyo maana tumelileta Azimio hili ili tuondokane na kufananishwa ni nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile alikuwa anasema kwamba hizi silaha za kibailoloja ni biashara kubwa, nchi kubwa bado wanazo na hawajabadilisha matumizi yake kuwa salama. Hili hatuna uhakika nalo lakini kwa sababu ukisharidhia mkataba huu na ukithibitisha kwamba kuna nchi ambayo imeridhia lakini haitekelezi haya yaliyomo katika mkataba una kila sababu ya kuipeleka nchi hiyo kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ili hatua stahiki zichukuliwe. Kwa hiyo, kama ukipatikana uthibitisho wa hayo basi bila shaka nchi wanachama zitafanya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ameomba sheria itungwe baada ya kuridhia. Kama nilivyosema tutatafuta njia nzuri ya ku-*domesticate* Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Salum Rehani ye ye alisema kwamba turidhie ili tupate msaada endapo tutapata athari za silaha hizi. Nakubaliana naye kabisa kwamba uwezo wetu wa kukabiliana na matishio ya silaha hizi ni mdogo. Kwa maana hiyo tukiwa moja ya nchi zilizoridhia tutapata msaada wa kujenga uwezo wetu wa kukabiliana na matatizo haya na bila shaka tutaweza kuwa na utayari zaidi endapo tatizo hilo litatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini vilevile alisema kwamba katika maeneo ya viwanja vyta ndege, bandari na mipakani kuwe na wataalam wa kubaini silaha hizi. Bila shaka hilo ni muhimu na litafanyiwa kazi. Vilevile alishauri sheria za kusimamia zitungwe, nakubaliana naye kwamba upo umuhimu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ruth Mollel ye ye alisema kuridhia mkataba huu kwa sasa ni muafaka kutokana na kuwa mikononi mwa watu amba wanaweza kuzitumia vibaya. Tunakubaliana naye mia kwa mia, hilo lipa na ndiyo maana tumeuleta turidhie ili tuweze kukabiliana na hao watu kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mkataba utasaidia nchi zote walioridhia kuteketeza silaha hizo au kutumia kwa matumizi salama. Ndivyo mkataba unavyosema kwamba mara baada ya kuridhia kama unazo, aidha, uziteketeze au utumie kwa matumizi salama ambayo yatathibitishwa na nchi wanachama kuhakikisha kwamba unachosema ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iungane na Jumuia ya Kimataifa ili ipate msaada endapo tatizo hili litatokea kwetu. Tunakubaliana nae mia kwa mia na ndiyo sababu kubwa inayotupelekeea kuridhia mkataba huu ili tuweze kusaidiwa endapo tatizo hili litatukuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ametoa ushauri kwa Serikali kutunga sheria na kanuni kwa mikataba yote iliyosainiwa na kuridhiwa. Hatuna pingamizi na hilo, kila baada ya kuridhia mikataba tutaangalia utaratibu bora zaidi wa kutunga sheria ili ku-*domesticate*, aidha, maazimio ama mikataba hii, ndiyo itaweza kufanya kazi sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Augustino Masele, ye ye amesema Tanzania iunge mkono Azimio hili ili tujumuike na nchi nyingine 182 kupambana na silaha hizi. Nakubaliana naye mia kwa mia na ndiyo azma kwa kweli ya Serikali yetu kwamba tunalileta Azimio hili ili tuondokane kuwa kat i ya zile nchi chache zinazotajwa kwamba hazijaridhia na pengine wao wana sababu ya kutofanya hivyo, kwa kweli kama Tanzania hatuna sababu hiyo na ni vizuri sasa tuondoke kuwa katika kundi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rweikiza, ye ye ametoa pongezi kwa Serikali kuleta mkataba huu kwa ajili ya kuridhiwa pamoja na kuchelewa, tunakiri na tunashukuru kwa pongezi hizo. Pia amesema kwamba Tanzania iwe sehemu ya dunia katika kukabiliana na silaha hizi, kutoridhiwa ni kuunga mkono ziwepo silaha hizo. Nakubaliana naye mia kwa mia, kwamba kwa wakati tuliokuwa nao, usiporidhia basi una sababu. Ndiyo maana kuna baadhi ya nchi zimetajwa hapa kwamba hazijaridhia kwa sababu zinategieana, huyu akiridhia mwingine hajaridhia anaweza akazitumia dhidi yake. Sisi hatuna sababu hiyo na wakati sasa umefika wa kukamilisha Azimio hili kwa kulridhia rasmi ili tuondokane na kuwa katika nchi ambazo hazijaridhia na kuonekana kwamba tunaunga mkono uwepo wa silaha hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ameonyesha umuhimu wa kuridhia mkataba huu ni uwezekano wa kupata ile misaada mbalimbali . Naungana naye mkono, nimezitaja faida ambazo tutaweza kuzipata, zote ni muhimu sana na ni wakati sasa turidhie ili pamoja na kusaidiwa endapo janga kama hili litatoka na vilevile kuna kujenga uwezo wa watu wetu na kukabiliana na matatizo haya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunafanya tafiti nyingi zinazotumia vimelea hivi vyatanga bakteria na virusi na vikitoka nje ya maabara zinaweza zikasabisha hatari kubwa. Kwa hiyo, hawa watatusaidia kujenga uwezo wa wataalam lakini vilevile kuboresha maabara zetu ili tuweze kuondokana na majanga yanayoweza kutokea kwa bahati mbaya, sio kwa makusudi. Maana hizi silaha zinaweza kutumika kwa makusudi, lakini vilevile ajali zinaweza zikatokea kutoka kwenye maabara na kwa maana hiyo lazima tujenge uwezo wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushauri ambao umetolewa kwamba ukiacha Azimio hili tunalolizungumzia leo la *Biologically Weapons* na Sumu, vilevile kuna mikataba mingine ya *Chemical Weapons Convention* na *Nuclear Weapons Nonproliferation*, ule wa *Chemical Weapons* tulishausaini na kuridhia huu wa *Nuclear Weapon* bado upo katika mchakato. Ni mategemeo yetu kwamba yote hii ikishasainiwa na kuridhiwa basi Tanzania itakuwa moja ya nchi ambazo zinapingga kabisa matumizi ya silaha za maangamizi ya halaiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nitakuwa nimepitia karibu hoja zote zilizosemwa, nimekumbushwa tu kwamba waliochangia katika hoja yetu hii ni Wabunge tisa (9) ikiwemo Kamati ile ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani. Tunashukuru sana kwa maoni yao na ushauri wao na tunaahidi kuyazingatia yote yaliyoelezwa katika ushauri uliotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia  
Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia  
na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake wa  
Mwaka 1972 liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana Kamati kwa niaba ya Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri mliyofanya na ripoti mliyotuletea hapa, hata Wabunge wengine wamepata fursa ya kutoa maoni yao. Pia Wabunge wote waliochangia tunawashukuru kwa mawazo hayo maana yanaenda kusaidia kwenye utekelezaji wa Mkataba huu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu wataalam pia wako hapa na Mheshimiwa Waziri, tuwaombe sasa upande wa Serikali muangalie zile sheria kama zipo zinazokinzana na huu Mkataba ambao Bunge limeridhia, wataalam wazitazame ili hizo sheria Bunge lipate nafasi ya kuzibadilisha. Tunawatachia kila la kheri katika utekelezaji wa Mkataba huu. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Waziri wa Fedha na Mipango. (*Makof!*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja niliyoitoa asubuhi ya kuliomba Bunge lako Tukufu liweze Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwanza wewe mwenyewe kwa kuongoza mjadala huu vizuri, naishukuru sana Kamati ya Bajeti, Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti ambaye ndiye aliyasilisha hoja na ushauri wa Kamati, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, lakini pia mwakilishi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wachangiaji wengine watatu ambao kwa ujumla wameunga mkono rai

ya Serikali kwamba Bunge liridhie Azimio nililoliwasilisha.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikianza na Kamati ya Bajeti, tunawashukuru sana kwa ushauri mzuri na Serikali imeupokea. Tumesikia vizuri kwamba tuhakikishe panakuwepo uwazi, ubora na usahihi wa utolewaji wa taarifa za kitakwimu na matumizi yake, ni jambo jema. Tumeambiwa tuhakikishe kuwa shughuli za watakwimu zinazingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi na kwa kweli hili ndyo lengo hata la Sheria yetu ya Takwimu ya mwaka 2015 na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Kamati imetukumbusha kuweka mikakati ya kuondoa changamoto, hususani uhaba wa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa takwimu, ukosefu wa teknolojia za kisasa, kutofanyika kwa tafiti kwa mujibu wa kalenda ya utafiti, pamoja na upungufu wa matumizi ya takwimu za kiutawala. Pia, wametuushauri kwamba tuanze kufikiria kutenga rasilimali watu, nyenzo na fedha za kutosha kwa ajili ya taasisi hizi muhimu, ni jambo la msingi tunalipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa pia tuhakikishe mamlaka za takwimu, watakwimu na wote wa tasnia hii ulinzi wa maisha binafsi, lakini siri za kibiashara na watoa taarifa, vilevile kusimamia na kuhakikisha kuwa mkataba huu unahifadhiwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa kweli haya yote ni ushauri mzuri na Serikali imeupokea na tutayazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wachangiaji nao wametoa ushauri mzuri sana. Mheshimiwa Richard Mbogo naye ameungana na Kamati pia kwamba Serikali ihakikishe kwamba huu mkataba unahifadhiwa katika lugha ya Kiswahili. Hali kadhalika Mheshimiwa Adadi Rajab amesisitiza umuhimu wa Azimio hili na kwa kweli ameufafanua vizuri sana na tumepokea ushauri kwamba tuhimize nchi nyingine, Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ili nao waweze kusaini na kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hili tutalifanya kazi, kwa sababu kwa bahati nzuri, Tanzania ni Mwenyekiti wa Kamisheni ya Takwimu Afrika na tutatumia nafasi hii vizuri kwa ajili ya kuwashawishi wenzetu. Pia amesitisiza lile la kuiwezesha *NBS* kwa maana ya fedha na watu. Kadhalika Mheshimiwa Obama ameeleza vizuri sana malengo ya Mkataba na kuyafafanua vema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hoja ambazo zilitolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani kwanza, walieleza kwamba wanashangazwa tumekaa miaka tisa baada ya kulisaini na baadaye ndipo tumeliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio hili ili liweze kuridhia. Napenda nitoe tu taarifa kwamba ilikuwa ni muhimu sana kwanza tuweze kutunga ile Sheria yenyewe ya Takwimu ya mwaka 2015. Kama nilivyoeleza Tanzania siyo nchi pekee ambayo haijardhia mkataba huu na nafikiri hili la kutunga sheria ilikuwa ni muhimu, la msingi ni kwamba kawia lakini ufile. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa pia kwamba baadhi ya taasisi hazina nguvu na badala yake zinategemea maelekezo kutoka juu. Hapa napenda nisisitize tu kwamba, Ofisi Kuu ya Takwimu inazingatia misingi na kanuni za uzalishaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu kwa mujibu wa sheria lakini kwa kuzingatia taaluma na weledi na hakuna maelekezo kutoka juu ambayo ni kinyume cha hiyo misingi. Kwa hiyo, hawana sababu ya kuwa na wasiwasi, si kweli kwamba tunategemea maelekezo kutoka juu. Kupata maelekezo kutoka juu yanazingatia misingi ya sheria lakini uweledi wa kitakwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na hoja kwamba Benki Kuu ya Tanzania inatakiwa kutoa Taarifa za Hali ya Uchumi na wadau wanalamika taarifa hizo hazitolewi kwa wakati au hazitolewi kabisa kwa umma. Napenda niseme kwamba hili siyo kweli, taarifa za Benki Kuu zimeendelea kutolewa kila mwezi lakini pia kila baada ya miezi mitatu na miezi sita na zimeendelea kutolewa na isipokuwa pale ambapo pana sababu mahsus. Kwa mfano,

kulikuwa na kipindi tulihitaji kufanya *reconciliation* ya takwimu za biashara za kimataifa na pale ndiyo taarifa ilichelewa. Hata hapa mkononi nina *Economy Bulletin* ni ya *quarter* ambayo inaishia Juni, 2018. Kwa hiyo, taarifa zinaendelea kutolewa lakini pia taarifa hizi zinawekwa kwenye tovuti ya Benki Kuu na wananchi wote wanakaribishwa kuitembelea na wataona taarifa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa pia kwamba Sheria ile ya Takwimu pamoja na Sheria Makosa ya Mtandao zimekuwa mwiba mkali katika kudhibiti vyombo vya habari pamoja na uhuru wa wananchi kutoa maoni. Nisisitize tu kwamba sheria hizi pengine ni mwiba mkali kwa vyombo vya habari ambavyo vinavunja sheria lakini si vinginevyo. Hoja niliyowasilisha ni Azimio kuhusu Mkataba wa Takwimu wa Afrika na pengine siyo kuhusu marekebisho ya sheria ambayo ilikwishardhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kambi Rasmi ya Upinzani ilisema Sheria ya Huduma kwa Vyombo vya Habari ni mwiba kwa wanasiasa wa upinzani kwa kupewa mashtaka ya uchochezi. Naomba nirudie tena kusema kwamba wanasiasa wanaotumia takwimu za mfukoni au za uongo ili kuweza kusogeza ajenda zao mbele za kisiasa, kwa kweli hawa wataendelea kupata tabu tu, tunawaomba wazingatie sheria iliyopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilielezwa kwamba pengine Serikali ina wasiwasi katika masuala ya takwimu na uwezekano mkubwa kwamba takwimu zinatolewa na *NBS* zina upungufu ambapo haitakiwi Watanzania wafahamu. Uwezekano wa takwimu zinazotolewa na chombo hiki muhimu kuwa na upungufu ambao hautakiwi kuonekana kwa Watanzania hayo ni yakufikirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kipindi cha mwaka 2006 - 2017, takwimu zinazotolewa na *NBS* zilikuwa na *second best* katika Afrika baada ya Afrika ya Kusini na hii ni *assessment* iliyofanywa na Benki ya Dunia, hata siyo sisi. Kwa hiyo,

niwahakikishie kabisa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba takwimu zetu zinazotolewa na *NBS* ni za uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na madai pia kwamba baadhi ya wadau wa maendeleo wametishia kuondoa fedha za misaada ya kibajeti. Hayo matishio sijayaona na mimi ndiyo Waziri wa Fedha. Tunao utaratibu pia nchini ya *Development Cooperation Framework* ya wadau wetu wa maendeleo kutoa taarifa na hakuna taarifa kama hizo Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani walieleza kwamba Serikali pengine ni vyema iwasilishe Sheria nyingine ya Takwimu na kufuta ile ya 2015 na marekebisho yake ya mwaka 2018. Kwetu kama Serikali bado hatujaona sababu ya msingi ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na mchangiaji Mheshimiwa Kubenea ambaye alitoa hoja mbalimbali. Napenda ni sisitize kwamba kwanza Azimio nililowasilisha tunaliamini kabisa na kile kifungu cha 24(a) na (b) ambacho alisema kina lengo la kuzuia watu kufanya utafiti mbadala, siyo kweli. Sisi tunachosema ni kwamba ukitaka kufanya utafiti basi ufuate utaratibu ambao umeelekezwa na sheria. Sisi tunachotaka ni kujiridhisha na misingi, kanuni na malengo ya utafiti. Hatutaki tafiti za upotoshaji au zile ambazo zitakwenda kwa namna yoyote kuhatarisha usalama wa nchi yetu kiuchumi, kijamii wala kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilidaiwa pia kwamba nilinukuliwa kwenye mitandao, nawasihii sana Waheshimiwa Wabunge hii mitandao muiangalie sana. Hakuna mahali popote katika nafasi yangu nimelelegeza masharti, ilidaiwa kwamba nililegeza masharti ya ile Sheria ya Takwimu baada ya kukutana na *World Bank*. Siwezi kuthubutu kulegeza masharti yaliyowekwa na sheria iliyotungwa na Bunge hili. Tulipokutana na *Vice President* wa *World Bank* kule Indonesia nilimfafanulia malengo ya marekebisho tuliyofanya hapa Bungeni. Nilimshawishi pia anaweza akatuma wataalam

wake walete michango yao wakati tunaandika kanuni za kutekeleza marekebisho ya sheria ile. Kwa hiyo, hakuna mahali ambapo nilllegeza masharti ya sheria liyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri la mwisho nililosikia lilikuwa kwamba tunawazuia kutoa takwimu mbadala. Sisi tunasema kwamba ukitoa takwimu mbadala kinyume cha matakwa ya Sheria ya Takwimu basi hapo utakuwa unakinzana na sheria ya nchi na utashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena naomba kukushukuru wewe, Kamati ya Bajeti na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani na wote waliochangia kwenye hoja niliyoitoa asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maeleo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liweze kuridhia Azimio la Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba  
wa Takwimu wa Afrika liliridhiwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri walioifanya ya kupitia, siyo tu ule mkataba lakini pia na mambo mengine

na wamefanya tafiti nyingi kwa kadri ya taarifa waliotuletea hapa Bunge na hata Wabunge wengine tumepata fursa ya kuchangia. Tunawashukuru sana Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambaao wamechangia katika maeneo mbalimbali na baadhi ya maeneo huenda yakawa ni maeneo ambayo Sheria yetu ya Takwimu itatakiwa kuangaliwa. Kwa upande wenu Serikali muangalie kama kuna sababu ya kuileta ile sheria Bungeni kama kuna vifungu vinavyokinzana na mkataba huu ambaao leo Bunge limeazimia kuuridhia. Kwa hiyo, niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa mkataba huu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mambo mengine lakini uko wasiwasi uliokuwa unaelezwa na Wabunge kuhusu sheria zinazotungwa kwa ajili ya utekelezaji wa maazimio kama haya. Kuna aina mbalimbali za utekelezaji huo, unaweza ukaweka kwenye sheria yako mwenyewe, ukaweka vifungu vya mkataba fulani ama ukautengenezea sheria tofauti.

Kwa hiyo, kwa upande wa Serikali waangalie kama mikataba hii miwili inahitaji sheria tofauti kuletwa hapa Bungeni basi muilete ili kuwe na maana kuridhia kwa mikataba hiyo. Ikiwa mnataka kuingiza vifungu vilivyopo kwenye mikataba hii ambayo Bunge imeridhia kwenye sheria zilizopo pia mfanye hivyo, kama hizo sheria hazina vifungu hivi. Itaturahisishia Wabunge kujua kwamba kazi tunayoifanya ya kuridhia mikataba hii siyo tu inaletwa tukisharidhia inakaa lakini mnaifanyi kazi.

Kwa hiyo nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na ratiba yetu, mtakumbuka tuliletewa orodha ya ziada kwa hivyo, tutaendelea na huo utaratibu wetu. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**AZIMIO**

**Azimio, Azimio la Bunge la Kumpogeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada na Maamuzi mbalimbali ya kuwainua Wananchi Wanyonge hasa Wakulima wa Korosho na Wakulima wa Mazao mengine.**

*(Hapa Wabunge walishangilia kwa makofi na vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mbunge anayetaka kuleta hoja hii Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungao wa Tanzania na Katibu wetu wa Bunge, nikushukuru wewe binafsi, nimshukuru mama yangu, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama na uongozi wote wa Bunge katika kuhakikisha kwamba Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada na maamuzi mbalimbali ya kuwainua wananchi wanyonge hasa wakulima wa korosho na wakulima mazao mengine linapata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la bei ya uhakika wa mazao mbalimbali katika nchi yetu lilikuwa limeota mizizi na kuendelea kuathiri maendeleo na ustawi wa wakulima wetu hapa nchini. Mathalani tatizo la kukosekana masoko na bei nzuri ya mazao mbalimbali limekuwa likilalamikiwa na wakulima wenyewe wa mazao mbalimbali wakiwemo wakulima wa mazao ya mahindi, kahawa, mpunga, mbaazi, ufuta, alizeti, korosho na mazao mengine yanayolimwa kwa wingi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la bei ndogo ya mazao na ukosefu wa masoko ya uhakika limekuwepo hapa nchini kwa muda mrefu bila kuchukuliwa hatua madhubuti na dhati katika kubaliana nalo. Suala la bei ndogo za mazao wakati mwingine limekuwa ni mpango wafanyabishara wachache kuwadhulumu haki wakulima wetu wanaotumia jasho jingi katika kuzalisha mazao husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba katika uchumi wa soko unaoendeshwa na watu wachache wenye nguvu ya fedha upo uwezekano mkubwa wa baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa na uzalendo na hofu ya Mungu kutumia umasikini wa wakulima wetu katika kuwadhulumu haki ya kupata bei stahiki za mazao yao kwa visingizio mbalimbali ikiwemo kisingizio cha kushuka kwa bei ya mazao husika katika soko la dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu wa Serikali ya Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ametambua changamoto ya bei ndogo za mazao ya wakulima wetu na kuamua kuitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali. Mathalani, tumekuwa tukishuhudia Mheshimiwa Rais akitoa maelekezo na miongozo mbalimbali ya namna Serikali yake inavyopaswa kuwatafutia masoko wakulima wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu ameendelea kuchukua hatua mbalimbali za kupigania bei nzuri ya mazao ya wakulima wetu, hivyo basi, jitihada hizo zinaonekana na zinaleta faraja na neema kubwa kwa wakulima wetu hapa nchini. Mathalani juzi tarehe 12 Novemba, 2018, Mheshimiwa Rais wetu aliamua kusitisha ununuzi wa zao la korosho kwa njia ya minada baada ya kutoridhishwa na mwenendo mzima wa ununuzi wa zao hilo kwa bei zilizopangwa na wafanyabiashara. Mathalani, iliripotiwa kwamba msimu huu wa kilimo wa mwaka 2018 wafanyabiashara wa korosho walipanga kununua korosho

kwa bei ya Sh.2,500 kwa kilo, tofauti na bei ya Sh.3,500 ya kilo moja ya korosho ghafi iliyotumika katika msimu wa 2017. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais hakuridhishwa na mwendo wa bei ya zao hilo na kuamua Serikali kununua zote zilizozalishwa na wakulima wetu kwa bei ya zaidi ya Sh.3,300 kwa kilo moja ya korosho ghafi. Kwa kuwa uamuzi huo wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, umeweza kuokoa fedha za wakulima zaidi ya shilingi bilioni 160 za kitanzania, iwapo korosho hizo zenye ujazo wa tani laki mbili zingenunuliwa kwa bei ya Sh.2,500 bei ambayo ilikuwa imependekezwa na wafanyabiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi uliofanywa na Mheshimiwa Rais wetu umelenga katika kuondoa wakulima wetu katika minyororo ya unyonyaji, ulanguzi uliokuwa umekidhiri katika Taifa letu. Kwa kuwa uwamuzi huo utaleta tija kwa wakulima wetu na kukuza uchumi wa nchi, hivyo basi, kwa unyenyekevu mkubwa na heshima mbele ya Kiti chako naliomba Bunge lako Tukufu katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu, Kikao cha Saba tarehe 14 Novemba, 2018 liazimie na kutoa kwa kauli moja mambo yafuatayo:-

(i) Kumpongeza kwa dhati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na kuunga mkono uamuzi wake wa kusitisha ununuzi wa zao la korosho kwa bei ya kinyonyaji na kueleleza korosho zilizopo zinunuliwe na Serikali kuititia Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa fedha zitakazotolewa na Benki ya Kilimo kwa bei ya Sh.3,300 kwa kilo moja ya korosho. (*Makofii/Vigelele*)

(ii) Tuiombe Serikali kuchukua hatua za makusudi na za haraka kutafuta masoko ya uhakika kwa mazao mengine kama vile pamba, pareto, kokoa, katani, mahindi, mchele, kahawa, mbaazi, ufuta, alizeti na mazao mengine yote ya kimkakati yanayozalishwa kwa wingi katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iimarishe uwezeshaji wa wananchi kupitia utaratibu wa kuyaongozea mazao yetu kwa kuyachakata hapa hapa nchini na kuyapatia wigo wa ajira kwa vijana wetu na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwaomba Watanzania wakiwemo wafanyabiaashara, wakulima, wavuvi, wafugaji kuendelea kuunga mkono na kuipa tija Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ili iweze kutekeleza majukumu yake na kuwaleta maendelea Watanzania kwa ufanisi na kwa kasi ya haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza naomba niseme maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea kejeli nyingi sana, nimepokea...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu malizia hoja yako kwa sababu Kanuni zinataka usome ulichoandika, halafu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

Mheshimiwa Kingu, mengine utazungumza wakati wa kuhitimisha hoja yako. Malizia Azimio.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu wetu, Mtapewa fursa kwa wachache kuchangia azimio hili halafu baadaye tutaamua kama Bunge tunaliunga mkono au laa.

Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu wetu, ninayo majina kutoka kwa Uwakilishi wa Vyama vilivyopo Bungeni. Tutaanza na mchango wa Mheshimiwa Hassan Masala, atafuatiwa na Mheshimwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa kifupi sana juu ya Azimo hili la kumpongeza Mheshimwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mkulima wa korosho lakini pia nawawakilisha wakulima wa korosho katika Mkoa wa Lindi. Wilaya yangu ndiyo inaongoza kwa kiasi kikubwa kwa uzalishaji katika msimu uliopita na hata msimu tuliokuwanao. Kwa mara zote nilizosimama ndani ya Bunge hili, ajenda zote ambazo nimezitungumzia, hakuna hata siku moja nimeacha kuzungumzia korosho kwa sababu korosho ndiyo maisha yetu, uhai wetu na uchumi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiki ambacho kimejitokeza na kwa *Hansard* jinsi ilivyoturekodi wakati tunaizungumzia korosho, tutakuwa watovu wa fadhila kama tutashindwa kutoa neno la pongezi na shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Tano ambayo inaongozwa na Rais wetu mpPENDWA, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Maamuzi aliyoachukua ni mazito sana. Ni maamuzi ambayo yanaenda kuandika historia kwa wanyonge amba walikuwa wanapata shida katika nchi yetu hii na hasa wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niungane na mtoa hoja, kwanza kumpongeza kwa maono aliyo yapata, lakini pia niungane na wote amba wanaitakia mema nchi yetu kwa kumpongeza na kuendelea kumuombea Mheshimiwa Rais wetu maisha mema lakini pia maisha yenye upendo zaidi kwa wanyonge. Maamuzi aliyoachukua, ameyachukua kwa wakati na sisi tumeshauri, na mimi binafsi nimetumia namna nyingi kufikisha ujumbe kwa ajili ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru mengi ya maamuzi yaliyofanyika, binfo nimeshiriki kwa niaba ya wakulima kushauri na tumeona yamefanyiwa kazi. Hapa tunatoa neno kama wakulima, lakini pia tunaunga mkono juu ya ku-support mazao mengine ambayo pia Watanzania wetu walikuwa wanayalima ili nayo pia yaweze kupata utaratibu mzuri wa ununuzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilitaka nilzungumzie ni eneo la kupongeza uamuzi ambaa ameenda mbele zaidi, wa kutaifisha na kuchukua maghala yale ambayo kimsingi sasa hivi kama yanatumika kuwa maghala. Kipo Kiwanda cha Buko kipo pale Lindi Mjini, hawa wanunuzi au hawa watu wa *Lindi Farmers* walichukua wakawa wanafanya kama ghala tu, lakini kwa uamuzi wa Mheshimiwa Rais akisaidiana na wasaidizi wake, walichukua kile kiwanda na sasa hivi kinaenda kufufuliwa kwa ajili ya kubangua. Huu nao ni ukombozi mkubwa kwa wakulima wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hatua hii haitaishia hapa. Jana nimepata taarifa, Naibu Waziri wa Kilimo alikuwa ndani ya Jimbo langu, Nachingwea Mheshimwa Innocent Bashungwa, ameenda pia kukagua Kiwanda cha Mamlaka ya Korosho, Nachingwea. Tunaamini hiki nacho pia Serikali itaenda kutaifisha ili kukifufua kwa ajili ya kuendeleza na kuongeza thamani ya zao la korosho. Kwa hiyo, maamuzi haya na maamuzi mengine yote yaliyochukuliwa, sisi kama wakulima na wawakilishi wa wakulima tunawapongeza sana na tunampongeza Mheshimiwa Rais katika hili na tunamuunga mkono na tuko pamoja kwa niaba ya wakulima tunaowawakilisha hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo nilitaka nilichangie sasa pamoja na kupongeza, bado naomba nishauri maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumetumia korosho kama sehemu ya kuingiza kipato kwa wakulima na Halmashauri zetu, ziko baadhi ya tozo kwa mfumo wa

malipo ambao umependekezwa na umetolewa maagizo, Halmashauri zetu zitaenda kuathirika. Kwa hiyo, naomba mamlaka nyingine ziangalie namna ya kufidia kiasi kidogo cha fedha ambacho mwaka huu tungeenda kukusanya ili Halmashauri zetu ziweze kujiendesha na ziweze kutoa huduma katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani sisi tulikuwa tunakata shilingi 30/= katika kila kilo. Fedha hii tulikuwa tuipeleka katika kuchangia elimu. Tulikuwa tunajenga majengo ya madarasa na kuchangia nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu awamu hii hawataenda kukata hii fedha, basi tunaomba TAMISEMI, Wizara nyingine na pia Mheshimiwa Rais, aone namna ya kukaa vizuri na wataalam wengine ili tuweze kutoa mchango ambao utaenda kufidia pale ambapo tunaenda kupunguza. Halmashauri ya Nachingwea peke yake mwaka huu tutapoteza zaidi ya shilingi milioni 900 ambayo kimsingi katika bajeti ya kawaida tayari itakuwa tumeshayumba kuendesha Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niliona nitoe ushauri huu kwa wale wanaonisikiliza ili nao waone namna ya ku-*compensate* pale ambapo tunakwenda kupata *deficit* ya fedha ambayo tungeweza kuichangia. Yote sisi tunashukuru na kwa kweli tutaendelea kumwombea Rais wetu yaliyo mema ili aweze kupata maono zaidi ya kuwatumikia Watanzania, nasi tutaendelea kumuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masala, nadhani Serikali wapo hapa, pengine ni kujipa muda kwenda kusikia Mheshimiwa Rais alitoa maagizo gani hasa. Kwa sababu hakukataza watu wale kuweza kulipa, ila alisema fedha zao walipwe ndiyo wafuatiliwe na wanaowadai. Kwa hiyo, maana yake, hata hizi kama makubaliano yalikuwa ni

kwamba wanatakiwa kulipa, maana yake wakishalipwa ndiyo waambiwe wachangie.

Kwa hiyo, huo uelewa wa pamoja unaweza kuupata mkikaa pamoja na Serikali ili muone ujumbe wa kuupeleka kule kusini ili msiingie kwenye hiyo hasara unayoisema. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Godbless Lema ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi na kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, na mimi nichangie hoja iliyokuwepo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mtoto au mzaliwa wa mkulima wa korosho. Hakuna muda, iwe bajeti au wapi nisitaje neno karosho. Waswahili walisema ashibaye hamjui mwenye njaa. Kwa kipindi kirefu tangu tumepata uhuru, zao la korosho halikumfaidisha mwananchi ambaye ni Mtanzania. Walikuwa wanawapa wananchi shilingi 600 /=kwa kilogramu, lakini bado kuna tozo humo ndani na anapewa kwa wakati wanaotaka wao. Tumedhulumiwa vya kutosha, sasa tunasema basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, korosho kwa muda mrefu imeuzwa kwa shilingi 600/= mpaka shilingi 1,200/= mwisho; na walikuwa wanawalipa kidogo kidogo, siyo zote. Kuanzia mwaka 2017 niliuliza swalii la papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kuhusu tozo ndogo ndogo ambazo ni kero kwa wakulima. Tozo zile zilivyotolewa wakulima wa korosho walipata shilingi 4,200/= kwa kilo moja. Huu ni uchumi wa kumkomboea mwananchi hasa wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambaao wanalima korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa na fadhila kama haki hii wanayopata watu wa Lindi, Mtwara na Ruvuma nikanyamaza. Kwa faida ya nani? Mimi ni mtoto wa mkulima,

anapopata shilingi 4,200/= itamsaidia mkulima kupata shule, kumsomesha mwanawe na mwenyewe kujitosheleza kiuchumi na nchi yangu vilevile itapata tozo ndani yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, historia itabakia kuwa historia kuwa wananchi hawa walikandamizwa vyta kutosha, walikuwa na maisha duni, walidhalilika vyta kutosha kupita wafanyabiashara ambao hawakuwa na huruma na nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivi kwa maana, wao walikuwa wanununa korosho, lakini mpaka mwaka 2015 tulipata shilingi billioni 141 tu. Mwenyezi Mungu amesaidia, mwaka 2017 korosho imetuingizia shilingi triliioni 1.2; lazima tuseme ahsante. Shilingi triliioni moja hii ukiondoa shillingi billioni moja, ina maana tulikuwa na faida ya shilingi triliioni moja *point something*. Tutaendelea kuvumilia tukinyonywa mpaka lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tufunguke. Tusiangalie mambo wanayozungumza ya blah, blah, Mtanzania wa kawaida umekuja hapa kumtetea mkulima, hukuja hapa kuitetea nafasi yako. Kama umekuja hapa kumtetea mkulima, mimi na wewe tutaungana mkono. Ndiyo maana nimesisimama hapa kuunga mkono juhudzi za Rais, Mheshimiwa Dkt. Joseph John Magufuli ili aongeze bidii wananchi wa Mkoa wa Lindi, Mtwara, Ruvuma na wakulima wa korosho wazidi kufanikiwa. (*Makofii/Vigelegelii*)

**MBUNGE FULANI:** *Thank you very much! Thank you!*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, palitengenezwa mbinu chafu za kufunga viwanda vyote vyta korosho, hakuna ajira Kusini. Mkoa wa Lindi hatuna kiwanda hata kimoja, tulikuwa na viwanda viwili na vyote vilifungwa na wakafanya magodauni. Lindi tulikuwa tunaajiri watu 1,400. Kupata ajira kwa Mkoa wa Lindi kwangu ni faraja. Kama sitasema watajiuliza, wewe unataka kumuunga mkono nani

wakati sisi wenzako ndio tunaiunga mkono hoja hii iweze kutusaidia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanunuzi wa korosho hawakuwa na huruma na Watanzania, tulikuwa tunahitajika kupata miradi ya *Corporate Social Responsibility*. Hawakujenga shule, hawakujenga zahanati, hawakutupa maji, hawakutupa barabara. Kwa faida ya nani? Leo mtu ambaye hakusaidii hata kwa maji, unafaidika na nini? Nataka nilete changamoto kwa Wizara za Kilimo na Idara ya Masoko, walikuwa wapi wakichezewa namna hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu Idara ya Masoko wamefanya nini kutafuta soko la wakulima wa Tanzania? Wamefanya nini kutafuta soko la watu wa alizeti na soko la kahawa? Wamekaa wamebweteka, wenzetu wa Uganda wamejunga na Burundi na Rwanda, wako katika *African Improved Food Network*. Sasa hivi wenzetu wameruka juu kibiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa na sisi tutaungana na wenzetu tuweze kuwaokoa Watanzania. Kwa muda mrefu watu wakizoea biashara za kawaida kuona Watanzania ni maskini, hawana uwezo kujikomboa, wakati wa kujikomboa umefika, Tanzania tuendelee mbele na tusonge mbele na tutafanikiwa bila uoga. Tanzania yenye maendeleo inawezekana. Tanzania yenye uchumi inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Joseph Pombe Magufuli kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, asanteni sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa. Mheshimiwa Daimu Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema na Mheshimiwa Jaqueline Msongozi ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi leo ya kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maamuzi yake sahihi yaliyokuja kwa wakati kwa ajili ya wakulima wetu wa korosho katika mikoa yote mitano inayolima korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono azimio hili na ninampa pongezi kubwa Mheshimiwa Mbunge aliyetoa wazo hili kwa kuwa limekuja wakati muafaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa mwaka 2018/2019 wa korosho wakulima wa korosho wamepata adha kubwa ya kupata pembejeo. Kwa maana ya kwamba kutofika pembejeo kwa wakati walitumia gharama kubwa, mfuksa mmoja wa *sulphur* ulifika kuanzia shilingi 70,000/= mpaka shilingi 100,000/=. Kwa bei ambazo zilikuwa zinatolewa na wenzetu wanunuzi zilikuwa haziwezi kukidhi haja ya gharama zile ambazo zilikuwa zimetumiwa na wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uamuzi wa Mheshimiwa Rais umekuja wakati muafaka ambapo umemjali mkulima kukidhi haja ya gharama zote alizozitumia wakati anahudumia mikorosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuwa uamuzi huu umekija wakati muafaka kwa sababu kusimama kwa mauzo kwa takribani mwezi mmoja na nusu kungesababisha maghala mengi kuja, maana korosho isingeweza kutoka kwenye maeneo ya wakulima wetu kwenda kwenye maghala makuu ambako korosho zimejaa ambapo zilikuwa zinasubiriwa kununuliwa. Kwa kuwa manunuzi yalismama kwa maana ya minada, korosho zile zimerundikana na sasa hivi kuna uwezekano, muda siyo mrefu maghala yangeweza kuja na korosho na kukwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile wakati wa mvua unafika, korosho zile zisingeweza kusafiri kwa sababu mahali

pa kuhifadhi pasingekuwepo. Pamoja na hilo, mwaya wa wanunuzi wale wa kangomba walianza kujitokeza kwa sababu wakulima walishakata tamaa kwamba korosho zao mwaka huu hazitaweza kununuliwa. Kwa hiyo, nampongeza sana Rais kwa uamuzi huu kwa kutoa hii bei kwa sababu mkulima sasa amepata nguvu mpya na hataweza kushawishika kirahisi kuuza korosho zake kwa njia ya kangomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mawili/matatu kama ushauri katika maamuzi haya. Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ina wadau wengi ambao wanashughulika na biashara hii, hasa tukiangalia upande wa ukusanyaji wa korosho, korosho zinakusanywa kwenye maghala ya Vyama vya Msingi, zinasafirishwa mpaka kwenye maghala makuu. Kwa hiyo, korosho zinalipa zikiwa kwenye maghala makuu. Kuna gharama zillizotokana na kusafirisha korosho hizi na kukusanya ambazo zimechukuliwa na Vyama vya Msingi na Chama Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Rais aangalie wadau walioshughulika katika kukusanya korosho hizi wapate stahiki yao ili mfumo usisimame. Maana wasipolipwa wasafirishaji wa korosho hizi kutoka vijijini mpaka mwenye maghala makuu ambapo askari wetu ndio watakuwepo pale, usafirishaji unaweza ukasimama kwa maana korosho zilizobaki kule kwenye vijiji hazitaweza kufika kwenye maghala makuu. Kwa hiyo, hili waangalie wadau wa Vyama vya Msingi ku-cover zile gharama zao, waangalie wasafirishaji ambao wamesafirisha korosho zile kutoka kwenye vijiji mpaka kwenye maghala makuu kuweza kulipa fedha zao ili na wao waweze kuendelea na biashara ya kusafirisha korosho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nina pendeleko kubwa sana au ushauri kwamba Mfumo wa Stakabadhi kama nilivyozungumza, una maeneo matatu; mtunza ghalaa naye anastahiki yake. Kwa kuwa tumesema tunaenda kuwalipa wakulima shilingi 3,300/= na huyu mtunza ghalaa ambaye yupo kwa mujibu wa sheria amesajiliwa na

Bodi, ana Leseni za Maghala Tanzania, naye angalie aweze kufanya malipo yake kwa wakati ili wakulima, wale vibarua wanaoshusha na kupakia korosho waweze kupata stahiki yao na mfumo uweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naendelea kупонеza jambo hili, limekuja kwa wakati muafaka, tunaomba aendelee kutusaidia kwa wakulima wetu kwa namna moja au nyingine ili kupunguza machungu yao na kuweza kutoa jasho na kulima mazao yetu kwa ajili ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naiub Spika, naunga mkono hoja na Azimio la kumpongeza Rais. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana. Mheshimiwa Godbless Lema atafuatiwa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kuna mstari kwenye biblia unasema; "Makwazo hayana budi kuja, ila ole wao wawakwazao wenzao." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo ni halali kumpongeza Mheshimiwa Rais, mvumilie ni halali vilevile kumsema na kumkosoa Mheshimiwa Rais. Kama mtaanza miongozo hapa, maana yake hamjui uhalali wa pongezi. Pongezi maana yake kuna kukosolewa. Sasa mimi nitajikita kwenye kukosoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Rais haya mambo hayapendi, *I can guarantee you*. Ninyi ndiyo mnasababisha *frustration* kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli. Huwezi ukawa unatafuta Unaibu Waziri au Uwaziri kwa unafiki wa kiwango hiki. Huwezi! Utapata. Nilikuwa na-*consult* na Roho Mtakatifu nione utamtoa nani hapa, sijamwona, ila utapata kwa sababu umejua *tune*. Wewe...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema ongea na Kiti.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe na utaratibu wa kusikiliza. Usiibuke tu, yaani unalipuka kama gesi imewashiwa kiberiti! Sikiliza kwanza. Mheshimiwa Lema, ongea na Kiti, usiongee na mto hoja.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, biashara duniani inatengenezwa na vitu viwili, *demand and supply*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais angeweza kupongezwa kama leo kungekuwa na makampuni zaidi ya 1000 yanashindania kununua korosho, mahindi, kahawa na alizeti katika Taifa hili. Unavyoingiza Jeshi la Wananchi likachukue korosho wakati huna soko, *logistic* peke yake ya Jeshi kuchukua korosho kuanzia magari, kuanzia kutoa wanajeshi kambini kwenda kununua korosho, *logistic* peke yake inaleta hasara kubwa kuliko mapato Taifa ambayo inakwenda kupata. Kwa hiyo, una... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla umesimama, nataka kujua unatoa taarifa, utaratibu ama Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla taarifa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Muda wangu ulindwe sana Mheshimiwa.

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mchangiaji, rafiki yangu, Mheshimiwa Godbless Lema, kwamba ukisoma uchumi, huwezi kuangalia *forces* mbili tu, *forces* za *demand and supply*. Ni lazima... (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mimi pia ni mfanyakibashara, kwa hiyo, naongea ninachokielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lema alipokuwa anazungumza watu wote tulitulia kumsikiliza, hakuna ambaye anazomea wala kuzungumza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Mwakajoka, umekaa Kiti cha *Chief Whip* wa Upinzani. Kwa hiyo, wewe ndio unatakiwa kuhakikisha huku nyuma wanasiliza wenzao kama wanavyosikilizwa. Sasa wewe usiwe sehemu ya kunyoosha vidole na mikono. Msikilize hoja yake, usikilize maamuzi yangu, Mheshimiwa Lema atapewa nafasi ya kuzungumza. Tusizungumze wote kwa sababu sasa ukimzungumzisha yule, anakujibu wewe. Tunaelewana Waheshimiwa? Nadhani hilo ni jambo dogo sana kwa Kambi hii makini kushindwa kulifuata. Tutunze midomo yetu, tusikilize anayechangia.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yangu ni fupi tu kwamba katika kanuni za uchumi, ukiangalia *forces* ambazo zinaweza zikasababisha bei kupanda ama kushuka, ama kuwa *stable*, ama uchumi kuanguka ama kuinuka ama kuwa *stable* siyo tu *forces* za *demand* na *supply*. Wakati mwengine hutokea kukawa na *government interventions*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilipenda amalizie *theories* zote. Mimi ni *MBA (Major Economics na Marketing)*, so don't worry, naongea ninachokielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lema wakati anachambua kuhusu *forces* ambazo zinaweza zikaathiri

uchumi, asiishie kwenye *demand and supply*, afahamu pia kuna nyakati Serikali huingilia kati ili kuweza kuweka mambo sawa. Ndiyo maana kuna mifumo ambayo inasaidia kuweka *stabilization* ya uchumi kama *price stabilization fund*, nchi nyingine zinaweka mifumo ya kudhibiti bei, nchi nyingine zinaweka mifuko ya kununua mazao na kama Tanzania tuna NFRA ambayo inanunua mazao, inaangalia bei zinavyoenda, bei zikiharibika wanawenza waka-flood mazao kwenye soko na hatimaye bei ikawa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda apokee hiyo taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, akapambane kwanza na lile suala la *airport* la kuzuia magay ambalo limekushinda, ndiyo uje uongee jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ya kawaida tu. Mheshimiwa Paul Makonda aliongea kuhusu *homosexual*, huyu akatoa tamko, Mheshimiwa Mahiga akamkataa. Mpe taarifa kama hiyo kwanza Mheshimiwa Mahiga aliyesema jambo la *gaylinaruhusiwa*. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, ongea na mimi, usiongee na mchangiaji. (*Kicheko*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunachosema ni nini, ni kwamba Mheshimiwa Rais katika suala la korosho na mni-note leo, hii biashara inakwenda kuanguka kama kahawa. Biashara siyo nguvu, ni majadiliano. Haiwezekani Waziri Mkuu, juzi tumeona kwenye televisheni, kashapata wateja na Mheshimiwa Rais aliweka *deadline* kwamba saa kumi mwisho. Waziri Mkuu ametangaza hadharani; "nimepata wateja na wako tayari kununua tani zaidi ya 200,000. Mheshimiwa Rais anasema; "achana na hao wateja." Halafu anayemwambia sio Mheshimiwa Lema, ni

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayesimamia shughuli za Bunge za Serikali na Bunge. Anaambiwa, achana na hao, wanajeshi nendeni, mkachukue vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari yake ni nini? Wale Wawekezaji wanaona hiyo *mood* ya Kiongozi Mkuu wa nchi. Hamuathiri korosho peke yake. Wanaotaka kuja kwa ajili ya madini wanaona *mood*, kwamba siku hizi *policy* na sheria zinabadiishiwa hadharani. Haya ndiyo matatizo makubwa. Kusipokuwepo na msingi imara wa kusimamia *policy* na sheria watu hawatakuja. Kwenye kahawa hawatakuja kwa sababu watasema, Tanzania maamuzi yake huwa inafanya kwenye mikutano ya hadhara na kwenye lkulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wakati wa *Acacia*, hapa mkaja mkatumbia kwamba wamekubali wanalipa pesa. Leo Mwanyika yuko ndani, wazungu mmewaachia. Haya mambo mnayakosea. Namna nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais ni kumwambia ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huku kuna watu wenye maarifa sana na wenye akili sana. Uoga! Mnateetea ada, mnatetea chakula, mnaua misingi ya nchi hii kwa kutetea *school fees* za watoto wenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mtu anakuja anasema tunaweka Azimio la Kumuunga Mheshimiwa Rais mkono. Rais akikosolewa, ataongoza vizuri. Familia zinagombana, zinakosoana. Nanyi mko wengi, ndio Chama Tawala, hili suala limekosewa. Sasa tulipokuwa tunasema kwamba, leo magari yanakwenda kuchukua korosho, hakuna mteja, *godown* wapi? Maana yake unawaza *logistic* ya *godown*, *logistic* ya magari; haya, ukishapata unawaza kutafuta mteja kwenye *whatsapp*. Mteja akipatikana, unawaza kupeleka melini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini ilikuwa rahisi nini? Waziri Mkuu, hao watu waliosemwa wanununa...

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Taarifa apewe mdogo wangu jamani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, muda wako unalindwa. Mheshimiwa Vuma.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Lema, kwamba soko la korosho lipo; na soko la kwanza la korosho ni Watanzania wenyewe. Zitabanguliwa... (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Safi sana. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sikiliza.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ni walaji wazuri wa korosho. Zikibanguliwa, watanunua na kutumia vizuri. Kwa hiyo, *primary market* ya korosho ni Watanzania wenyewe. Ahsante. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Ndio. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huyo nimekunyuwa naye chai jana kantini. Kama kuna mtu alikuwa analalamika, haki, nakwambia kama kuna mtu alikuwa analalamika, ni huyo. Uuuh! Ayayaya! Huyo! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekunyuwa naye chai yule nakwambia. Kama kuna mtu alikuwa analalamika kwamba Mheshimiwa Rais anakosea, nchi inaenda mputa mputa ni huyo. Sasa mimi siamini. (*Makofi/Kicheko*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, turudi kwenye hoja. Ni hivi, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba hali ya korosho itakuwa mbaya. Tunachosema ni kwamba hata kama Mheshimiwa Rais anao mkakati wa kuongeza thamani ya bei ya korosho, mkakati huo lazima uende na *consensus* ya wafanyabiashara wa kimataifa. Kwa sababu kwa nini korosho ni muhimu kwa Tanzania? Kwa sababu ya *forex*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Taifa hili kwenye mambo mengi tumeyumba. *Tanzanite* kule imeyumba, kwenye kahawa, miaka ya nyuma mimi nikiwa mdogo wakati wa Mheshimiwa Lyatonga, Wachaga waliamua kukata kahawa zote kwa sababu ya mambo ya haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndiyo nasema Waheshimiwa Wabunge pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais na siyo kila kitu anachofanya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ni kibaya, hapana. Ila kuna wakati nia njema ikikosa busara inazaa dhambi na ubaya. Kwa hiyo, nia njema ili iweze kuzaa busara, ni lazima niwe *bold* kumwambia ukweli. Umwambie Mheshimiwa Rais hii hapana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi, najiuliza, Mwalimu Nyerere angekuwa kama ninyi, ambaye ndiye mwanzilishi wa Chama hiki cha Mapinduzi, nchi hii kweli ingepata uhuru kweli! Eeeh, huyu Mheshimiwa Kingu aliyeleta hii hoja, yeye ndio angekuwa ni Mwalimu Nyerere, sasa hivi angekuwa anaishi Marekani na Taifa hili bado lingekuwa bado liko chini ya wakoloni. Mwambieni Mheshimiwa Rais ukweli. Tengenezeni hadhi ya Waziri Mkuu. Waziri Mkuu akiweza kuwa *blasted* hadharani, wewe Waziri utafanywa nini? Utapata wapi *confidence* ya kufanya *decision?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametafuta watu, ameleta. Mheshimiwa Rais angesema tu kwamba jamani, hawa wafanyabiashara walioikutana na Waziri Mkuu, tuonane Ofisini Ikulu, tunywe chai, tuongee. Biashara ni *talking*, siyo mabavu. Biashara haiendeshwi kwa matamko. Natoa siku tatu! Kwani mnauza ini ninyi? Mnauza moyo? Mnauza figo? Nisiponunua korosho, nakufa? Nisiponunua korosho, ni damu? Kwa hiyo, biashara *m-negotiate*, bwana unataka nini? Jamani niongezeni hiki. Hakifai, kwa sababu gani? Hivi ndivyo biashara duniani inaendeshwa. (*Makofi*)

Mheshimimiwa Naibu Spika, mtu wa kwanza kuonesha mahusiano mema na wafanyabiashara wa ndani na wa kimataifa, lazima awe mkuu wa nchi. Mkuu wa nchi akikosa hiyo *attitude* watu watakimbia. Ndiyo maana leo ukiangalia majarida mbalimbali duniani wanaisema Tanzania kama sehemu mbaya ya uwekezaji duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namwambia Mheshimiwa Waziri hapa, kuna matamko tu yametoka, Arusha *cancellation* ya watalii ni ya kutosha, kwa sababu ya tamko tu. Kwa hiyo, *statement* ya kiongozi wa juu kwamba Jeshi litafanya, madhara yake mengine ni nini? Tukianza kuingiza Jeshi kwenye shughuli za kisiasa na za kibiashara, wanajeshi watatamani kuwa Watawala. Wakitamani kuwa watawala, yatakuja kutokea mambo yaliyokuwa yanaisumbua Nigeria siku za nyuma. Nawe unayetaka Uwaziri na Unaibu Waziri, endelea kuomba lakini pongezi kama hizi, bora upeleke nyumbani kwako. Hapa kwa watu wenye akili, usishiriki. (*Makofi/Kicheko*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lema. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mambo mengine, nimefurahi Mheshimiwa Lema alivyosema Rais

anaweza kuita watu kunywa chai Ikulu. Maana hapo juzi kati tu ameita watu kunywa chai Ikulu, watu wakaanza maneno. Kwa hiyo, ni halali yake kabisa na Mheshimiwa Lema kasema. Kwa hiyo, chai zinanyewa Ikulu jamani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, nilimtaja pia Mheshimiwa Ezekiel Maige. Hawa wote watafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Haonga. (*Makofi*)

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa naunga mkono hoja. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza kwa makini sana kaka yangu Godbless Lema, katika yale aliyokuwa anasema, jambo moja tu nimeliona la msingi.

**MBUNGE FULANI:** Changia ya kwako.

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mengine nimesikia ni kelele tu na kulalamika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naomba kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais ambaye kimsingi nasimama hapa nikiwa najivunia kabisa kuwa na Rais wa aina hii. Ni Rais ambaye anatembea katika tabia hii. Kwanza kabisa ana hekima, ana busara, ana umakini, ni mchapakazi, ni mzalendo, mwenye weledi na uthubutu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana kwa uamuzi aliouchukua hasa pale ambapo kwa kipindi cha takribani miezi miwili, kumekuwa na wafanyabishara ambao

walikuwa hawana maamuzi sahihi, walikuwa wanaleta tu usumbufu; mara leo hivi, mara bei hii, wanachotaka wao. Kutokana na hilo, Mheshimiwa Rais amechukua uamuzi ambaao unakwenda kurekebisha jambo hili. Nami niseme, nimefurahi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi unapoona kwamba mambo hayaendi, kama baba mwenye nyumba, kwa nini usichukue maamuzi magumu? Utakalia *negotiation* na watu wenye usumbufu kwa sababu gani? Kama baba mwenye umakini na weledi na unajitambua, ni lazima uchukue maamuzi magumu. Ndiyo aliyofanya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. (*Makof*)

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo na kesho, wale wafanyabiashara watajifunza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, kuna taarifa. Mheshimiwa Vuma.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa mzungumzaji aliyejita katika kumwongezea tu, kwamba alichokifanya Mheshimiwa Rais ni sahihi na aliwaita Watu Ikulu kufanya *negotiation*, nao hawakukubali, lakini niweke kumbukumbu sahihi vizuri kwamba mimi sijakaa jana na Mheshimiwa Lema na wala sijakaa naye tangu nije hapa Bungeni. Ahsante. (*Makof/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, endelea na mchango wako.

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mheshimiwa Vuma nimeipokea vizuri sana.

Mheshimiwa Nailbu Spika, tunashuhudia uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa kwenda kununua korosho tani zaidi ya 200,000 ambayo inakwenda kuwafanya wakulima wetu wa

Mikoa ya Kusini sasa, wanakuwa na amani, lakini watakuwa wamefanya uwekezaji mzuri kwenye korosho, uwekezaji wenye tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Mungu aendelee kumpa maisha marefu. Pia, nimwambie tu Mheshimiwa Rais wangu, kwamba asikatishwe tamaa na watu wa aina hii. Ukitaka kumtambua mtu aliyeokoka, utamtambua kwa matendo, lakini pia ukitaka kumtambua shetani, utamtambua pia kwa matendo yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, humu tumechanganyika, lakini kupitia matendo, utatuju humu ndani kwamba wako walilokoka na wako wanaokwenda na nyendo za shetani. Nasema haya kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais tulipokuja na hoja ya makinikia, bado watu walijitokeza kupinga hatua nzuri zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais, lakini pia tuliwashuhudia watu wakipita kwenye *ma-corridor* ya Morena kule wakipanga mikakati mbalimbali, hao ndio watu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niseme tu, siku moja nitakuja kuwataja hapa, tuliwaona kule Morena, wanafanya vikao ambavyo vilikuwa vinatengeneza mazingira ya kuzuia maamuzi ya Mheshimiwa Rais juu ya makinikia. Kwa hiyo, jambo lolote zuri linalofanywa na Mheshimiwa Rais, wako watu ambao hawapendi wako watu ambao hawalifurahii kwa sababu wana ajenda yao ya siri na ni madalali wa shughuli ambazo wao wanazijua, ni madalali wa matumbo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuja na hoja hapa ya *Stiegler's*, walismama watu hapa wanapinga *Stiegler's* isifanyike. Tunao humu, tunawafahamu. Tumekwenda kwenye suala la *standard gauge*, nalo halikadhalika. Juzi, tumekuja na mpango, wamekuja na suala la Katiba humu ndani. Mtawajua kwa matendo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe ushauri katika Wizara ya Kilimo na Idara zake zote. Mheshimiwa Rais, jana ameapisha Mawaziri, ni juzi nadhani...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge upande wangu wa kushoto, upande unaoanza hapo kwenu tu mpaka huku, wakipiga kelele mnazozipiga saa mwenzenu anachangia, sijui kama humu ndani tutaelewana. Tuwe na utamaduni wa kusikilizana, ninyi si mtapata fursa ya kujibu kwani kuna taabu gani?

Mheshimiwa umetoka kutajwa hapo, Mchungaji unavaa Kola siku nyingine, tafadhali. Waumini wako ukiwa wewe unazungumza nao wanazungumza inakuwa vipi? Heshimu mamlaka, ndiyo tunavyofundishwa na biblia ambayo tunasoma wote, heshimu mamlaka. Mimi nazungumza, huwezi kuzungumza.

Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kaa chini tafadhali. Naomba ukae. Unapiga kelele, naomba ukae. Mheshimiwa Msigwa naomba ukae; naomba ukae, naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Toka nje Mheshimiwa Msigwa, toka nje.

**MBUNGE FULANI:** Mtoe nje, mtoe nje.

**NAIBU SPIKA:** Nenda nje. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa nenda nje, *out*. Hebu, *Sergeant at Arms. (Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Mhe. Mch. Peter S. Msigwa alitoka ukumbini)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Magereli, makofi yametosha. Mheshimiwa Jaqueline Msongozi. *(Makofi/Kelele)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawaambia kila siku watani zangu, someni alama za nyakati, naendelea. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kama ifuatavyo; Wizara ya Kilimo, nataka niwaambie Mawaziri ambao wamepewa dhamana juzi katika sekta ya kilimo nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri hakikisheni mnamsaidia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa, msaidieni sana, pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanafanya kazi kubwa msaidieni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nataka niseme kwamba mmeona changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta ya kilimo, simameni imara nendeni mkatatue changamoto zilizopo kwenye eneo hilo. Mimi niseme kwa kuwa sekta ya kilimo inagusa moja kwa moja maisha ya watu, na ndio maana imesababisha kumekuwa na mambo haya kadha wa kadha yaliyotokea siku mbili hizi, kama hamtakuwa makini, mimi nasema tu kwamba ningekuwa karibu sana na Mheshimiwa Rais ningemwambia afyekelée mbali, awafyekelée mbali hao ambao hawatasimamia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sasa ninaendelea...

**MBUNGE FULANI:** Muda

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ... wewe si ndiye unayepanga muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, ndugu zangu wapendwa wakati umefika msome alama za nyakati

na kwamba pandeni gari la Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Gari hili lina kasi ya maendeleo, uchumi, utafika mapema na utafika ukiwa salama 2025. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme maneno yafuatayo, ujumbe mnono kwa Mheshimiwa Rais wangu *yaya gete, vava vaikuipandika fresh, vakwipandika fresh, nhananhana*. CCM oyeee. (*Makof*) **[Hapa Alitumia Lugha Kisukuma]**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pascal Haonga atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kusema kwamba kazi ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali, dniyo kazi ya Bunge hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitika sana kuona Waheshimiwa Wabunge wanaipongeza Serikali badala ya kuishauri na kuisimamia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kama kwa mfano Heche ana mtoto wake anaitwa Grace akienda kumnunulia gauni halafu unaanza kusema tumpongeze Heche kwa kumnunulia mtoto wake gauni, huo ni udhaifu wa hali ya juu sana. Hayo ni majukumu yake kuyafanya namna hiyo na si kumpongeza pongeza. (*Makof*)

Kwa hiyo niwashauri Wabunge wenzangu wa pande zote mbili bila kujali itikadi ya vyama vyetu, kumpongeza Mheshimiwa Rais ni kumuharibu na kutomwambia ukweli kwamba Mheshimiwa Rais hapa unakosea. Kwa hiyo, mimi naomba tu kwamba tujikite katika kumshauri Mheshimiwa Rais na si kumpongeza kama ambavyo tunafanya mahali hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais ameonesha kitu ambacho kwa

kweli mimi kama Mbunge sikutegemea, ameonesha ubaguzi wa hali ya juu sana; ameonyesha ubaguzi kwa wakulima mbalimbali walilioma mazao yao kwa mfano wakulima wa mahindi, kahawa, pamba, mbaazi, tumbaku... (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaraibu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo mazao yote nchi nzima hali ni mbaya kweli kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip* ni taarifa ama utaratibu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara naomba ukae.

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Nina Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Lakini taarifa yangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuomba utaratibu wa kikanuni kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a) Mbunge ye yote anapotoa ndani ya Bunge taarifa na mchango wowote hatatoa taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, anachokifanya Mheshimiwa Haonga hapa ni kulidanganya taifa na kulidanganya Bunge. Anamtuhumu Mheshimiwa Rais kwamba ameonyesha ubaguzi wa hali ya juu, si kweli. Kwa wale wote waliomsikiliza Mheshimiwa Rais siku ile ametoa maagizo na akayataja mazao kadhaa ya chakula na biashara ndani ya nchi na kuagiza watendaji wa Serikali wahakikishe kwamba mazao hayo yote yanatendewa haki na masoko yanapatikana na akatoa mfano mzuri tu tena kwenye kesi ya mahindi akaeleza uwepo wa soko Malawi na akaagiza lifanyiwe kazi. Pia kaagiza Mawaziri na watendaji kwenye suala kama la mazao ya zabibu akaagiza lifanyiwe kazi. Alitoa mfano wa Bodi ya Pamba kwamba nayo ijiandae katika kuhakikisha inasimamia vizuri zao la pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezi kuvumilika Mbunge akatumia nafasi ya kuchangia humu ndani na kutaka kupotosha ukweli ambao upo dhahiri na kwa mtu ye yote aliyemsikiliza Rais anajua kabisa hakubagua mazao yoyote katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kutoa fursa ya Wabunge wengine kuchangia sikusudii kurudia aliyo yasema Mheshimiwa Jenista, lakini amesimama kwa mujibu wa Kanuni 64(1)(a) akiturejesha hapo kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, na kwamba Mbunge anapochangia pamoa na kwamba anao uhuru wa mawazo na Katiba Ibara ya 100 inamlinda, hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Haonga wote tumemsikia, sina haja ya kurejea aliyo yasema lakini kuzungumza kwamba Mheshimiwa Rais analeta ubaguzi, taarifa hizo ni lazima ziambatane na taarifa rasmi, tuwe tunamjadili hapa Rais kwamba sasa ameanza kuvunja Katiba. Kwa sababu hoja hiyo haipo mbele yetu ya kujadili mwenendo wa Rais, Mheshimiwa Haonga tafadhali unapoendelea na mchango wako jielekeze

kwenye hoja bila kusema Rais ni mbaguzi, kwa sababu siyo mbaguzi na hapa hatuna hoja ya kujadili mwenendo wa Rais ambao ndio ungeweza kuleta hizi hoja zote pamoja. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Haonga naomba ujielekeze kwenye hoja yako, lakini usitoe tuhuma kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu Kanuni ya 64 imetaja mambo kadhaa ambayo hayaruhusiwi humu Bungeni. Kwa hiyo, hizo tuhuma unazozieleza kuhusu Mheshimiwa Rais kwa kuwa hayupo kwenye hoja ya mjadala wa mwenendo wake haiwezi kuletwa kwa njia hiyo wakati wa kuchangia hoja hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Haonga tafadhali jielekeze kwenye mchango bila kuonesha kwamba mwenendo wa Rais ukoje.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme tu kwamba hapa ambacho nakizungumza ni kwamba mazao yote nchi nzima mahindi, mbaazi, kahawa na karibu mazao yote hali ni mbaya, bei iko chini sana. (*Makofii*)

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Kama Serikali leo imeanza kufanya biashara...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara nilikukalisha kuhusu taarifa kwa sababu kama ulikuwa unatazama Mheshimiwa Tunza Malapo alisimama kwa ajili ya taarifa na nilimzuia kutoa taarifa yake. Kwa hiyo, sasa hivi watakaosimama kwa ajili ya muda na wachangiaji bado nipo nao hapa ni wale wanatukumbusha kuhusu kanuni zisivunjwe.

Kwa hiyo, kuhusu utaratibu wataruhusiwa kusimama, taarifa nimezikataa, ahsante sana Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** (*Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

**NAIBU SPIKA:** Hawakusikii kwa sababu *mic* nimeizima, kwa hiyo hawakusikii. Mheshimiwa Haonga endelea na mchango wako.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahindi leo ninavyozungumza hapa, Mkoa wa Ruvuma kule anapotoka Mnadhimu pale debe ni shilingi 2,000/= hadi shilingi 2,500/= na gunia ni shilingi 15,000/= hadi shilingi 18,000/=. Mwaka mmoja na nusu uliopita debe moja la mahindi ilikuwa shilingi 18,000/= na gunia moja ilikuwa zaidi ya shilingi 100,000/=. Wananchi wetu wameshindwa kuuza mahindi yao mwaka jana, hayo mahindi hadi mwaka huu yapo lakini Serikali hatukuona ikiinuka kwenda kununua mahindi ya wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambako robo tatu ya chakula kinachozalishwa katika nchi hii kinatoka Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Songwe, Katavi, Iringa na maeneo mengine, leo Serikali kama ilikuwa na dhamira njema ingeanza na wakulima wale wa mahindi ambaao wallingia hasara mwaka jana. Wakulima wa korosho walitaka kuingia hasara mwaka huu, lakini mwaka jana walipata faida. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kiongozi wetu Rais wa nchi hii hatakiwi kupendelea upande wowote ule mimi nadhani kwamba angeanza na wale waliotangulia kuingia hasara. Ninavyozungumza na wewe mbaazi ni shilingi 80/= kwa kilo, lakini mbaazi mwaka mmoja na nusu uliopita mbaazi iliuzwa kwa shilingi 2,000/= kwa kilo moja. (*Makof*)

Kwa nini sasa huyu Rais tunayemsifia leo hapa asiende kuagiza mbaazi zikanunuliwa kwa wakulima wa mbaazi ili aweze kuwaondolea hasara? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa iliuzwa kilo moja shilingi 4,000/= na kitu mwaka jana, hivi ninavyozungumza

na wewe kahawa inauzwa shilingi 2000/= na kitu kwa kilo moja. Kwa nini kama Rais kweli ana nia njema asiende kununua kahawa hiyo kama ambavyo inafanya kwenye korosho? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumbaku imejaa kwenye maghala iliyolimwa msimu uliopita na hii ya sasa, hali ni mbaya, lakini leo unakwenda kwenye zao moja na ndicho nilichokuwa nakizungumza hapa, sikuwa na nia mbaya kwamba sasa Serikali kama ina nia njema kuanzia sasa itangaze kwamba mazao yote kuanzia kesho itaenda kuyanunua na kama haitafanya hivyo bado dhana ya ubaguzi haiwezi kuachwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba labda kitu chako kinisaidie neno zuri ambalo tunaweza kulitumia ni lipi kuacha mahindri kwenda kwenye korosho, utanisaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu Bunge letu hili. Mimi nadhani bajeti na mipango yote inapitishwa na Bunge. Leo kama Mheshimiwa Rais ameagiza korosho inunuliwe yote hatukupitisha Bungeni kujadili, fedha zinatoka wapi na Serikali itapataje faida, ndiyo kazi ya Bunge hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mimi nashauri Bunge au muhimili huu ikiwezekana tu ufutwe kabisa kwa sababu hauna kazi. Kwa sababu kama Rais anaweza akasema fedha zipo zipelekwe, kazi ya Bunge imeisha, maana yake Bunge limenajisiwa. Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni lazima tuwe wawazi, tumepokwa mamlaka ya kusimamia na kuishauri Serikali na tumepokwa mamlaka ya kutunga bajeti, tunaidhinisha bajeti kwa ajili ya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu vizuri kwamba kama kuna jambo limejitokeza kwenye Wizara fulani kungetokea *re-allocation* ingekuja Bungeni hapa kujadili na tukaweza kukufanya kwenye korosho. Leo Rais anakuwa yeye mwenyewe ndiye Bunge ndiye anapitisha bajeti mwenyewe na anaamua kila kitu. Sasa haya mambo ndiyo mambo

ambayo Lema alikuwa anazungumza hapo kwamba Bunge hili na nchi hii inawezekana pamekuwa ni mahali pabaya ya kuishi ni kwa sababu tumeshindwa kuisimamia na kuishauri Serikali. Wakati huo huo badala ya kumwambia anapokosea sisi tumekuwa tukimpongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina nia mbaya lakini kuna muda mwingine ukiona mtu anapongeza wakati mwingine hata Rais kuna muda mwingine akafika mahali labda akasahau kuvali viatu kwa bahati mbaya kuna mtu atasema umevaa viatu vya bei nzuri kwa sababu anaogopa kumshauri Rais. Kwa hiyo, naomba haya mambo tuwe makini sisi kama Bunge, kwa hiyo Bunge lisipokwe mamlaka yake.

Jambo lingine, ninaomba niseme tu kwamba Serikali ya CCM haijawahi kuwajali wakulima wa nchi hii hata mara moja, na hii wote tumeona mtiririko wa fedha usioridhisha. Kwa mfano, mwaka 2016/2017 fedha za maendeleo kwenye Wizara ya Kilimo zilizokuwa zimetengwa zilikuwa bilioni 100.5 na fedha zilizotolewa ni takriban bilioni mbili. Bajeti ile kwenye fedha za maendeleo zilitkelezwa kwa asilimia 2.2 na unapozungumza kilimo maana yake unazungumzia na wakulima wa korosho... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge wakati tunaendelea na hii michango ya hii hoja nadhani wote tuiisikia wakati ikisomwa hapa, ni vizuri kuwa tunaipitia pitia kwa sababu inazungumzia korosho lakini inayo mazao mengine, kwa hiyo, tuiweke vizuri ili wakati tunahojiana hapa tuwe tumeelewa tunahojiana kuhusu nini. Kwa hiyo, ili twende pamoja tuiipitie hii hoja siyo ndefu sana.

Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige. (*Makofii*)

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, na mimi napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa yaliyotokea na pili kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi aliouchukua. Waswahili wanasema mpinzani wako akikusifia ujue una matatizo, lakini ukiona anakulaumu ujue kuna mambo umeyafanya vizuri na ndiyo maana mimi sishangai majirani zetu upande wa pili hawataki kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu aliyoyafanya ni mazuri kwa wananchi hasa wanaolima korosho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda kuchukua fursa hii kuunga Azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoshughulikia zao la korosho na mikakati iliyowekwa kwa mazao mengine, lakini nilipenda niongeze na zao la zabibu mionganoni mwa mazao ambayo yamependekezwa na lenyewe liingle. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais hakuwanusuru wakulima wa korosho tu, ameunusuru uchumi wa Tanzania. Mwaka jana korosho imeingiza pesa za kigeni dola milioni 542, maana yake imeongeza hata thamani ya shilingi yetu na ni zao namba moja lilioongoza kuingiza pesa za kigeni, inashinda mazao matano ikiwemo pamba, tumbaku, chai pamoja na kahawa na karafuu kwa pamoja bado korosho imesimama namba moja. kwa hiyo, uamuzi huu ni wa busara kwa mustakabali wa uchumi wetu kwa ujumla, lakini pia kwa mustakabali wa wananchi wa mikoa inayolima korosho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu amesema kwamba Mheshimiwa Rais ana ubaguzi, nataka niwakumbushe kwa wale ambao wameingia Bungeni pamoja na mimi au zaidi ya mimi; mwaka 2008 tulipata mdororo wa uchumi na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ilisaidia kwenye mazao ya pamba na kahawa. Labda tofauti ambayo ninaiona ni kwamba mwaka 2008 tuliwawezesha wafanyabiashara ambao walinunua pamoja na vyama vyaya ushirika, sasa hivi tumewapa wanajeshi. Labda 2008 kuna mifuko ya watu ilinufaika, mwaka huu wanaona hakuna

kitakachochungulia kwenye baadhi ya mifuko ya watu, hiyo ndiyo tofauti lakini suala hili limeshafanywa kwa pamba na tumbaku. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais hakuna alichokosea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanasema kwamba soko linaendeshwa na *demand and supply*, tunakubali, lakini mwaka jana korosho zilikuwa tani 331,000 bei ilifika shilingi 4,000/=, mwaka huu ni chini ya tani 300,000 tunakadiria kama tani 210,000, kwa maana ya *supply* imeshuka kwa nini bei ishuke? Sasa katika mazingira hayo Serikali lazima iingilie kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumelipa Jeshi, katika nchi nydingine wangeweza hata kwenda kutosa baharini lakini tu mradi wananchi wake umewalinda na soko umelilinda. Kwa sababu ukiwapa kwa bei ya kutupa mwaka huu na mwakani watataka kuja kwa bei ya kutupa, lakini kwa vile tunawanyima mwaka huu mwakani watakuja na adabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alikaa na wafanyabiashara wakamuomba kutumia Bandari ya Dar es Salaam akawaruhusu, wakaomba kupunguziwa ushuru wa Bodi ya Korosho kutoka shilingi 17/= mpaka shilingi 10/= wakakubaliwa, lakini bado wakarudi wakaenda kucheza mchezo uleule. Sasa mimi nawashangaa sana wanosema kwa nini Jeshi litumike. Wakati wa mafuriko Jeshi hatulitumii? Juzi MV Nyerere ilivyozama hatukulitumia Jeshi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu hili suala la korosho kwa sasa hivi ni dharura, mvua zimeshaanza kunyesha bado korosho zipo kwenye maghala mengine ambayo hayana ubora, ukichelewa ndani ya wiki tatu korosho zimepoteza ubora. Kwa hiyo, Jeshi ni lazima liingie na likafanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninapendekeza suala lingine kwamba katika miaka ijayo Serikali iingie makubaliano na Serikali zile ambazo zinakuja kununua

korosho katika maeneo yetu. Nchi ambazo zimepandisha bei ya korosho ni Uturuki, Uchina pamoja na Vietnam, nadhani hao tufanye nao makubaliano. Wanunuzi wengine wanakuja mtu na kaka yake na shangazi yake wanakubaliana bei kesho tukanunue shilingi ngapi, kwa hiyo, lazima tutafute njia za kuondokana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nirudie tena kuipongeza Serikali yangu kwa kile ambacho imekifanya. Niwashangae sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Kingu, na mimi Mheshimiwa Kingu kwa kweli nakupongeza, angesimama Mbunge wa kutoka maeneo yanayolima korosho wangesema eeeh, sasa kasimama Mheshimiwa Kingu wanasema anataka Naibu Uwaziri, mara Uwaziri, ina maana sisi tusichangie?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaombe jamani, mimi nazungumza kwa kwa niaba ya wananchi wa Mtwara, maamuzi ya Mheshimiwa Rais wameyafurahia na wanayapongeza. Habari ya kusema eti wananchi wanaogopa askari siyo kweli, ni uzushi, askari tumefanya nao shughuli nydingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuiomba Serikali yetu kujipanga, hasa bodi zetu za mazao, kwa kiasi kikubwa wamechangia kutufikisha hapa. Mwaka jana korosho imeuzwa mpaka shilingi 4,000/=, mwaka huu bei elekezi unakuja kuiweka shilingi 1,500/=; hasa ililenga nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na suala la mwisho ambalo ninataka nili...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Dakika moja Mheshimiwa Hawa, muda wako umekwisha.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipendekeze suala moja la mwisho, hakuna

mnunuzi aliyenunua korosho mwaka huu, korosho zilizonunuliwa hazifiki hata tani 4,000 na sijui kama wamezichukua. Tuiombe Serikali ihakikishe hakuna bandari inayoruhusu kupidishwa korosho kwa sababu hakuna korosho iliyonunuliwa, na hata hao watakaosema wanasafirisha njugu kwa Bandari ya Dar es Salaam, karanga, wakague hayo makontena isije ikawa korosho za kangomba wanataka kuzasafirisha kwa njia ya njugu. Kwa hiyo, korosho wanazo wanajeshi hakuna mtu mwingine kusafirisha korosho. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mheshimiwa Ezekiel Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nilitaka kushtuka kidogo kwa sababu ni kama mara ya pili unaniruka, lakini naamini kwamba ni sababu za kimsingi zilizosababisha hilo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze sana Mheshimiwa Kingu kwanza kwa kuliona hilli wazo na niseme tu kwa kweli hii tabia inayoanza kujitokeza ya kila mtu akitaka kusema wazo zuri lilihofanywa na Serikali basi anaonekana kwamba anatafuta Uwaziri, si jambo zuri. Tupeane nafasi ya kila mtu kueleza mawazo yake na kila mtu aeleze jinsi ambavyo ameguswa na jambo hilo, unaweza ukawa umeguswa *negatively* kama ambavyo unahisi, lakini pale ambapo Serikali na Rais amefanya mambo ya msingi ni vizuri tukatambua na kuheshimu kazi hiyo nzuri iliyofanyika. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa ya moyo wangu naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, maamuzi aliyyofanya nimeyatafakari na nimejaribu kuyaangalia katika vigezo vyote, yanakidhi vigezo vyta kijamii

(*social locus*), wananchi wake wanapata matatizo wanataka kudhulumiwa, lazima Mheshimiwa Rais aingilie kati. Yanakidhi vigezo vya kisiasa (*political locus*), lakini vilevile yanakidhi vigezo vya kiuchumi na pengine kwenye hili nitaomba niligusie kidogo kwa sababu kuna namna fulani ya uelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfumo wa soko kwa maana ya kuzungumzia bei kuwekwa na *supply na demand*, forces za *supply na demand* kama ambavyo kuna baadhi ya wazungumzaji wamezungumzia, uwekaji wa bei kwa mtindo huo mara nyingi huwa unakwenda hivyo kama nguvu za asili za soko ziko huru kufanya kazi yake. Katika uchumi, amezungumzia kidogo hapo Mheshimiwa Waziri, Dkt. Kigwangalla kitu kinaitwa *government intervention*. Mara nyingi pale katika mfumo wa soko kunapotokea kitu tunaita *market distortions* au *unfair competition*, vitu hivi vina-trigger *government intervention*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *unfair competition* inaweza ikatokea pale katika soko kuna mfumo unaitwa *monopoly*, au kuna kitu kinaitwa *duopoly* au kuna kitu kinaitwa *oligopoly* au katika mfumo wa soko hata kama washindani wengi, lakini wanapofanya kitu kinaitwa *collusion* au kitu kinaitwa *cartel*, katika mazingira hayo mfumo wa soko wa *supply and demand* hauwezi ukatumika kuweka bei iliyo halali kwa muuzaji. Katika mazingira kama hayo haipukiki kutokea *government intervention* na ndicho kilichotokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi wa kwamba kulikuwa na *market distortion* na *unfair competition* uko wazi kabisa. Mtakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitisha kikao cha wadau na Mheshimiwa Rais akashiriki, akawaeleza kanunueni korosho kwa siyo chini ya shilingi 3,000/=. Walipokwenda kununua wote tunajua kilichotokea kwenye ile minada ya korosho, waliyojiteze ni wanunuzi wachache sana na magazeti yaliandika bado soko lilikuwa limedoda. Bei waliyokuwa wakiongeza shilingi moja, shilingi mbili, yaani shilingi 3,016 ndiyo bei iliyokuwa kubwa kuliko zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kuwa wamepewa siku nne hawa wanunuzi, walijitokeza wanunuzi 13; na ndicho alichokisema Mheshimiwa Rais, kwamba hawa wanunuzi 13 ambao wako tayari kutoa bei zaidi ya 3,000/= kama walivyokuwa wameelekeza walikuwa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndipo hapo sasa unarudi kwenye haya mambo ninayoyasema ya *unfair competition, cartel* na *collusion*. Katika mazingira kama hayo ni lazima Serikali iingilie kati na ndicho Mheshimiwa Rais alichokifanya, ni haki yake na ni wajibu wake. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hiyo, Mungu ambariki sana na niwaombe sana viongozi wengine katika Serikali kwa maana ya Mawaziri sasa tumsaidie kama alivyoelekeza kwenye mazao mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo azimio lenyewe limesema kwamba mfumo huu wa kuanguka na kupanda kwa bei ya mazao hauko kwenye korosho peke yake. Ni kweli na mazao mengine yanaanguka bei nyakati fulani, lakini mimi natoka kwenye eneo ambalo wanalima pamba, wote ni mashahidi, baada ya kuanguka kwa vyama vya ushirika miaka ile pamba ikaanza kuwa inafanyiwa biashara na wafanyabiashara binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukifika kanda yetu takriban wote unaowaona wana fedha, *individuals*, wafanyabiashara wakubwa, wengi wao wanafanya biashara ya pamba. Kwa nini, ni kwa sababu wanifuafika na hizi *market distortions* na *market cartels* wanazofanya ambazo hatimaye wanamuumiza mkulima wa pamba, wanamuumiza mkulima wa korosho, wanamuumiza mkulima wa zao lingine lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira kama hayo mimi nataka kuomba sana, kama ambavyo Mheshimiwa Rais ameelekeza na hata pendekexo la azimio liliyosema, ni lazima taasisi za Serikali zilizopewa wajibu wa kusimamia bei kuanzia utafutaji wa masoko, bodi za mazao zifanye kazi yake vizuri. Ni lazima Wizara zinazohusika na biashara na

kilimo zisaidie katika kuboresha mazao yetu kwa maana ya kuchagisha au kuhamasisha uchakataji wa mazao yetu kwa ndani, lakini vilevile kuhamasisha na kuweka ubora wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nyakati pia mazao yetu yanakosa ubora. Kuna wakati tulipata *tender* ya kupeleka mahindi Sudani Kusini miaka ile, lakini mahindi yetu yalikosa ubora yalipokwenda kupimwa kwenye maabara, kwa hiyo ni lazima Wizara ya Kilimo iwe na maabara zinazopima mazao ya kilimo kama mahindi. Kuna wakati kuna mfanyabiashara mmoja alipeleka makontena 20 za mihogo China, zilipokwenda kupimwa zikaonekana hazina viwango, *infact* ikabidi yale makontena ayatupe, na wakampa dola 1,000 kwa ajili ya nauli ya kurudi. Siwezi kumtaja jina lake kwa sababu za kijamii, lakini ukweli ni kwamba wakati mwingine ubora wa mazao yetu unakuwa hausimamiwi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninataka tu niwaombe sana viongozi, kwa maana ya Wizara, wasaidie kutafuta masoko; waimarishe ubora wa mazao yetu, lakini kikubwa zaidi ni lazima wakulima sasa kupitia vyama vyao vya ushirika pia wasaidiwe kuanzisha mfumo wa kingabei (*price stabilization*)...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jerome Bwanausi atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ajiandae.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe

mmoja kati ya wanaoweza kuchangia Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wameeleza sifa za Mheshimiwa Rais, lakini moja ya sifa za Mheshimiwa Rais ni ujasiri na asiyelogopa kufanya maamuzi magumu ya kuwasaidia wananchi wake. Mheshimiwa Rais amejidhihirisha kwamba yeye ni ukombozi wa wanyonge. Mheshimiwa Rais sisi wote tunamfahamu, ni mkweli na hana hofu ya kueleza kile anachodhani kina ukweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka kwenye Jimbo la Lulindi, Wilaya ya Masasi na Wilaya ya Masasi ndiyo Wilaya ya pili kwa uzalishaji wa korosho nchini, Tandahimba ndiyo inaongoza, ya pili Masasi. Nataka tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Mheshimiwa Naibu Spika kwamba usiku wa kuamkia jana wananchi kila kijiji wamekesha kumshangilia Rais, wanaendelea kumshangilia na kumpongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyokuwa kwenye soko la zao la korosho ilikuwa ni tete sana. Kwanza wamechelewa sana kupata soko, lakini kwa utaratibu wa miaka mingi ya nyuma, wananchi wengi walikuwa wanadhulumiwa fedha zao hasa na wafanyabiashara ambao hawana nia nzuri na wakulima wale. (*Makof*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais kitendo alichokifanya ni cha ukombozi kwa wakulima wa korosho. Nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wengine waliosema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli haina ubaguzi wowote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia Mheshimiwa Waziri Mkuu akitumwa na Mheshimiwa Rais kwenda kushughulikia zao la tumbaku wakati ule hali ya soko la tumbaku ikiwa mbaya, lakini tumeshuhudia Mheshimiwa Rais akimtuma Waziri Mkuu kwenda kushughulikia zao la kahawa. Kwa hiyo kwa kweli wale wanaosema kwamba Mheshimiwa

Rais ni mbaguzi hata hao watakaowasikiliza baadaye kama kipindi kitarudia watawashangaa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo hiki cha Mheshimiwa Rais kuamua kulitumia Jeshi kwenda kufanya kazi ile ni kitendo sahihi kabisa. Jeshi letu lina kazi ya kutumika wakati wa vita, lakini hutumika wakati pia wa huduma za jamii, kwa hiyo yupo sahihi kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashangaa sana wale wanaobeza tunaotoa pongezi za Mheshimiwa Rais, nadhani kwa wakulima wa korosho wote wataendelea kuwashangaa na kutowaelewa wale wote wanaobeza kazi inayofanywa na Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amejikita kuvunja ukimya lakini pia kuvunja hali ya kutochukua hatua kwa kutoongeza thamani ya mazao yetu. Mheshimiwa Rais ameelekeza kwamba sasa korosho zianze kubanguliwa hapa nchini, huu ni ukombozi mkubwa na sisi Waheshimiwa Wabunge hapa ni mashahidi, hata ukienda kwenye *supermarkets* utaona bei ya korosho iliyobanguliwa kwa kilo ilivyo kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tulikuwa tunaongea sana na kupiga kelele kwa nini viwanda takribani saba ambavyo tulipata mkopo wa Benki ya Dunia vyote havifanyi kazi hivi sasa na wale wote ambao walisema watavichukua vile viwanda kwa ajili ya kubangua korosho wamevigeuza viwanda vile kuwa *godowns* na wanajipatia fedha kwa kuhifadhi korosho. Kwa hiyo, maamuzi ya Mheshimiwa Rais ya kuamua viwanda vile vichukuliwe na Serikali ili korosho ibanguliwe hapa nchini, ni lazima tuipongeze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na furaha sana wakati mwininge unaweza ukapunguza maneno ya kusema. Sisi wakulima wa korosho furaha tuliyonayo ni kubwa na mimi nasema tuongeze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nishauri tu, kwamba hii changamoto ambayo ameitoa Mheshimiwa Rais na hii aliyoelekeza kwa watendaji mbalimbali na Waheshimiwa Mawaziri ya kuanza kuweka mkakati mpya wa kutafuta mazao kwa ajili ya wakulima wetu iwe ni endelevu. Ametoa mifano mingi tu, wote tumemsikiliza kwenye hotuba, ameelekeza kuhusu mahindi na mazao mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye zao la korosho ni lazima sasa utaratibu wa upatikanaji wa pembejeo kwa wakati uweze kuzingatiwa ili uzalishaji wetu uweze kwenda juu, kama alivyosema Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, kwamba zao letu ndilo liliongoza kwa kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni.

Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba watendaji wote wanaohusika na kuhakikisha kwamba pembejeo inapatikana kwa wakati iweze kupatikana, lakini kuhakikisha kwamba soko kwa wakulima linapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kumekuwa na maelezo mengi kuhusiana na suala la kangomba, labda nitoe ufanuzi, wengine hawajui. Kangomba ni bakuli inayotumika kwa wafanyabiashara wa kati kwenda kununua korosho kabla msimu haujaanza. Sasa kama Serikali tukianza kuhakikisha kwamba soko linapatikana mapema, suala la kangomba litakuwa halina nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi, tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mariam Ditopile, atafuatiwa na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Kuchauka ajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais. Niweze

kuwaunga mkono wenzangu wote walio tangulia kuchangia kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutetea kauli yake ambayo tangu anaomba ridhaa kwa Watanzania alisema anakuja kufanya kazi kwa ajili ya Watanzania wanyonge. (*Makofii*)

Naomba ni-*declare interest* kama navyofanya kila siku nikiwa nachangia kilimo. Mimi ni mkulima na mfanyakibashara wa mazao ya kilimo, na kwenye korosho pia nimo kwenye biashara ya *ku-export* korosho nje ya nchi. Pamoja na kwamba mwaka huu sifanyi biashara, lakini namuunga mkono Mheshimiwa asilimia 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuelewe, yameongelewa mengi hapa, masuala ya uchumi, lakini Rais ndiye mlezi wa nchi. Kuna kitu kinaitwa *ad-hoc decision making*, maamuzi ya dharura kwa ajili ya maslahi mapana kwa ajili ya taifa letu. Kumetokea anguko la bei katika soko la dunia, sisi kama Tanzania tunafanya nini, Mheshimiwa Rais alianza kwa hatua ya kuwasikiliza *Stakeholders* wakiwemo wafanyakibashara. Kikao kile cha Mheshimiwa Waziri Mkuu kilichofanyika Mheshimiwa Rais aliacha shughuli zake na akaenda aliwasikiliza na wakamsikiliza, lakini ilipoenda kwenye utendaji makubalianao hayakuwa hayo, ndiyo maana amefikia hatua hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na tunaona kabisa kauli yake kwamba nitanunua kwa shilingi 3,300/= na nitamlipa mkulima mwenyewe mkononi. Kwa hiyo, lazima tuone tuko kwenye *situation* gani na maamuzi gani ya kututoa hapa tulipo, hizi ngonjera nyingine jamani tuziweke na tuwe na akiba ya maneno, mtaumbuka. Mliongea hivi hivi kwenye makinikia, lakini leo hii W izara ya Madini ndiyo inaongoza kwa kukusanya maduhuli, zaidi ya asilimia 100 wanakusanya hawa na maongezi bado yanaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi kwenye michango yangu huko nyuma nilikuwa nasema na niliponda sana kitendo cha Bodi ya Korosho kuleta miti ya mikorosho nchi nzima, nilisema *what is that?* Tukiwa bado hatujajidhatiti

sisi kwenye kuweka soko la uhakika tunaongeza *production*. Sasa leo hii *production* yenyele lakini bado soko lilikuwa linayumba. Kitendo cha Mheshimiwa Rais kuiacha na kuibangua korosho ni cha kishujaa, na hii mbegu wanaipanda tutaifaidi milele niwahakikishie tunaenda kuuza korosho iliyobanguliwa, sasa tutakuwa na soko, hatotegemea tena madalali. Hii *triangular* ya mzunguko mzunguko tunatoka hapa tunampata mfanyabiashara anakwenda India kwa mfanyabiashara mwingine akauze kiwandani ibanguliwe iende Marekani, *what is that?* Umethubutu Mheshimiwa Rais na utafanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nirejee kusema mmeongea sana! Ooh, ana ubaguzi. Mmesahau sukari vibari viliacha kutolewa kwa ajili ya kuingiza sukari ili kumlinda nani kama siyo mkulima wa miwa?

Nilisema tukishauri tushauri ukweli, tukikosoa tukosoe ukweli, tukipongeza tupongeze ukweli. Ndugu yangu uliyeleta hoja unapongeza ukweli. Tumeongeza Serikali kupitia Waziri Mpango wameongeza kodi kwenye mafuta yanayoingia tunaenda kumlinda nani, kama siyo mkulima wa mbegu za mafuta wakiwemo wakulima wangu wa Dodoma? Mtasema Rais ni mbaguzi? Kwenye kahawa tumeona na maeneo tofauti tofauti, hata kwenye mahindi mimi nimeathirika lakini aliyesababisha Mheshimiwa Rais amechukua hatua alilishwa tango pori. Narudia tena na mwenyewe ameuliza jamani kuna nchi ina bajeti ya kununua mahindi? Mbona hamtaki kwenda kuuza mahindi ya Watanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nisema knye hoja hii namuunga mkono anaenda kufanya *revolution*, anaenda kuleta mapinduzi kwenye zao la korosho, kwa sababu hili zao letu mmesema wenyewe limezidi mazao matano katika kuleta kipato tena cha fedha za kigeni. Kama tunakwenda kuliongezea thamani tatizo liko wapi? Kama tunaona tuimarishe ndiyo maana nikasema *ad-hoc*, tunatumia jeshi kwa sababu *its an ad-hoc decision making*. Ni dharura hii mvua zinakaribia ile nguvu jeshi ya kazi ni kubwa, kwa nini tusilitumie vizuri jeshi letu... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, tutamalizia Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa mtoha hoja ajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niungane na wachangiaji wenzangu katika kuunga mkono azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kusisimama hapa na kuweza kutoa wazo langu. Pamoja na kumshukuru Mwenyewe naomba nimshukuru mtooa hoja Mheshimiwa Kingu. Naomba nimshukuru kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu kwamba jambo hili ni jambo jema na mimi naungana naye mia kwa mia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Mheshimiwa Rais ni binadamu kama binadamu wengine anapofanya jambo jema ni lazima apongeze na katika hili wala tusiwe na neno la kumung'unya ni lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais ameweza kutenda jambo jema sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa Mheshimiwa Rais kabla hajachaguliwa kuwa Rais alitokana na Chama cha Mapinduzi, akiwa anaenda kupigiwa kura na wananchi alikabidhiliwa llani ya Chama cha Mapinduzi. Ndani ya llani ya Chama cha Mapinduzi ilieleza mambo mengi sana moja wapo ni kuwasaidia wanyonge na pia

kuhakikisha anatafuta masoko ya mazao likiwemo zao la korosho. Binafsi kwa kweli naomba nimpongeze sana na sina shaka naamini anaitendea haki llani yetu ya Chama cha Mapinduzi na sisi kama wana CCM na wale wote wenye nia njema wenye kuitakia nchi yetu nia njema ni lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia suala la korosho. Mimi ni sehemu ya wakulima wa korosho na mara nyingi nimekuwa nikisimama hapa kuzungumza matatizo wanayokumbana nayo wakulima wa korosho. Mambo mengi ambayo walikuwa wanakumbana nayo ni pamoja na mifumo mibovu, lakini kabla ya kufikia wakati wa kuuza katika mfumo rasmi wakulima wa korosho wamekuwa wakinyanyasika sana kupitia walanguzi.

Sasa kupitia jambo hili mimi sina shaka, ninaamini kabisa mimi pamoja na wakulima wa korosho wa maeneo yote tumefurahi sana na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na katika jambo wala hatutakiwi kutumia damu katika kumpongeza tutumie jasho tumpongeze Rais wetu ili aendelee kufanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuingiza pato katika taifa hili kupitia zao la korosho lakini pia wananchi wamekuwa wakinufaika sana kwa kutatua matatizo yao. Hivi tunavyozungumza hapa wananchi walikuwa tayari na sintofahamu kuhusu kama hizi korosho zao zitauzika lakini kwa uamuzi wa Mheshimiwa Rais wana hakika sasa watanunua batii, watasomesha watoto wao wataweza kufanya shughuli nyngine za kimaendeleo, pia wataweza kulima kilimo cha wakati kwa kupitia uuzaji mzuri wa korosho, mimi kwa kweli naomba niungane na wote katika kumpongeza Mheshimiwa Rais... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani kengele imeshagonga, ahsante sana.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa mimi naunga mkono azimio hili asilimia mia kwa mia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niseme kwamba nilishamuunga mkono Mheshimiwa Rais tangu tarehe 13 Agosti, 2018 nilipotamka kumuunga mkono, nilipopindua meza. Kwa kweli suala hili la kumuunga mkono pamoja na kwamba limeanzishwa na zao la korosho, lakini kama mwenyewe ulivyokuwa umelieleza Bunge lako tukufu kwamba tusome tujue azimio linaeleza nini kwa sababu kuna watu wengine ambao walijikita kwa lengo la kuja kupinga tu ndiyo maana hawakutaka kusoma wajue kwamba mazao mengine yameongelewa, na ndiyo maana wakaja na hoja kwamba kuna hoja ya ubaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mheshimiwa Rais hatuna sababu ya kuacha kumpongeza kwa jambo hili kubwa la kijasiri alilolifanya, na mimi tangu jana jioni mpaka leo hii nimepata simu nydingi sana kutoka kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Liwale, wakitafuta ni namna gani wanaweza kuonekana na wao wamemuunga mkono Mheshimiwa Rais. Mwisho kabisa wazee wa Mkoa wa Lindi na Mtwara leo hii wamenipigia simu wamesema bado wako kwenye tafakari ya kutafuta ni namna gani watu wa Kusini na watakuwa na zawadi gani ambayo watampa Mheshimiwa Rais ambayo hatoweza kuisahau na wao hawata weza kumsahau. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho mtu wa mwisho amenipigia simu amesema wanakusudia kunituma mimi niende kwa Mheshimiwa Rais ili nimwambie barabara inayotoka Mtwara – Tandahimba – Newala – Nachingwea – Liwale ipate jina lake ili iwe kumbukumbu ya kwao, kwamba

watu wa Kusini ili waone kwamba wamempa zawadi wanampa barabara inayotoka Mtwara – Tandahimba – Newala – Nachingwea – Liwale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini tumesema hivyo, ni kwa sababu zao hili la korosho linaloongelewa hapa leo miaka mitatu nyuma halikuwa na bei hii, lakini Mheshimiwa Rais tangu alipoingia zao hili limeonesha kufufuka, mpaka mwaka jana tukapata zao hili kwa shilingi 4,000/= . Kwa hiyo sasa Mheshimiwa Rais amejifunza, kwamba kama mwaka jana zao hili lilifika shilingi 4,000/= kweli zao hili linaonekana kwamba kweli kwenye soko kuna kuyumba, lakini kuyumba ambako kumeongelewa hakukufikia kiwango hiki na hao wafanyabiashara inawezekana ndio waliosababisha haya, kwa sababu ninyi mnakumbuka, Bunge hili tunakumbuka mwaka tumeambiwa korosho zetu tumekuta zina mawe zikiwa Vietnam, lakini kwa nini zile zikizokwenda India hazikukutwa na wawe? Jambo hili lilikuwa linaulizwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mambo Mheshimiwa Rais ametafakari ameona pamoa na kwamba hawa wamekubali hawa watu 13 kutoka watu zaidi ya 30, 40 walioingia kwenye soko mwaka jana, leo hii wamekubali hawa 13 akaona kwamba hapa kuna sintofahamu; amechukua uamuzi sahihi wa kufuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mzungumzaji mmoja hapa ameongelea mambo ya *logistics*, hivi kama *logistics* kuchukua jeshi na vyombo vyetu kusomba korosho *logistics* yake itakuwa kubwa kuliko wafanyabiashara, hawa wafanyabiashara walitaka kuzibeba korosho kutoka, Liwale, kutoka Mtwara, kutoka Lindi kuzipeleka Dar es Salaam kwa usafiri gani? Si kwa usafiri wa magari haya haya? Kwa nini kubeba Serikali *logistics* iwe ya bei ghali kuliko kubebwa na wafanyabiashara? Jambo ambalo haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, kuhusu matumizi ya jeshi. Mimi jana nimemsikia Mkuu wa Majeshi amesema huu, hii *operation* siyo *operation* ya kijeshi hii ni *operation* ya kutoa

huduma kwa wananchi, na moja ya mujukumu ya Jeshi letu ni wakati amani ambapo jeshi letu linataka kuhudumia wananchi kwenye majanga kama haya. Kwa hiyo mimi sioni matumizi ya jeshi kuwa ndiyo matumizi mabaya ya jeshi letu, mimi namuunga mkono Mheshimiwa Rais. Hata hivyo tu...*(Makof)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ilishagonga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mia kwa mia, ahsante sana.

**CCM oyee!!.. (*Makofi/Vigelegel*) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**WABUNGE FULANI:** Oyeeee!!..

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hayo maneno ya mwisho nimefuta, msije mkageuza mkuutano wa hadhara humu ndani itakuwa taabu. Mheshimiwa mtoha hoja, Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa tena ninaomba nilishukuru sana Bunge lako tukufu na Wabunge wote kwa hekima zao kubwa walizozionyesha kwa taifa kwa dunia katika kujadili hoja ambayo ilikuwa mezani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba niseme mambo yafuatayo, Taifa la Marekani Taifa ambalo kimsingi ndiyo linaloamini sana katika *liberal economy*; mwaka 2008 walipopata m dororo wa kiuchumi chini ya uongozi wa Barrack Obama Serikali ya Marekani ilitoa pesa *US dollar* trilioni moja katika kuviooka viwanda vya Kimarekani. Fedha hizi zilitolewa kwa makampuni kama *General Motors*. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo upotoshaji unaotaka kuletwa kwenye Bunge juu ya hatua ya hatua za kimkakati alizozichukua Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano katika kuwasaidia wakulima wa korosho, nimesikiliza hoja nygingi za wenzetu, ni aibu kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli tumekuja Bungeni kuwa sauti ya wanyonge, tunamuona kiongozi wa kitaifa akichukua *initiatives* ambazo angenyamaza kimya wanyonge wanyonge walikuwa wanakwenda kuumia, tunakuja hapa tunakuja kubeza na kuanza kutajana majina ya ajabu hii ni haibu kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nilikumbushe Taifa, mwaka 2008 ulipotokea mdodororo wa kiuchumi Tanzania Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete katika sekta ya pamba kama mnakumbuka na baadhi yenu mlikuwa watendaji wa Serikali, akina January Makamba, Mawaziri mmo humu, mlikuwa mnaandika hotuba za Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais Jakaya Kiwete alichukua hatua katika kuwanusuru wakulima wa pamba kwenye taifa hili, hii ndiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Wakati wowote panapotokea kitu kinachoitwa *invisible hand* katika *principle*, wachumi mko hapa, hakuna Serikali duniani itaacha kutumia *theoryya invisible hand* katika kuwa-rescue watu wake yanapotokea mambo kama haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanafanya ma-*cartel*, Mheshimiwa Rais amewaita watu wamezungumza lkulu wamehaidi kwenda kununua korosho, wanaondoka wamekwenda kiweka mgomo wa kununua korosho Serikali ya CCM itukanwe Rais atukanwe, Mheshimiwa Rais ameonesha ujasiri wa hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upotoshaji umezungumzwa hapa, watu wamesema Mheshimiwa Rais hajaleta bajeti Bungeni. Ndugu zangu ngoja niwaambie, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ndiyo imekuwa *bestowed* na jukumu la kwenda kununua korosho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niliambie Bunge lako Tukufu Serikali yetu *it's a non-profit making institution*, haifanyi biashara. Kitendo cha Mheshimiwa Rais kuikamisheni Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwenda kununua korosho nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Rais wetu ameshauriwa vizuri na ametumia hekima kubwa. Nitumie fursa hii kulipongeza Baraza la Mawaziri na Mawaziri wote na washauri wote wa Rais kwa ujasiri waliounesha na kufikia hatua hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nihitimishe kwa kusema, wengi wamekuja wametaja mazao mengi sana hapa. Nataka nikuambie maamuzi aliyoachukua Mheshimiwa Rais, amezungumza mdogo wangu Mariam Ditopile amenigusa sana, wakulima wa korosho wangeachwa leo msimu wa mvua wakati wowote utaanza, tafsiri yake ni nini wanaotucheka leo walikuwa wanataka waone Taifa letu likimeguka na kuingia kwenye matatizo makubwa, jambo ambalo macho ya makini ya Chama cha Mapinduzi na uongozi wake wameyaona na kuchukua hatua za haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize, mazao kama pamba korosho, tumbaku, kahawa, chai niliisahau, *these are the strategic cash crops* ambazo nchi lazima iyaangalie kwa jicho la karibu. Kwa hiyo, maamuzi yaliyochukuliwa na Mheshimiwa Rais sisi kama Bunge lazima tuyaunge mkono, lazima tumtie moyo Mheshimiwa Rais anapofanya maamuzi ambayo hata mimi mwenyewe sikutegemea kama Rais angefanya maamuzi ya namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo kwa heshima na tahadhima nikushukuru sana wewe binafsi nimshukuru sana Mheshimiwa Spika na Bunge lote, na Waheshimiwa Wabunge wote mlionchangia, hata mlionibea, mimi ninamapungufu yangu lakini mimi ni mtu wa Mungu, sina chuki na mtu. Kazi ya Kibunge niliyotumwa na wapiga kura wa Singida Magharibi ni kuja kuishauri Serikali ya chama changu na kuikosoa kwa staha, na kuipa compliment pale inapofanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana Mungu ibariki Tanzania, Mungu libariki Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi/Vigelegele*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji, na ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri, Waheshimiwa Wabunge nakala ya Azimio ile iliyokuwa imegawiwa ndiyo itakayoingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kwa sababu wakati wa kuzungumza Mheshimiwa Kingu kuna mahali alikuwa akiongeza maneno, sasa kwa mujibu wa kanuni zetu Taarifa Rasmi za Bunge zitachukua taarifa hii ambayo ni rasmi kikanuni. Kwa hiyo sasa nitawahoji kwa taarifa hii ambayo Mheshimiwa Kingu ameileta.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada na maamuzi mbalimbali ya kuwainua wananchi wanyonge hasa wakulima wa korosho na wakulima wa mazao mengine lilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge na mimi nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Kingu na wengine wote ambao ameshauriana nao kuhusu wazo hili, ni wazo zuri na mimi nichukue fursa hii kuungana nanyi kwa niaba ya Mheshimiwa Spika kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi

anayoyachukua na wakati mwingine maamuzi magumu lakini anaturahisishia kazi sisi kama Bunge maana humu ndani pangekuwa panakuwa padogo mambo haya yasipokaa vizuri. Kkwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi haya aliyoyachukua ambayo yanawapunguzia adha wananchi wetu hasa wakulima wa korosho lakini na wakulima wengine ambaao mazao hayo bado yanatazamwa. (*Makofii*)

Waheshimiwa wabunge baada ya kusema hayo nimuombe *Chief Whip*, kwa sababu yuko hapa, Serikali itusaidie kuwazitaarifu zile Halmashauri zilizopo kwenye maeneo wanayolima korosho kuhusu maamuzi ya Mheshimiwa Rais kuhusu makato kwenye zile bei wanazolipwa na Serikali. Ili wale ambaao wameagizwa kukata baada ya mkulima kulipwa, aliwaaambia wakamsubiri mahali, mimi ndivyo nilliyomsikia, lakini itarahisisha si kila mtu anakuwa na tafsiri yake. Serikali itoe tafsiri ya yale aliyoyasema Mheshimiwa Rais ili kule yanakowenda basi utekelezaji ufanane na yale ambayo ye ye alikuwa ameyaruhusu kwa ile kauli yake basi yakae kimaandishi na wale kule wapate ujumbe unaofanana kuondoa mkanganyiko kutoka Halmashauri nyingine kwenda halmashauri nyingine. (*Makofii*)

Kwa sababu hapo kuna mambo ya kodi tumesikia kuhusu michango hapa na pia kuna mikopo na yote nadhani aliyazungumza vizuri lakini ni vizuri upande wenu Mheshimiwa Jenista mtusaidie ujumbe uwafikie wananchi vizuri.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa ninalo tangazo moja linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kama ilivyokuwa imetangazwa wakati wa kikao cha *briefing* kesho siku ya Alhamisi tarehe 15 Novemba, 2018 baada ya kuhairisha Bunge kutakuwa na hafla yaani *cocktail party* katika viwanja vya sherehe vya Bunge pemberi ya Kituo cha Afya itakayoandalisha na uongozi wa Benki ya CRDB, mahususi kwa ajili ya kutambua ushirikiano wa kibiashara uliopo kati ya benki hiyo na Waheshimiwa Wabunge, pia kumtambulisha

mtendaji Mkuu mpya wa benki hiyo Ndugu Abduli Majidi Mussa Nsekela. Mgeni rasmi katika hafla hiyo atakuwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhehimiwa Job Yustino Ndugai, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki.

Aidha Waheshimiwa Wabunge mnaombwa siku ya kesho kutoegesha magari eneo la maegesho ya Wabunge ili kupisha shughuli za maandalizi ya hafla hiyo. Mnahakikishiwa kwamba kutakuwa na ulinzi wa kutosha katika yale maegesho ya sehemu ya nje ya upande wa pili.

Kwa hiyo magari yatalindwa vizuri, tupaki magari yetu kule kwa sababu hilo eneo la maegesho ya kawaida litakuwa likitumika kwa ajili ya maandalizi ya sherehe ambayo Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge siku ya kesho. (*Makofî*)

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Alhamisi saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.47 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 15 Novemba, 2018 Saa Tatu Asuhuhi)*